# (CKRC)

# VERBATIM REPORT OF

# CONSTITUTIONAL PUBLIC HEARING

# KINANGO CONSTITUENCY, AT KINANGO SECONDARY SCHOOL

ON

30TH MAY 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KINANGO CONSTITUENCY, HELD AT KINANGO SECONDARY SCHOOL, 30TH MAY 2002**

**Present:**

1. Com. Dr. Mohammed A. Swazuri
1. Com. Bishop B.N. Kariuki
1. Com. Nancy Baraza

**Secretariat in Attendance**

1. Mr. Apamo - Programme Officer
1. Mwero wa Mkalla - District Co-ordinator
1. Jacque Nyamoo - Verbartim Recorder
1. Egda Kagoni - Asst. Programme Officer.

Meeting opened at 10.00 a.m with Com. Dr. Mohammed Swazuri on the chair.

Natuombe, Bwana katika jina la Yesu tunakushukuru, tunakuinua, tunakutukuza kwa maana ndiye Bwana. Tunasema ni asante kwa siku ambayo umetuawadia Bwana tunakuomba Bwana. Tunakuomba Bwana ukaweze kutusaidia, yote tutakayosema ikaweze kutusaidia ikaweze kutoka rohoni mwetu na wewe Bwana ukaweze kuyatia mihuri Bwana. Mungu wangu ninakushukuru kwa sababu ya wapendwa ambayo umewaleta ndiyo tukayazungumuze ya kujenga nchi yetu ya Kenya Mfalme wa Wafalme Jehova ninakuomba roho wako aweze kututawala tusikuzungumze ya kimwanadamu lakini bwana yote itayatakayo ombewa iwe yatokana kwako ewe bwana Mungu tunaomba wale walio njiani Mungu tunaomba uweze ukawakaribisha na ndiyo tuweze kunena na kukubaliana mfalme wa mfalme kwasababu Jehova umesema ya kwamba pale wawili, watatu watakaosema utakuwa pamoja nao tunaamini ya kwamba bwana utatutembelea ninasimama kinyume na mipango na gombe zote za ibilisi shetani ambazo zinaweze kuja kuchangana mkutano huu katika jina la Yesu Kristo Mungu ukaweze kuonekana na ukatutangalie hata tunapomaliza tukamalize na wewe bwana tutakushukuru tutakapoona mapenzi yako na nguvu zako ni katika jina la Yesu Kristo tunaomba, tukiamini. Amen.

Asante sana bwana muhubiri, tuko na commissioner mama hapa Nancy Barasa tuko na commissioner mwingine hapa Bishop Bernard Kariuki na mimi naitwa Mohammed Swanzuri sote macommissioners, tuko na team yetu hapa wanaorecord hapa na hayo wengine hapa na tuko chairman wa ile kamati ya kikatiba ya Kinango Constituency iko hapa wachuvi wako hapa na wengine wengi, tuko na District coordinator Bwana Mweru kwa hivyo kila anayetaka kuutoa maoni tutampatia dakika tano. Tulifanya hivyo jana Saburu na tukapata zaidi ya watu mia mbili. Kwa hivyo tunataka mfuate utaratibu huo. Yule aweza kutoa maoni yake kwa kutoa memorandum ulioandika mswada ulioandika sasa ukiuleta mswada ule kama unataka kuotoa tu bila ya kusema tutauweka pale kwa bwana Apamo ata record au unataka ule mswada upitie kidogo utaka hapa tutakupatia dakika tano. Na sio kusoma kila mswada neno badaa ya neno. Itachukuakua muda mrefu. Tunataka utupatie mapendekezo ya ule

mswada. Na hata ukimaliza kuutaja hayo mapendekezo itabidi uandike tena pale. Au unaweza kutoa maoni yako kwa kusema tu hivi hivi na utuambie mapendekezo. Shida zote tunasinjua. Tufanye nini tuondoe shida hizo. Uzianze kutaja vile ambvyo tunateseka tumefanya hivi mapendekezo ni hivi. Shida ya shamba ni hivi tunataka hivi. Shida ya kitu fulani ni hivi tunataka hivi. Dakika tano tano tafadhali. Hatutapata horodha ilio andikwa hapa. Kwa hivyo alikuja hapa na anataka kutoa maoni na hanjaandika jina lake tafadhali aende pale inje kuna meza pale ataandika jina lake. Haya tutaanza na bwana Joseph Njiri Mwako. Itafika hapo?

**Joseph Njiri Mwako**: Mwenye kiti, macommissioners, wanachama wote wa tume ya marekebisho ya katiba nchini, wananchi wenzangu wa Kinago hamjambo. Kwanza nataka chukuwa nafasi hii kumshukuru bwana commissioner kunipa nafasi hii ili niwenze kuzungumza machache nakutoa mapendekezo yale ambao niko nayo. Kwanza zaidi nitaguzia upande wetu sisi walemavu. Walemavu tungependa katiba itakayokuja zaidi iwaweke walemavu katika mstari wa mbele haza zaidi katika serikali inayokuja na pia katika kila jambo katika kila maendeleo ye yote. Walemavu wawekwe katika mstari wa mbele. Hiyo ni moja.

Na pili, tungependelea haki iweko kati yetu na wale wananchi wengi wowote wa hali ya kawaida isiwe na hali ya utetanshi bali ikuwe na hali ambayo ingependelea sisi tuwe tunaona tuko sawa sawa na wale wenzetu wale wana viombo vyote. Tungependelea serikali ijao iwe serikali ya umoja wa kitaifa na iwe serikali ambayo kwa kweli haitabangua mtu awaye ye yote. Tungependelea serikali yenye amani. Serikali ambayo haitakwa na utafauti wowote mbali iwe serikali ambayo itakwa inapendwa na vizazi na hata vizazi. Tungependelea pia kuona ya kwamba haki inadumishwa za kibinandamu ata kwa upande wa mashamba, kwa upande wa adhi na upande wa hali ya kimasomo. Walemavu kwa upande wa masomo tungependela serikali ijao wapewe haki sawa upande wa masomo ili isiwe na ile hali ya kwamba watu wa kawaida wanaweza kusema kwamba hao wanaweza kutushida la bali iwe kuna hali ambayo tunaweza kusema ya kwamba wako katika mstari moja ama katika mstari ya mbele.

Mwisho, tungependela serikali ijao idumize zaidi na zaidi uhuru ya kuwabudu katika makanisa na pia katika misikiti ili watu wote wawe wanaweza kuwa na haki na uhuru ya kuwabudu katika makanisa wanayopendelea. Pia watu wawe na uhuru ama mKenya ye yote awe na uhuru wa kukaa mahali popote a napotaka bila kusumbuliwa bila kutatizwa na mtu yeyote.

Kwa kumaliza, ningependelea uchaguzi mkuu ujao uwe uchaguzi wa haki na wa kidemokracia kwa wa Kenya wote bila ubaguzi bila kubagua rangi au umbile. Ni hayo machache. Asanteni.

**Com. Barasa:** Atoe details chake pale tuenda kwa D. N. Thuo. Hayuko. A.K. Mundugu.

**Mundugu**: Asante sana mwenye kiti mimi naitwa Hassan Kombo Mundugu Nazera Mkangi. Nashukuru sana bwana mwenye kiti na wananchi wenzangu. Mimi ningependa maoni hivi, katika serikali ambayo naitarajia kuunda katiba mpya mimi binafsi

naunga mkono serikali ya majimbo. Na katika kifungu cha serikali ya majimbo ningependela upande wa local government irudishiwe mamlaka yote iwe shida zote ndogo ndogo tunapitishia wenye hapa Kwale kama ni shida ya mashamba, tunanjua tabu zetu na tupewe nguvu tunjue shida hiyo tutaimaliza wenyeweye hapa Kwale kule tupeleke tu recommendation. Ingine ni ya kuchangia ni kwamba katika serikali ambayo tunapendelea. Ningependelea hata dhuluma Duruma apate haki yake yote na kusema apate haki yote ni kwamba kuna vikongojo fulani ambazo mdhuluma Mduruma amenyefanya kama hana uhuru. Tukiingilia upande wa dini utapata dhuluma Duruma yeye ni mtu ambaye anakubali kwamba shehemu zingine ni tukufu na utapata Muislam sehemu ile huenda akeyehalibuakaharibu. Utapata epistle anaweza enda sehemu hiyo akaiharilibu pia kama tuseme sisi tuna sehemu zetu ambazo tunakubali kwamba during dry season sehemu ambayo kunaweza enda huko tukaoba mvua na tuna believe kwamba tukaiomba mvua inakuja. Lakini hao wandugu zetu huenda sehemu kama hizo wanasiharibu. Tungekubali kwamba dhuluma Duruma nafasi kama hiyo iwe sheria kwamba mtu ye yote ambaye dhuluma Duruma hii akubali kwamba sehemu hizo siwe sehemu zakuharlibiwa kwa binafusi ya kuomba Mungu wake. Dhuluma Duruma awe na haki kwamba siku ya juma ikubaliwe kwamba ni sheria ni siku ya kupumshika. Na kubali kwamba kuna sehemu zingine apapo abampo watu hawataki kufish. Yaani kuna special rivers ambazo we believe kwamba huwa na sort of fishing we do not get blessings from the Lord. Kwa hivyo tungesema hivi, sisi wa Nduruma vitu kama hizo ziwe sheria, Mkristo, Musliam akifish in those areas awe anaweza punished by the law. Kwa sababu kama Kivulugani there is a river, river Kindemi, yingine kwingine kuna there is a place known as Mwandudua. Mwandundua is a place where actually we believe wakati wa dry season you can just go there and pray our Lord and we believe that hapo mahali within short time tutapata mvua. Lakini hawa wa Kristo wamedhalau wamenda kule wakafanya opposite the way we believe. Kwa hivyo tungependelea hiyo iwe sheria. Muwislam akienda akifanya hivo, Mkristo akienda akifanya hivo tupewe nguvu ya kumstaki. Ombi langu lingine ningengependelea kwa sababu tuna mira mila tofauti tofauti na katika mira mila zetu tunaamani kwamba Duruma akilala na bibi ya mwenzake kuliwa mali. Kwa hivyo ni pendekezo langu tupewe nguvu na tupewe sheria ya kwamba these kangaroo laws zetu ambazo sikoziko huko ziwe sina zina nguvu zaidi kwa sababu tumeona kwamba sisi tukipatiwa hali ya Mdruma vile anaichi anaishi ambavyo akiondoka hapa akienda huko au akienda in the normal courts unapata kwamba Mduruma haki yake imewacshwa yuma kw a sababu sisi tunaamini kwamba kuna watu ambao wanapewa natural powers by Lord. Tuna wazee wetu ambao tuna amini kwamba mchawi anaweza kujulikana through kiapo na kuna watu ambao tuna amini kwamba ukienda pale tutaambiwa huyu ni mchawi, huyu si mchawi lakini tumeona kwamba kuna unyonge. Mtu kama yule apewe nafasi ya kutosha kwa hivo tungeomba korti kama kangaroo laws kama hivyo epewe ipewe uzitu zaidi ndiyo imefanya watu wa hapa kwetu utapata mtu anaenda kule alafu badaa ya hapo anasitakiwa tena polisi badaa ya hapo anaenda kule mambo yana bandilika na anakuakua hiyo ni makosa lakini sisi tuna amini kwamba those people have extra powers na we believe kwamba hata Mungu kuna watu ambaonye emewavolunter kwamba hao watu wa na powers hata ya kuzumgumza na ngombe. Kwa hivyo we believe mtu kama yule anaweza kutufanya tuwe na haki zetu cha ki Duruma.

Langu la mwisho, ili ningependelea Mduruma ambaye ainakunja awe ni mtu ananjua haki yake. Na kunjua haki yake ni kwamba anaweza kupewa mamlaka na serikali ya kuhakikisha kwamba mtoto, bibi yake;, bwana ndiye mwenye mamlaka. Haya mambo ya kwambiwa bibi na bwana wana haki sawa mapendekezo yangu ina sema kwa Mdruma hakuna. Asanteni.

**Com. Nancy Barasa**: Wewe Mduruma.

**Mundugu:** Ndiyo

**Com Barasa:** Na wewe Mduruma anajiona unajiona sawa sawa kama iko na Wakenya engiwengine? Ni Mkenya. Awa Awe anabaki tu Mduruma na bibi yake na hii nchi ingine hii Kenya kubwa hahuziki hahusiki nayo? Kenya Kubwa. Mduruma sio Mkenya?

**Mundugu**: No. Si kwangu.

**Com. Barasa:** Unajua tuna tunanjengancha katiba ya nchi inaitwa Kenya. Sio katiba ya Waduruma. Naonajione kama wewe ni mkubwa kuliko Mduruma pia.

**Mundugu:** Kwa kweli mama amejaribu kuniuliza swali na ningependelea kulijibu hili. Katika serikali huwa ina madaranja tofauti tofaoti kuna ngazi ya kutoka from the grassroot to the top. Kwa hivyo nikisema hivo ni na amini kwamba ili serikali ambao itachaguliwa naweza iweze kuwa kua ya majimbo, inawenza kuwakua serikali ya muungano, lakini ni nasema katika serikali hiyo hiyo Mduruma apewe nafasi hizo hizo kwa sababu tunaamini kwamba serikali haiwezi kuundwa na kabila moja. Lakini ni kwamba Mduruma nawe ananjisikia yuko huru. Asante.

**Com. Bishop Kariuki:** Umesema kwamba kina mama Wanduruma hawana haki sawa na wanaume. Sasa kuna mambo ambayo kina mama wanaumia kwa sasa ambayo inahitaji kutengenezwa na katiba au ungependa wakae vili vili tu walivyokuwa wakikaa.

**Mundugu:** Mimi nikiwa Mduruma nitakubali kwamba ni Mduruma na haki ya Mduruma lazima ikubaliwe. Ni kisema hivyo ni kwamba desturi hii ya kwamba bibi na bwana wawe sawa inachangia divorce na inachangia kwamba nyumbani hakuna peace kwa sababu sisi tuna amini kwamba bibi ni mtu wa kulea watoto na bwana ni mtu wa kutafuta. Na watu hawawezi kuma kuwa sawa katika nyumba moja. Na utaona kule mahalimali ambapo watu wamesemekana wako sawa there is a lot of divorce na ina encourage a lot of let us say sehemu kama hizo nimeona kama watu hawaishi vizuri hakuna heshima ndani yake.

**Com**. Register hapo. Mwachichi.

**Mwachachi:** Kwa jina ninaitwa Immanuel Siboya Mwachichiu na nickname ninaitwa Kundongo si Mujaluo lakini. Sio undongo Kundongo. Mimi ningetaka kuchangia point moja kwa katiba hii. Mimi nimefikiria sana kwa sababu Kenya ni moja na tunaoma tunaoma mambo yote inaenda sawa lakini tunaona hapa kwetu mambo mengine si sawa. Ni likukuaa nikomba

tume hii ikinja si ta lala siku hiyo nitakunja nitoe n\hiihaya maoni yangu. Maoni yangu insema ninasema hivi. Sisi tunategemea sana mifugo na mnazi. Katika hizi vitu viwili tunategemeaama sisi hapa singine zingine zimekwenda kama hivi sasa hakuna mifugo kama vile zamani. Imembakia ni mnazi. Mnazi watu wengine wanatambua kama mti wa pwani lakini mnazi ni wa Kenya nzima. Ninashangaa ama ni naomba tume hii wakati imekutana kwamba mnazi hapa kwetu unasumbiliwa. Pombe. Natoboa kabisa leo. Nasema hivi tunaona mtu akibeba mnazi au anazisaidia mnazi anashikwa. Na hali ni kinywanji kama zile zingine za Kenya. Na watu wale wengine hawashikwi. Ni likua likua nanjiuliza ni kwa nini. Siku ya katiba ni lini nitaisema. Kwa hivyo leo nimekunja kuwambia tunataka mnazi iwe uwe free Kenya yote. Si hapa Kinango peke yake. Ama itumike kama vinywanji vingine tunafanya katika Kenya hii.

Langu lingine la pili, ni juu ya ardhi. Ardhi nasema hivi nilipozaliwa mimi hapo Kingango niliambiwa hi ardhi ni ya serikali kuu. Nampaka dakika hii ninaambiwa hii ni ya serikali kuu. Hiyo serikali kuu kutoka hapa Kasasa sijaiona. Na waona watu wale wale na kama ni wale wale tunaomba serikali inayokunja afanye ifanye mpango itugawanyiwe watu wa Kinango hii ardhi. Kila mtu awe na mahali pake, mana kila mtu anakunja anakunja na barua ambaye ni serikali kuu. Na hiyo si serikali kuu ni mahali nimepozaliwa nilipozaliwa mimi. Kwa hivyo ningependelea Kinango igawanywe.

**Kessy:** Mimi naitwa Arindi Augustus Kessy. Bwana mwenye kiti sitazungumza mengi lakini nitazungumsza kidogo. Mimi ni juu ya pension. Kila mara tunaona mishahara yaoengezwa na katika macommission hizi hata juzi juzi nilukuwa nasikia commission ilitanja mambo ya watu walioretire waongezwe kitu lakini miaka twende nenda miaka kwenda rudi hatuoni kitu kama hizohiyo. Na sisi pia ni watu tuna mafamilies na kitu hata ikongiongezwa si hutuongezwi na wengineo wengineo. Sijui hua aje. Ndiyo nataka nielewe.

La pili, mimi labda ni na bibi anafanya kazi nami pia nafanya kazi. Mmoja wetu akienda anapewa kitu kidogo mpaka hata haiweze haiwezi kumaliza miaka mitano na huko tuna watoto wamebaki hapa. Kwa nini hiyo miaka mitano isiongezwe mpaka wale dependants hawa wakapata zo zote mpaka wa kamalizika. Kwa mfano siku hizi kuna ugonjwa wa ukimwi inamaliza watu kila wiki. Sasa hawa wanawazwa wanaachwa wataangaliwa na nani kama mzee na mama wamekwenda.

**Com. Barasa**: Tuko na Ngala Ayub. Mzee wangu hapo dakika tano. Wazee wangu muniwe ladhiradhi.

**Ali Ayub**: Mimi wakati wote hukaa mabarazani lakini sijajitamburisha sana kwenye mabaraza, isipokuwa najulikana mtaa wetu huu wa kinango na kwa hivyo mimi nimechaguliwa mtu wa KANU wa kwanza.

**Com. Barasa:** Jina lako nani?

Ali Ayubu: Jina langu ni Ali Ayub, Alingala Ayubu, wabunge wanaanza kusimamia hii kiti, kutoka akina Bidu kutoka akina nani, lakini sasa naonekana kwamba nimevunjwa hapa kwetu Kinango, hapa hapa town kwetu Kinango tuko kando kando. Mimi

nilikuwa ni mtu ambao hutafuta njia yeyote, vijijini kote, kusema barazani hapo, na misikiti, na kumletea habari hizo kwa Chifu na nimekuwa nikiendelea hivo hivo. Lakini hivi sasa nimesahaulika mabarazani, shabiwi wala nini na huona vitoto vidogo tu, vile vinavyotumwa. Hata nikiwa hapa nyumbani akapita mzee mmoja huonana naye kwa mabaraza wakati wowote na akaniambia mimi nakuakualika baraza. Wapi? Kinango, nikamuliza; mwenye kukuakualika baraza ni mimi au ni wewe? Basi ikawa shida.

**Commissioner:** Sasa unataka katiba ikufanyie nini?

Ningeomba Katiba kwamba kazi yangu iwe ile ile ya mzee wa miji. Eeh wa kutangaza na kuheshimiwa, sasa imekuwa heshima hakuna tele, heshima hakuna tena. Hakuna haja hata ya mshahara, kazi ni ile ile ya kidesturi kukitokea baraza nionekane mbele kama mimi ni nani! Basi wananifichaficha na wamechukuwa watoto wadogo ndiyo wanasimama kwenye baraza. Basi mi naona nasikia uchungu kwa kuwa kama wamenisahau na tena si watu tu wa majumbani, hata hapa hapa kwetu maofisini. Ingine la pili mimi naona uchungu sana nataka nijue kwamba nitaendelea na ile kazi yangu hiyo ikitokezea kuna shida furani fulani nielezwe na vichifu na machifu ndio twendelee nao pamoja.

**Com. Barasa:** Bwana Chifu wa Kinango yuko?

Hajaingia, akiingia utatwambia tuchunguze mambo ya mzee.

**Com. Barasa:** Baada ya mzee Ali, tuna Gasma Rumba.

**Rumba:** Mwenyekiti, Macommissioners wote, na ndugu zangu hamjambo! Mimi kwa majina naitwa Gasma Rumba Nyamau ni mzaliwa wa Guma Location, nataka kuchangia vitu viwili muhimu, ya kwanza ni kuhusu magonjwa ama tunaweza kuyaita special diseases kwa mfano; ukimwi, ukoma na magojwa mengine ya kitalamu ile wanayoijua. Ningependekeza wakuwe na sheria malum ambaye ambayo itawawezeshayezeza serikali kuwaangalia wale wagonjwa kikamilifu. Kwa sababu kwanza mtu akiwa mgonjwa namna hiyo huwa hawezi kutafuta chakula kwa cha watoto wake na pia yeye mwenyewe akili yake imeharibika. Kwa hivyo mimi ningependekeza kuwe na sheria hasa ya kuwa hasa akijurikaka akijulrikana ni ukoma au ugonjwa ule wa kumaliza, kuwe na sheria hata kwa hospitali huwa mgojwa akiingia huwa ataangaliwa bila kusumbuliwa, mtu wake au yeye mwenyewe.

Ya pili ni kuhusu uridhi wa watoto, tunajua yuko baba na mama kama wazazi wa mtoto mmoja hata kama ni wawili au watatu. Sijui kama kuna sheria lakini sioni ikifanya kazi. Kwa sababu baada ya kuoana lazimami na sheria kutengenezwa; wakati pengine kama wameachana kwa bahati mbaya na Bibi kulingana na kimila cha Kiafrika, nafikiri bwana ndiyo ndiye kiongozi pale. Kwa hivyo ningependekeza kiongozi achukue uridhi wa chochote kilichombakia;

**Com. Barasa:** Kama bwana amefariki?

**Rumba:** Sikusema kufariki, nilisema kuachankuachanaa. Sasa hawa watoto badala ya kugawanywa humu na huku, wapewe mlolongo mmoja na sheria iwe iko mikononi mwa ule mkubwa, mkuu wa familia.

**Com. Barasa:** Nani ndiye mkubwa?

**Rumba :** Badu hujanielewa!

**Com. Barasa:** Unasema ya kwamba bibi na bwana wakiachana watoto wawe mikononi mwa bwana kwa sababu bwana ndiye mkubwa wa familia.

**Rumba:** Eeh ndiye hii sasa hayo ndiyo maoni yangu ya pili. Mwanamke ana haki ya kuchukuakua mali hata kugawanya mali ana haki ambapo sheria tunaka iwe na upande mmoja tu ule wa mwanaume. Siyo kwamba hatutambui akina mama tunawatambua lakini kwa sababu kuoa kikwetu si kama wale wazungu kuoa kikwetu ni kuchukuakua mtu kwao na kumleta kwetu.

**Rumba**: Nafikiria hivyo; ndiyo maana mimi nasema namna hiyo.

**Com. Barasa:** Unasema hao watoto waende na baba na mama aende asiwaone tena? Naunajua mama ndio mlezi mzuri wa watoto, unajua hivyo? Na sasa unasema aende zake asahau hawa watoto? Unafikiri hiyo ni sheria mzuri kwa kweli? Yeye hakusaa hakuzaa hawa watoto?

**Rumba**: Asahnte sana mama kwa swali lako. Ni kweli mlezi namba one ni mama kwa sababu ndio anakaa na watoto wakati wowote. Kulingana na haki tunayotake tunayotaka kuirlekebisha kwa leo huyu baba ana haki zaidi kwa sababu ndiye mkuu. Unajua mimi naweza kusema hivyo pengine; Presidenti ama mtu yeyote mkuu yuko na haki kidogo zaidi kuliko mtu wa chini kama mimi. ZIiko, kitu kama hicho, sasa mimi ningependekeza baba awe na haki zaidi hasa kwa watoto kwa uridhi wa watoto.

**Com. Barasa**: Na wale watoto. wale wa?

Kwenye uridhi wa mali sasa, uridhi wa mali hiyo ni sehemu ingine, uridhi wa kwanza mimi nasema ni ule wa watoto peke yake nimezungumzia pale.

**Rumba:** Kwa upande wa mali ziko.

**Com. Barasa:** Mwingine ni Bwana Ali Juma Nyam. Ali Juma Nyam.

**Ali Juma Nyam:** Asanti Asante sana Bwana mwenye kiti, commissioner na wananchi wenzangu. Kwa majina naitwa Ali Juma Nyam naishi hapa Kinyango. Maoni yangu, kwanza naanza na umilikaji wa ardhi. Ninapendekeza kwamba katika katiba hiyo ambayo inatumika siku za usoni ardhi imilikiwe na mwananchi wa Kenya raia wa Kenya mtu wa Kigeni asiweze kumiliki ardhi.

Ya pili, kuhusu ardhi imilikiwe na mtu binafsi. Katika upande wa haki za wafungwa, upande wa wafungwa, ningependelea wakati wa upigaji kura wafungwa wapewe haki sawa na wale ambao wako huru ili waweze kupiga kura. Katika cardi ya upiganji kura ningependelea irekebishwe hadi ya kwamba mtu au mwananchi aweze kupiga kura mahali popote. Lingine ni kuhusu mfumo wa serikali, ningependelea katika mfumo wa serikali uwe ya wa majimbo. Kwa maoni yangu nafikiria hiyo itaweze kuleta ugawanyaji wa rasili mali sawa sawa kwa nchi nzima. Na katika masunduku ya kupiga kura ningependelea masunduku ya upigaji kura yawe transparent uweze kujua kule ndani kuna nini na pia kukiwezekana zile kura ziwe zikistudyiwa katika pale mali ambapo wapikaji kura wanapiga ili zikipelekwa ziende hesabu katika sehemu ya wakilishi bungeni.

Na ingine kabisa ya mwisho inazungumza kuhusu wafanya kazi.

**Ali Juma:** Ni ya mwisho.

**Ali Juma:** Eeh nimesema badalaada yakuwa zinameshahhesabiwa katika pale mahali huwa zimepigwa zimekuwa zikiende hesabu katika sehemu ya wakilishi bungeni badala yakuwa zikihesabiwa pale. Ingine kabisa nilikuwa nizungumza nizungumze kuhusu wafanyi kazi wa serikali wapewe haki sawa wakati wa siasa ukifika waweze pia nao wasiwe na uoga wawe na uhuru wakukuaa wanaweza kuzungumza siasa mradi tu wasizifanye katika sehemu zao za kazi.

Na ya pili, oni langu lazungumza kuhusu wale wafanyi kazi kuwa wamestaafu muajiri, wakati mtu anastaafu, katika mshahara; kama wale wengine wanaongezewa wao hupuuzwa kwa hivyo wao pia waweze kuongezwa kwasababu wamefanya kazi nzuri kwa miaka ishirini na tano. Pili pia mwajiri aweze kumwangalia masilahi yake ya kiafya amlipe pesa za matibabu aendelee kumlipa mpaka atakapochukuliwa na Mwenyezi Mungu na pia amwangalie masilahi ya nyumba. Nna kuhusu hawa wafanyi kazi wengine ikiwa serikali imekubaliana kuhusu mambo ya, pengine kama nyongeza za mishahara na kadhalika serikali inayokuja iweze kuheshimu ule mkataba na ikiwa itafika hadi ya kwamba waweze kufanya mgomo usiitweo mgomo ule haramu kama umefuata zile taratibu za kisheria. Nnafikiria maoni yangu itakomea yatakomea hapo.

**Com. Barasa:** Thank you very much. Wambua Nzikali. Haraka haraka Wambua mwingine ajitayarishe Beatrice Janga. Jangaa or Janga. Haya Jangaa haya jitayarishe.

**Wambua Nzikali:** Asanti sana Mwenye Kiti. Mimi ningelipendelea, Mmimi ni Wambua Nzikali, mimi ningelipendelea katika elimu hii ya msingi iweze kuwa na ni ya bure na hali ya undamivu katika mahospitali uweze kutolewa bure igaramiwe na serikali. Naomba pia tume hii iangalie iwe ikiwawekewa elimu fulani, Counsellors amabao ama wagombeaji wa ucounsellor elimu ya chini hata kama itaanzia darasa la nane lakini mtu awe anaelewa anafuata kitu gani na hivi viama ambavyo huwa vinaandikishwa vya kisiasa viwekewe kipimo na wala sio yeyote anayesikia kuakuwandikisha chama awe anaenda na kuakuandikisha. vinastahili kuwa vitatu.

**Wambua:** Kiwango

**Com. Barasa:** Na hutaki waziangalie vile zinafanya kazi yakezake.

**Wambua:** Lazima ziangaliwe.

**Com. Barasa:** Tuangalie vile zinafanya kazi.

**Wambua:** Ndio

**Wambua:** Ah, bado. Na nyingine ni hawa utawala wa majimbo ningelipendelea tuwe tukiwachagua sisi wenyewe isipokuwa watu hawa hawana transfer huwa tuko nao miaka hamsini ni hamsini wanafanya vyema wanafanya vibaya tuko nao. Ingine ni kwa upande wa Mayor, mamayor tuwe tukiwachagua wenyewe na wala si counsellors. Yangu ni hayo.

**Com. Barasa:** Mwingine ni Beatrice

**Beatrice:** Majina yangu ni kama vile mmeyasikia Beatrice Jangaa. Ninawakilisha kikundi kingine inacyoitwa Kisumuni Dinani na ……….. Kisumuni, Mmathanuni location Sauni constituency.

**Com. Barasa:** Inaitwa Kinango.

**Beatrice:** No Kinango constituency sorry sorry, pole pole sana.

**Beatrice:** Yaani tofauti kwasababu ni groups tofauti. Jana ilikuwa ni ya ………… Women's Group na sasa ni Dinani Kisauni ndiyo tumeshaa kuwa huko. Oni la kwanza, wamama wa huko walikuwa wanataka haki za watoto wao. W watoto wa huko sana sana wananyimwa haki zao kama zile za elimu, hawapelekwi shule. Moja kwa moja ukizaliwa mtu nenda ukakate miti tano hiyo makaa Ssasa nilazima wazazi wa mtu walazimishe watoto kusoma na tena aweze kuwa na uhuru wa kuwapa chakula na mavazi na nyumba inayofaa na pia afya.

Point nyingine hii ni kuhusu watu walemavu na haki zao, tunakuta mara nyingi walemavu wananyimwa haki zao sana sana kwa mfano kama ni upande wa kazi walemavu hawawekwi sawa na wale ambao wana miguu zao ama pengine mikono zao ama mwili wao ukiwa ni sawa. Kwa hivyo tunahitaji haki zao ziwe sawa kama vile yule mtu mwenye miguu misawa na kila kitu sawa kama ni kazi iwe sawa kama ni mlemavu awe Chief awe chief. Na kama pengine awe rais kama inawezekana awe rais mlemavu. Nikiendelea hata bungeni tunataka walemavu wapewe viti waende wakakae huku waongee wajadiliane watu kuhusu masilahi yao hata kwenye council pia.

Point ya tatu, hii ni kuhusu mila na desturi, utakuta mababa wa wetu huu Wwaduruma hata bibi akishafiwa na bwana wake

tayari wale ndugu zake yule bwana aliyekufa wanangangania yule bibi badala ya kumsaidia yule mama. Kwa hivyo kama ni kuridhikurithi, uridhi usimrithi ule bibi bali msaidie na watoto wake kusoma na maneno mengine.

Nikiongezea miundo mambo ni ya serikali sikwamba wabara wote wafukuzwe huko kwetu, au wafukuzwe kwetu Pwani bali kama kwa mfano ni bandari letu huko Mombasa, mkubwa awe ni wa Pwani na hata kama kuta kuwepo wa Bara lakini asili mia yake iwe kama ni ishirini na tano huo ndio uwe wa Pwani…….

Nikimalizia, hii ni upande wa raia, ; raia ni mtu aliyezaliwa mahali pale na kama amekuja mmezaa naye watoto pale watoto wale. Mmzungu akitaka kurudi kwao ni wako wewe baba wa hapa kwa hivyo watoto wa mtu wa inje wawe ni raia wa Kenya. Asanteni kwa hayo machache.

**Com. Barasamissioner:** Eeh Kazungu MwalugombaMwakugomba. Haya mzee wangu.

**Kazungu MwamgombaMwakugomba:** Hamjambo ma bibi na mabwana mimi sina maneno mengi. Ah, jina langu mimi ni Kazungu MwalugombaMwakugomba boss lakini sina mengi lakini ninaongea kitu ambacho nilikiona vile alikuwa mama akiongea hapa. Y yale mambo hata mimi yamenipata. Mmimi nini mlemavu. Nnilifanya na APDK Likoni, nimefanya miaka thelathini lakini wanasema mlemavu hana haki yakulipwa pesa zile zile, basi nilipambana nao. W walinipatia kitu kidogo ambacho si halali wanasema mlemavu hana haki ya kulipwa pesa za retirement walinipatia kitu kama elfu sitini na mimi nimefanya miaka thelathini ile ni haki? Aalafu wakanipatia barua ya kudai N.S.S.F. na pesa za kusafirisha vyombo vyangu walinipatia elfu tatu je ile ni haki. Wanasema mlemavu hana haki ya kulipwa je ile ni haki? Mmefanya mikutano mikubwa mikubwa mimi mnavyoniona hapa nilifika hadi Nairobi, Kasarani ndani nilifika kuongea mambo yale yale ya ulemavu na Bwana Mganga ndio alikuwa Chairman wetu lakini yalikuwa yanaendelea Mr. Mganga alikwenda mbele ya haki, yeye alikuwa anaongoza anasema mlemavu hana haki ya kulipwa pesa hizo walinipatia elfu sitini. Sasa mimi nashukuru ningeomba wale wenzangu waliobakia pale iwekwe mkazo wakiondoka waondoke na kitu kwa sababu uwe umepoteza nguvu zangu bure, mimi nimefanya miaka thelathini na wale nao wanastahili kufika miaka arobaini pale lakini wakiondoka wataondoka na vivi hivi hata kuwekwe mkazo. Mimi sina mambo mengi asanteni lakini naomba mambo mengine tena mimi nimejifunza ile kazi na ile kazi nimeijua ya useremala lakini kule nimeondoka sikuondoka na vifaa ninaomba kama inawezekana nipatiwe vifaa niwe naendelea na kazi yangu.

**Com. Barasamissioner:** Mr. Kazungu ulisema ulilipwa sixty thousand na wale ambao sio walemavu walilipwa ngapi? Wakiretire wanalipwa ngapi? Mimi ninaona huko kwetu ndio mwalimu sio mlemavu amelipwa forty thousand, sijui kule kazini kwako wale wengine wanalipwa ngapi wakiachishwa kazi? Sisemi hakuna ubaguzi watu walemavu wanabaguliwa sana lakini juu ya hii mambo ya pesa walilipwa pesa ngapi?

**Kazungu:** Wale walemavu

**Com. Barasa:** Hapana

**Kazungu:** Wale ambao si walemavu wanalipwa zaidi kuliko sisi, huwezi kujua lakini wanapewa zaidi.

**Com. Barasa:** John Githinji.

**John Githinji:** Mwenye kiti, kamati woteyote. Majina langu yangu ni John Kinyanjui Githinji. Mimi ningependelea tume ambaye ambayo inazungusha inazungmzia katiba ama katiba ya Kenya iwe namna hii. Mwanzo ningependelea kuwe ya kwamba yani wakati wa kuchaguana viongozi, councillors, MPs, kila mtu awe anachagua mtu ambaye anapenda. Kitu kile kingine ni kwamba hata kuwe ya kwamba pakifika pahali pa wale watu wanatoa pesa ule mtu ambaye anatoa pesa kwa sababu sio halali awe akistakiwa na awe disqualified katika uchaguzi huo unaoendelea ndipo kila mtu yeyote kama maskini akaweze kuwa anakiongozi.

Kile kingine ni kwamba ninaomba ya kwamba tukiangalia wakati wa kortini judges ama magistrate awe akiulizwa na mstakiwa swali kwa sababu sio yaani he is not above the law aulizwe swali na ajibu . kitu Kitu kile kingine ni kwamba elimu ambayo inasomwa kutoka darasa la kwanza mpaka wa darasa la nane iwe ni elimu kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la saba kwa sababu nikupotezea ule mtu wakati wake na ikiwezekana tume ya katiba iwe mwanakenya wote ajue sheria iwe ni subject kutoka darasa la kwanza mpaka pahali atakapofika na iwe ni sheria ambaye ambayo anasoma iwe ni subject kama mathematics, physics kama hiyo yote kwa sababu ni kwamba unaweza kuona mwanainchi wa Kenya ameenda kortini na hana representative kama lawyer anafungwa kwa sababu hajui sheria ya Kenya ya kwanza na ya pili inasema namna gani. Aawe anajua sheria za Kenya na awe anaweza kujirepresent katika kortini.

Lile lingine ni kwamba ni mfungwa. Mfungwa angaliwe sana mavazi ambaye anavaa asiwe mtu ovyo ovyo. Na kama ni kula akule chakula ambaye ambacho kinafaa si chakula hivyo hivyo akule chakula inafaa. Ile ingine ni kwamba nigependa kusema chief - assistant chief wawe wanachaguliwa ni na wenyeji wa pale, asiwe anachaguliwa na serikali na elimu lake, iwe amefika form four asiwe mtu hivyo hivyo kutoka form four ndiyo awe anaweza kuwa chief.

Lile lingine ni kwamba, ni wachuuzi ambaye ambayo tukiangalia sawa unaweza kuniunga mkono wanasumbuliwa zaidi ya mno katika Kenya nzima, haonekani kama mwananchi wa Kenya kwasababu anafanya biashara. Wale wachuuzi, hawkers waangaliwe sana vile wanaweza kusetiwa pahali pamoja wasiwe wanachukuliwa kwa sababu hapo ndipo chanzo chao na inapofika mpaka pahali wanaweka duka kama wale wengine. Jambo ile lingine ni mgeni mhindi ama mwarabu yeyote asio mzaliwa wa Kenya sawa akija asirithi mali hapa asirithi ardhi asirithi kabisa. Okay na katika bunge asikubaliwe kuwa kiongozi ama awe MP ama awe Counsellor anywhere, awe tu ni mtu amekuja na ni wa kawaida na jambo lingine ni kwamba hali katiba inasemekana majimbo ningependa serikali yetu ambaye ambayo inazungumza juu ya majimbo ielimishe wanainchi sawa majimbo ni nini kwasababu wengine hawa elewi ni nini wengine wanafikiria nikufukuza watu, hawaelewi ni nini kwa sababu itafika mahali iumize mwanainchi waelewe kabisa wafundishwe na ikiwa ni siasa waelewe na kukiuwezekana, watu ambao wasio pale kuletwe watu wa mbali wajue ni nini yaani majimbo maanake ni nini. Wajue ni nini majimbo.

Jambo lile lingine ni kwamba kuoa, ni kwamba mwanaume anaumia wakati wa kutoa kila kitu. panapofika pahali pa kugawanya mali unakuta mali imegawanywa sawa sawa na mama, na ule mama anaweza kupata opportunity aje aolewe na mali yangu nimeifanya alafu wanaenda kugawanya na ule mwanaume mwingine wakiachana. iwe ile mali ni ya ule bwana na watoto ambao amezaa nao pale.

Jambo lile lingine, pili ni kuhusu akina mama. Kkama serikali yetu inaongozwa na uongozi wa kidini ama wa ukristo tukiangalia bibilia hakuna pahali ambao mwanamke amekuwa kiongozi, ama chief ama D.O ama D.C. wawe wamepewa rank zile zingine lakini wasipewe hapo kwa sababu huwa serikali haionekani kama inaongozwa Kimungu ukiangalia kabisa katika bibilia. Kitu kile kingine ni kwamba elimu iwe ya bure kwa sababu hio elimu ilikuwako mimi nimesoma nimemaliza 1977 form four nikaona ya kwamba nilikuwa ninasoma bure lakini sasa tunashangaa kuona elimu ni ya kulipa hata kama italipwa iangaliwe kiwango ambaye kila mwananchi anaweza soma kitabu iwe ya bure, elimu iwe ya bure everybody should go to school na ajue ni nini ndio aweze kueleweka.

**Commisioner:**…………..

**John Kinyanjui:** Nitasema moja tu. Kitu kile kingine ni kwamba wakati hawa polisi wanashika mtu akipelekwa kortini kama itawezekana akaweze kuhukumiwa pale asipelekwe rumande awe yani sijui anafanyiwa mambo yake ndio aende akakubali kortini hiyo iwe hivyo. Na kitu kile kingine mwananchi wa Kenya kama ni mwananchi nisiwe asiwe aliulizwa anatoka wapi na anaenda wapi. Polisi wasiwe wakiwasumbuwa watu kwa sababu hata yeye polisi anaenda wapi?
naenda kule nakilizwa unatoka wapi na unaenda wapi mimi mwananchi polisi wasiwe wakisumbuwa watu hapo kwa sababu hata yeye polisi anaenda wapi?

**Com. Barasa:** Eeh. Haya mwingine ni Mwangoma Ndambari dakika tano mzee, Mwagoma Ndabari mnangojea wawili?

**Mwangomba:** Ah mimi naitwa Mwangoma Ngabari, location Ndavara, mimi ni village chairman huko sehemu ya Mombasa ah mwenye kiti na ndugu hamjambo. Mimi swali lyangu ambayo ambalo nitalieleza ni kwamba watu wetu kama sisi hatuna chochote tena hata tunabakia na mnazi na korosho ndiyo mali yetu ambayo itayotutunza lakini basi tuna matatizo kwamba mali yetu hii ambayo inayotusaidia ile inangushwa chini kabisa kila moja shilingi nane kweli nane na una wazazi, watoto ambao wako mashuleniukulini unawafundisha wewe oh korosho umepata gunia kama mbili na kilo ni shilingi nane, unachukuakua nazi, nazi ni shilingi nane sasa kile tunakivisomea katiba kwamba hapana hatuna haki hatuoni haki kabisa tunataka ile hali yetu. tunaomba Tunaomba pia hapa ambapo tunasomeshea watoto wetu na tunapata chakula humo humo wengine tuko wazee hatuwezi chochote ipande pesa nayo iwe kama ile mali ya kimaana.

Ingine ni kwamba tunasikitika zaidi kama sisi village chairman chairmen ambao hatulali, hatushindi tunashida tunafanya tukifanya

kazi usiku na mchana lakini tunafanya kazi bure halafu tunaenda kuombwa mafuta na akina mama na hatukupata hata sales moja. Sisi watu wa serikali natunafanya na sisi watu wa serikali ambapo nasi kama inawezekana tungepatiwa katiba yetu ambayo ingepata kama kitu kidogo. Tu tukawa nasi tukitoka kule masafarini tukija tupate kama mafuta na chakula ya watoto na madawa. M mbona hatupati na kazi ni pamoja moja kwa moja. Kkwanza sisi hatulali.

Lingine ni kwamba hii inchi yetu imeingiwa na ukame. tazamani Tazameni wale watu wazamani wangekuwa wakati huu wanakula mahindi ya kuchoma lakini siku hizi kabisa kabisa mtu mmoja kwa mmoja mfupi na sababu yake tumefikiria kama sisi watu ambae ambao hawajeokoka hawajaokoka tukaonelea tunaonelea hii inchi yetu, mizimu mafimbo yetu ah kile kitu ambacho kili kuwa zamani kikatengenezwa na kuku mweusi mafuta ya nyonwa wanapiga ngoma yake ngu ngu ngu basi tunapeleka kama ngombe, kama kuku, kama mbuzi tukifika pale tukipeleka pale ile mahali ikishakunywa ina kunywa sasa tumeharibiwa. T tunataka tuweke pamoja ombi langu tuwe pamoja. S sote tuombe ile ili mvua iwe tutapata chakula soteni. Asanteni.

**Com. Barasa:** Mbali nakuomba mvua, mjue mvua inanyesakuja m pahali ypenye miti mingi na misitu. Kwa hivyo mkikata misitu hata mkienda mkipiga makesha pale, yule Bwana hatawapatia mvua kwasababu mvua huletwa ikiwa kuna clouds ikiwa kuna mawingu ambayo yanaletwa na mvuke wa maji yanayotoka kwenye miti mingi kwa hivyo mkumbuke kupanda miti huko ni lazima. haya lakini miti nayo mupande. Huko kwenda kuomba ni lazima haya lakini miti nayo mpande.

Haya mwingine ni Fatuma Mukunju. Mama dakika tano.

**Fatuma**: Mimi Naitwa Fatuma Mukunju kutoka Kinango. Mimi ni chairlady wa tukuza. Kuna kundi kuna kundi la kugu ndilyo anakiliza na mimi maoni yangu nimemu memona mzee mwingine hapa tumetoka mbali sana. Na mimi nataka haki ziwe pote pote. Mmme, mke. Mke akiolewa na mumewewe na haki amshauri mme na kama mme amemkoszea mke, lazima akushauri na ukubali kosa lako. chuo liambie mimi ni walikosea lakini kubali kwa sababu unajua mimi si na haki. Sina haki kwa nini na mimi ni mwanamke?. Umenioa, tumetongozana na tunapendana, lazima tusilikizane nyumbani. Huwezi kuniambia ati sina haki. Wewe ukienda kazini niko shambani napikia na kuangalia watoto. kazi yote nyumbani Aalafu unaniambia sina haki. Sina haki kwa nini. ? Ni haki tupatane, na nipate uridhi urithi wewe ukifa namimi ni pate uridhi urithi wa watoto niwaendeleze. Unaona wewe unakufa na mtoto anambaki na mama na anaendeleza mpaka asomeshwe. si wako. Kwa hivyo sisi tusfuata ili haki.

Na haja jambo ingine kusime tusime mimi nilizaliwa na ndugu wangu wakiume. Na baba amezariga amewasa mali amewasa shamba. Lakini ule ndugu wangu wakiume ndiyo ndiye ako na haki ya kupata shamba na ile mali. Ninaona pale maumivu uchungu mkubwa makubwa sana. Kwa sababu baba ni yule tu moja. Na haki na mimi nipatiwe.

Lingine ni naomba sirikali yetu kubwa ikienda sisi watu wa pwani tupate na sisi majimbo. Sio tukipata majimbo tunasema watu wa huko watu wachache ala tuwataka wenzetu kwa sababu ni Wakenya. Lakini na sisi tupate kiongizi wetu. Sio tutawakataa

kwa sababu tutasema huyu ni mtu wa bara. nini Kkama bwana Ngila anasema tukipata hiyo majimbo hatujui maana yake ni nini aa. Majimbo nikama kila kitu kiupate kifadhi kama vile wenzetu una bidii una nini. Na sisi tataka tunataka tupate majimbo yetu hatufukuzi mtu kwa sababu sisi wote ni Wakenya. Hatuna ubanguzi.

Lingine kama niliyosema, nasema serikali kama serikali kama hii ni kweli kwa sababu imekosea likini nikienda pali mahali kama huna chochote hua munyonge huna haki. Mwenzio pale wakiwa wa mekudhulrumu akaenda akapata haki. Hapa twaomba serikali alinyangalieiangalie.. Wenye majudge sina mengi ni hayo tu.

**Com. Barasa**: Unasema nyinyi wa pwani mnataka majimbo. Hiyo majimbo unataka ikunfanyie nini. Unaona ukipewa hiyo majimbo nini kitafanyika? Tutakuwa na tofaoti gani kwa maisha yako?. Nataka tu nielewe. Itakufanyia nini?

**Fatuma**: Twataka na sisi tuwe kama wenzetu kule juu. Tuwe na uhuru kama wenzetu. Tuwe na kiongizi wetu hapa kama wenzetu. Ndiyo tutaka vizuri. Ndiyo tutakaa vizuri. Lakini sio kuwa tulikuwa tulitaka yale majimbo basi tuseme wengine hatuwataki hata. Tunawataka lakini tupate kiongozi wetu wa huko na sisi.

**Com. Bishop Kariuki**: Mama umesema juu ya haki ya akina mama. Unasema mzee akienda kazini na wewe unaenda shambani. Mnatafuta watu wawili. Hizo Hivyo nikusema mama unapendekeza mzee na mama wakiayaachana kama divorce, wagawanye ile mama katikati?

**Fatuma**: Sawa.

**Com. Bishop Kariuki**: Kuuliza tu?

**Fatuma**: Nataka bibi na bwana wakiwachana ile mali wagawanye sawa sawa kwa sababu wameiishi chumba moja. sio apewe mwaume wewe uondoke hivi hivi tu. Si huyu mzee tumeishi hapo hapo. Itakuwa ni maumivu. Itakufanya nini kule mimi.

**Com**. **Barasa**: Haya Rehema Kalumu.

**Rehema**: Mimi naitwa Rehema Kalumu. Mimi leo nimekunja kuzungumza kutoa maoni yangu. Kwanza ningependa kutoa maoni yangu kuhusu uridhi. Uridhi Urithi ningependa katika kabita katiba yetu ifanunue wasi wazi wasi wazi kwamba uridhi urithi kwa watoto iwe ni watoto wote. Sio mke sio mume. Ningependa uridhi urithi uridhiwe urithiwe watoto wote.

Pili ningependa elimu iwe ni ya watoto wote. Sio wengine waende wakaolewe wengine waende shule.

Tatu ningependa nionge urithi kwa akina mama. Katika sheria na dini zingine si nasema mume akifa mama anapata herufi moja

kwa urithi wa mumewe. Na hua ni hasara kubwa na yule mama anaondolewa hapo nyumbani. Anafukuzwa. Hiyo ni dini ya Kislam. Sina challenge lakini mimi nasema iangiliwe.

Tatu ningependa niongee urithi kwa akina mama. Katika sheria za dini zingine zinasema mume akifa mama anapata tenth moja kwa urithi wa mumewe. Na hua ni hasara kubwa na yule mama anaondolewa hapo nyumbani. Anafukuzwa. Hiyo ni dini ya Kislamu. Singeichallenge lakini ninasema iangaliwe kwa sababu hiyo ni mambo ambayo inaumiza akina mama.

Hiyo ya kufukuzwa basi tuizungumizie. Hiyo ya kufukuza akina mama wakifukuzwa kwa sababu mtu pengine ameolewa tangu kitambo ako hapo, amekuwa mzee hapo halafu anafukuzwa kwa vile bwana amekufa hajui aende wapi. Kitu kingine abacho nimeomba ni kuhusu kule kuolewa na kuachwa. Nafikiri sheria ikiwekwa itakuwa mali itagawanywa sawa, na wengine watawacha kuoa wakiachana. Kina baba wengi wanapenda kuoa mabibi wakiwaacha. Ile mali ikiwa itagawanywa sawa wataogopa kule kuoa wakiwachana. Watakua wanaoa huyu mmoja na wanakaa naye mpaka wanangojea kufa. Wakikaa na huyu mmoja, hata ukimwi hautapatikana.

Kitu kingine ni cha ardhi. Tungeomba ardhi yetu za wale ambao hawajapimiwa ardhi katika Kenya hii wapimiwe ili kila mwananchi awe na cheti za kumiliki ardhi. Kenya hii tukiwa sisi watu wa Kingango ndiyo tumezidiwa zaidi. Tupimiwe kila mtu ardhi sehemu yake. Kitu kingine ambacho pia ningependa kukieleza ni kwamba katika hii Kenya sisi watu wa Coast tunaangalia nazi, tunaangalia mkorocho, tunaangalia mambo ya mashambani tunalima. Sasa tunaambiwa tutoe nazi pekee yake na makuti lakini ile pombe ambayo inatoka kwa wengi ndiyo inawasaidia zaidi. Tunaambiwa hiyo tukionekana nayo tutapigwa. Tunashikwa tunapelekwa ata polisi. Halafu kuna vitu vingine ambavyo tulikuwa tukilima tunapata mazao lakini kitu kinachotuumiza zaidi ni kwamba ndovu wanaachwa wanaingia kwenye mashamba wanakula mimea yetu na hatulipwi hata shilingi moja. Kwa hivyo kama sheria itawezekana hapo ndovu ikae msituni. Wasiuwe wakaemsituni ili sisi tupate kulima tupate mazao. Na kama itawezekana tupewe ruhusa ya kuwafanya vile tutaweza.

Hiyo pombe ya mnazi ihalalishwe iweze kutengezwa, itengenezwe mitambo ambayo itatengeneza pombe ya minazi ile mwanardhi wa coast apate pesa kutoka kwenye ule mnazi iuzwe, itumwe kwenye kipakiti iuzwe inywe kihalali. Asante.

**Com. Barasa:** Hii pombe ya mnazi kabla ipigwe marufuku, watu walikwa wakilewa. Kulikuwa na hali gani watu wakinywa hiyo pombe? Nieleze vizuri nielewe.

**Rehema:** Pombe ya mnazi kabla haijapigwa marufuku watu walikuwa wakinyua kidogo kwanza. Lakini tangu ipigwe marufuku watu walizidi kuinywa paka kupindukia. Kwa sababu chochote kiki ambiwa hakitakikani ndiyo huwa kinatafutwa kwa bidii kipatikane. Kwa hivyo mkisema ikunyiwe, ihalalishwe, itakunyiwa na wengine wataenda kufanya kazi zao.

**Com. Baraza:** Tukisema kwamba sheria iseme wazee waende kwa saba, walime mpaka saa saba, wapande mimea mpaka

saa saba, wapande mimea mpaka saa saba halafu wakunywe hiyo itakuwa mzuri? Kwa sababu Uganda wamefanya hivyo na hupati watu wamelewa. Huko kwetu kule ninatoka asubuhi wanaenda kunywa. Ni kunywa tu day in day out. Sasa tutaua nchi. Tukisema saa moja kwa kila siku lakini wakati ule mwingine wote mnaenda kwa shamba mnalima itakuwa mzuri?

**Com. Bishop Kariuki:** Niseme hivi, maana wewe unasema hii pombe ya mnazi ni kama Cash Crop, na unasema kwamba kutengenezwe kiwanda ya kutengeneza na kuuza hata mbali. Si ndivyo unasema?
**Rehema:** Ndiyo hiyo nasema.

**Com. Kariuki:** Husemi tu kwa ajili ya watu wa hapa kukunywa?

**Rehema:** Yaani ninasema pombe ya mnazi itafutiwe kiwanda, itengenezwe itiwe ndani ya mapakiti, kwenye chupa iweze kuuzwa mpaka nchi za nje tupate pesa za kufundisha watoto na za kutumia.

**Raphael Nzavila:** Mimi kwa jina naitwa Raphael Nzavila. Naanza na kusema ya kwamba ninataka uchaguzi unaokuja usifanyike mpaka tuwe na katiba mpya. Sababu ni nazo za kutosha lakini nitaangalia wenzangu wa Kinango ni wengi. Naachia hapo nafikiri nimeeleweka.

Ya pili uchaguzi uwe katika katiba yetu mpya uwe mara mbili. Uchaguzi wa kwanza uwe ule wa Rais na mamayor na chairman wa council. Baadaye hawa wakiyachukua madaraka yao watayarishe uchaguzi wa wabunge na madiwani. Lakini huu uchaguzi unaoendelewa kwa sasa moja kwa moja, tatu jogoo tatu huku ni kwendeleza hongo. Corruption inaotea hapa na hatupati wabunge ama viongozi ambao wanstahili kwenda katika kwendeleza takatifu huko.

Katika uchaguzi ndani ya katiba yetu kuwe na sheria kwa sababu ufisadi ndiyo uliuwa Kenya hii. Unasikia wengine majimbo, wengine sijui nini, ni kwa sababu ya ufisadi ambayo imepita kiasi. Hata watu wanasema hawawezi kungolewa katika Jamhuri ya Kenya. Kwa hivyo katiba yetu mpya iwe inasimamia sana mambo ya ufisadi. Ianze kwa uchaguzi. Mtu atatoa, sisi hapa Pwani tuna msemo kajama, mimi mwenyewe nilikuwa Chifu kwa miaka ishirini na hiyo nimekula kajama. Kwa hivyo kajama kajama ikitolewa ichukuliwe kama kosa kubwa sana. Na mubunge aweze kusimamishwa na wale kajama. Kajama ni hongo ni ufisadi na hiyo ndiyo corruption hapa inanza hapo.

Tuwe na uchaguzi sawa. Maskini aendelee na tajiri aendelee. Ninasema tunataka, mimi hapa nataka kuwe na serikali moja kuu, serikali ya nguvu, President ana nguvu, ili tuanze kungengana na matatizo ya ulimwengu. Hata jama zinatengenezwa na lawyers kama Tanganyika na Zanzibar imeungana. Kuna Tanganyika na Zanzibar wameungana. Sisi hivi sasa tunatengeneza umoja wa Afrika Mashariki. Hilo lote tunataka umoja wa Afrika. Nanikutafuta umoja. Leo hii tukianza kugawanywa kwa sababu ya ufisadi ambao umetoa mizizi. Ninataka Serikali moja ya nguvu, inamaliza ufisadi tuweze kwendelea.

Kitu tu mimi ningependekeza ni kwamba tayari kuna district focus for rural development lakini hii imefungwa na ufisadi ambayo hakuna hiyo….

For Rural Development. Lakini hii imefumbwa na ufisadi ambayo ata haipo.Na hii ndiyo itakayopoza mambo ya huyu ataka hivi,anataka hivi. Hii ndiyo itakayosaidia sana. Kwa hivyo District focus ipewe nguvu ,pesa yote ije huko na ikifika kwa district madiwani wawe huko. Madiwani wana by-laws, wabunge wana laws na sasa pia tunataka by-budget, sio pesa ati inakuja kwa district accountant inakwishia hapo. Kwa hivyo tunataka madiwani wawe nao watatoa jasho ili wajue ni kitu gani kimeingia katika district na wakitawale na haya mambo mengine ya waKenya kugawanyana itakua itakwisha; majimbo itakuwa inakwisha kabisa.

Land, kitu ambacho sisi watu wa Pwani kinatuweka nyuma na wengine wetu wengi kutoka huko bara ni umasikini na ni kwamba land yetu haina dhamana kabisa. Ardhi yetu haina bei. Tukigusa hivi tunataka titles angalau mtu wako akishikwa huko kortini amewekwa rumande huko ukaweze kumtoa, hatuna, umasikini ni tangu jada hapo unaendelea kwa sababu ya kutotumia ardhi sawa sawa. Kwanza wageni wote ambao walikuwa na ardhi hapa wakina masultani wakina nani mtu ambaye si wakenya hiyo title ipigwe marufuku kabisa na katiba yetu.Iondolewe kabisa ardhi irudi kwa state, state irudishe ardhi kwa wananchi.

Pili ardhi yetu, hasa hapa Kinango ni ardhi ambayo wengine group ranch wengine namna hii kama hapa Kinango na mambo kama hayo. Iwe ni lazima kwa Mwananchi wa Kinango ama wa Kenya hii awe, anapata title deed.Pawe ndani ya group ranch kwa sababu hata kama ni group ranch mashamba yako na watu wanachungwa na hawachungi pale shambani it's wrong mtu kupewa title deed ya mahali kama hapo kwa hivyo mimi ninasema hiyo kila mwananchi awe na uhuru wakupata title deed .Mtindo ule wa kisiasa ya kipuzi wakusema ati atauza hiyo shamba yake hakuna vile vitu anavyotaka, watu wanataka title deed wafanye maendeleo halafu tumalize umaskini.

**Com. Barasa:** Haya Nyondo. Nyondo N. Ndolo dakika tano tafadhali usizidishe.

**Nyondo:** Kwa jina Nyondo Ngandu Ndolo, ni mzaliwa ……………Nataka kuchangia katika hizi hoja mbili. kwanza nina mambo kama mawili, matano. Kitu cha kwanza mimi ningeanzia ju, katika katiba yetu hii iliyopita ,rais alikuwa na mamlaka makubwa sana.Ningetaka katika rais wa Kenya wa Jamhuri ya Kenya ipunguzwe kuwe na waziri mkuu.kwasababu sasa ninavyoelewa mimi mwaka wa themanini na sita kulikuwa na madiwani wasio na kazi mingi kwa nini sasa katiba hio, hio hio rais ana viti kama vitatu, mimi maoni yangu ningesema abaki na kimoja ingine mwachie mwingine.

Ingine ni kuongezea katika ardhi ,sisi sote katika Kinango hii ama Kenya wenzetu wana vyeti vya mashamba sisi tuko hapa kama maskwota tunamngoja nani kuja kuchukua nchi yetu.

Lingine ,kila biashara huwekwa orodha kwa nini katika sheria ya makorti hakuna orodha ya bei ya kufanya mashtaka ama

atakayepigwa fine ningetaka hio katiba kama inawezekana na mimi ninasema iwezekana iwe na orodha kila korti kama lile duka kama yule pale hakuweka orodha, awe na makosa kwa sababu ni watu wengi wazee wananyanganywa katika makorti akienda pale hajui mashtaka ni shilingi sabini, yeye anatoa mia nane mashtaka ya hiyo kesi yake ni shilingi sabini pekee yake yeye anatoa karibu shilingi elfu saba.Ningetaka iorodheshwe kila mtu ajue. Kwa sababu yeye hajui anaenda kwa karani anaambiwa ukitaka hiyo case ya mahindi hapo imeibiwa utatoa mia saba na hali case ya ile mahindi imeorodheshwa ni shilingi sabini peke yake. Ningetaka iwekwe bei kama duka.

Lingine ninaonelea, sisemi katika kinango nasema katika Kenya nzima. Sheria iwe sawa sawa, mwanamke na mwanaume kwa sababu tukifikiria dunia ni watu wawili dunia si mtu mmoja. Na tukiendelea katika urithi kwa nini mtoto wakike anaachwa. Kwa mfano mimi niwe ni tajiri, bibi yangu nikimuoa ni maskini na watoto nikiwaacha wale wakike watakwenda wapi? Ndiyo maana ninasema, ardhi Kenya ipewe kila mtu. Atakapokufa huyu mtu, watoto wake wa kike na wa kiume wagawanywe hata kila kipande cha ardhi walichoachiwa.

Basi nilisikia tu kuna sehemu hii ya uchifu. Kwa nini katika katiba ya Kenya haiwezi kubali kwamba mwanamke nayeye awe chifu kama mimi. Basi mimi kulingana na miti mnasema inakatwa lakini mimi nilienda sehemu ya Bara hakuna mtu atakata mahali na cheti lakini mtu aingie hapa kukata mti yako inawezekana, unakata huko kwa sababu ni jagwa na nchi ya wenyewe. Si yetu. Kama ni yangu mimi ikiwa yangu kwani mtu anaweza kuingia kwa shamba akate miti. Ni kwa sababu hatujapewa vyeti. Ndiyo maana sisi hapa tuko maskini zaidi kutawala. Basi nataka kama sheria huko bara katika Kenya nzima sheria ni upate shamba kila mtu apatiwe shamba akiwa mtu wa Kenya. Asanteni.

**Com. Barasa:** Ungetaka uone wanawake wangapi bungeni?

**Nyondo:** Ningetaka tuwe sawa sawa. Ikiwa wabunge ni mia mbili na hamsini, kuwe wanaume ni mia na ishirini na tano na wanawake mia na ishirini na tano kwa sababu tuko sawa.

**Com. Barasa:** Tafadhalini, situnatengeneza katiba na tukitengeneza katiba kitu ya kwanza ni kuheshimu maoni ya mwingine. Si ni kweli? Tusipoheshimu maoni tunawagandamiza wengine. Hata wakisema kitu ambacho hupendi hiyo ni maoni ya nani? Tafadhali wacha maoni iende sokoni ile itashinda nyingine ndiyo itafanya nini; itafaulu.

**Com. Barasa:** Asante sana Mzee Nyondo. Andika yeye. Halafu pale Njira Tsuma. Njira Tsuma atafuatiwa na Nyamawi. Nyamawi Ngoa awe tayari.

**Njira Tsuma:** Mimi kwa jina naitwa Njira Tsuma, kutoka Ndagaye Location, Mwandimu Sub-location. Niko nayo maoni hapa. Kwanza kuwe na kusoma kwa lazima kwa watoto; awe wa kike au awe wa kiume. Ndoa za mapema kwa watoto zitupiliwe mbali kabisa, mzee yeyote atakayemuuoza mtoto wake mapema huyo achukuliwa hatua. Mwanamke pia naye arithi

mali ya wazazi wake sawa na yule mume.

Na pia kuko na lile jambo lingine la mwanaume kutoa sijui yaitwa malu kwa mtu mwingine sasa nilikuwa naonelea ule mzee akitoa malu kwa yule mwingine mimi nami niende kwa yule mwanamke nidai malu yangu.

**Com. Barasa:** Ulisema unaitwa Njira. Hii malu nataka kuelewa. Ati malu ni nini? Is a fine. Nataka kuuliza swali. Na mimi nikirudi huko Nairobi niende huko Western nitasema watu wa Kinango wako na mayowe, noise. Niende niwambie you are noise makers? Then you keep quiet so we listen to each other. Is the issue of adultery very very prevalent in Kwale? Hii mambo ya malu iko juu sana? Si mtakufa na Aids mkufe, mkwishe? Mtakwisha. Huko kwetu ata manamba hawaongei hii mambo ya kulala lala hakuna. Hawa watu wamekataa kufa. Wanakataa. Na nyinyi pia mtaanzia hapo kwa sababu mtakufa muache Pwani yenu bila mtu. Watu wanakimbia hii mambo ya AIDS sana si mkimbie, mkimbie mtakufa mkwishe.

**Com. Barasa:** Sasa twende kwa Nyamawi. Nyamawi Ngoa atafuatiwa na Mzomba Nyanje.

**Nyamawi Ngoa:** Mimi kwa jina Nyamawi Ngoa kutoka Ndavaya nikitoka katika kikundi cha Kema CPO ambalo ni shirika la jamii katika kata ndogo ya Ndavaya na pia nikiwa mwandishi wa KANU katika Ndavaya location. Natoa maoni yangu kuhusu katiba na kwanza naanza na majimbo. Na sababu ya kupendelea majimbo ni kwamba ni kuleta huduma karibu na jamii sababu yangu kubwa ni kuleta huduma karibu na jamii!.

Pili ni kuhusu mambo ya mahospitali, sasa gharama jamii imewazidi ningeomba irejeshwe kama zamani serikali ipeleke madawa kwa mazahanati kama vile ilivyokuwa.kwa hivyo katiba hapo isisitize sana kuhusu madawa iwe kama zamani.

Lingine ni kuhusu mambo ya mazingara hii hasa nataka isikizwe sana kwasababu kuna zile chemi chemi ambazo watu hawazichukuli maanani na ni muhimu sana kwa hivyo ningependa katiba hapo isisitize kwamba mtu yeyote atakayeziharibu hizo chemi chemi anapaswa kuchukuliwa sheria ya kisawa sawa.

Lingine ni kuhusu upigaji kura hii ninaonelea ya kwamba katika upigaji kura, iwe ikihesabiwa katika kile kituo kilicho piga kura badala ya kupelekwa kwingine baada ya kura ikimalizika kura zichaguliwe katika kituo hicho hicho ili kupunguza uibaji kura.

Lingine ni kuhusu vyama vingi, vyama hivi sasa vimefika arobaini na kitu, mimi naonelea vipunguzwe mpaka viwe kama vyama kumi na tena vyama hivyo vijisimamie vyenyewe baada ya serikali kusimamia wao. Kwa hayo machache nasema , asanteni.

**Com. Barasa:** Asante Bwana Nyamawi tuko na Mzomba Nyanje na Mzee Desmond uwe tayari.

**Mzomba Nyanje:** Mimi kwa majina naitwa Mzomba Nyanje kutoka Nzavaya Kema CPO. Hapa naiwakilishe Kema CPO.

Na naanza kuwaelezea maana ya KEMA. Kema ni shirika la jamii la Ndavaya ambalo kwa urefu wafu vile ulivyosema ni kuimarisha hali ya elimu, maji na afya. Kwa hivyo serikali hili limejaribu kufanya uchambuzi pamoja na jamii na wana maoni haya.

Kwanza, uchaguzi wa rais maoni yao wanasema kwamba rais lazima awe na umri wa kati ya miaka thelathini na mitano hadi sabini, awe ni raia wa Kenya ama mzalendo, awe na kura. Si lazima rais ateuliwe na chama chochote cha kisiasa mpaka awe na cheti cha kuhitimu chuo kikuu. Rais awe mamlakani kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano, kuidhimishwa kuwa rais ni afikie ama apate asili mia ishirini za kura katika mikoa mitano kati ya mikoa yote vinane. Kwa matatizo ya kiafya, kifo kujiuzulu; kuwe na haki ya kuwa na rais mshikilizi rais huyu mshikilizi ashikilie kwa muda wa siku sitini badala ya muda wa miaka tisaini. Usalama wa nchi uwe katika kamati ya usalama bungeni wala sio rais huyo mshikilizi.

Makamu wa rais:makamu wa rais achaguliwe na wananchi sio kuchaguliwa na rais kama ilivyo sasa, sifa zake ziwe sawa na zile za rais. Mamlaka ya makamu wa rais, apate kazi ya waziri na awe kiongozi wa shughuli za bunge. Barasa la mawaziri: Barasa hili lichaguliwe na rais na yule waziri atakayechaguliwa awe anakili ya nyadhifa hiyo. Mamlaka ya rais ya kuteuwa na kufuta: kuteuliwa kwa wafanyi kazi waote hasa zinapasa yule mteuliwa anakili sifa za sekta hiyo. Afisi zinawezaundwa na katiba kwa mfano; mkuu wa sheria, mkaguzi wa hesabu za serikali; tume ya wajiri, makatibu wa huduma. Uteuzi huu unapaswa kufanywa na kamati teule mbungeni inayosimamia mambo ya katiba na uajiri si kwamba ichaguliwe na rais.

Tume ya wajiri ya wafanyikazi; wanachama wa tume hili tulipendekeza kwamba wanachama hawa wapatikane kwa kila mkoa ambapo tutakuwa tumepata wanachama wanane kwa vile tuna mikoa minane nchini Kenya. Tupate 'director of personnel management' aingie pale. Wakati wa kufanya mahojiano na wafanyikazi kuwe kuna director anayehusika ndio ahusishwe kikamilifu. Mkuu wa tume hiyo achaguliwe na Rais mwenyewe kuwe na watu watatu kwa sekta ya biashara na viwanda.

Serikali za wilaya; madiwani, kiwango chao cha elimu kianzie darasa la nane ama la aba ama awe na cheti. Umri; kwa kuwa mpiga kura anaanzia miaka 18 basi diwani naye anaweza kusimamia udiwani akiwa na umri hao huo wa miaka 18, awe mpiga kura, awe mzalendo pia. Serikali kuu ipatie serikali ya wilaya majukumu na pesa za kufanyia kazi zao.

Mahakama; mahakama yaanzie ngazi za chini, kuanzia location kwa mfano wakati wa zamani tulikuwa na mahakama Kinango. Siku hizi kuna mzozano wa watu mahakamani.

Uridhi: kuna makundi ambayo yalikuwa yanadharauliwa hasa ya watoto kuanzia umri wa 15. Akifanya au akiuliza kitu kama hapa, anapuuzwa. Tusiwadharau, wao wana maoni na lazima watoe maoni yao wasikike. Pia kuheshimu na kulinda rasilimali zetu kama chemi chemi, misitu, madini, wanyama wa pori pia, tuwalinde kwa sababu hizo ndizo rasilimali zetu za Kenya.

Shirika hili linaomba, tume hili la urekebishaji wa katiba lishirikiane na D.O. kuzidi kuelimisha wananchi huko vijijini.

**Com. Barasa:** Ahsante sana. sasa tunataka Mzee Desmond atafuatiwa na Jonathan Ngumbao.

**Mzee Desmond Kitainge.:** Asante sana macommissioner na wenzangu wote mlio hapa. Kwa majina mimi naitwa Desmond Kitainge. Mbele ya kamati hii ya maoni ya katiba, ningetaka kutoa maoni yangu kama ifuatayo.

Kwanza, swala ambalo ni nyeti katika serikali yetu na nchi yetu kwa jumla ni la njaa. Swala hili mimi ningetaka likabiliwe hivi; kila mkenya mwenye umri wa miaka 21 mwenye afya awe lazima alime eka mbili wakati wa kilimo na apande na azalishe eka hizo sawa sawa ili kuepukana na swala hili nyeti; awe ameoa ama hajaoa, awe yuko kazini ama hayuko lakini apande eka mbili kwa lazima.

Pili, kila mwanakenya mwenye umri wa kufanya kazi na ana afya kamili, iwe ni jukumu la serikali kutoa kazi kwa mtu huyo asije akamaliza nguvu hizo bure tu kwa kunyang'anya watu.

Tatu, serikali hii yetu inawatu aina nyingi. Ina watu ambao ni vijana wa makamu na wazee, na wazee zaidi ambao wamefika wakati ambapo hawawezi kufanya kazi na hawawezi kitu chochote. Mimi napendeza kuwe na 'social welfare fund'. Serikali hii yetu kikatiba iwe na hii fund ambayo itatazamia hawa wakongwe walishwe. Kwa sababu sasa wanapata shida sana.

Nne, kuchangia katibu hii yetu; vyama vya siasa; serikali ilioko na opposition. Mimi napendelea kuwe na vyama viwili tu kuliko sasa vyama 47 ambazo zinaleta fujo, hata zingine ni za kikabila.

Tano, mchango wangu katika kamati hii ya katiba, ni kwamba mwanasiasa yeyote anapo 'campaign' na kutoa ahadi zake nzuri au zipi na ambazo baadaye zinaonekana hatazitimiza kwa wale aliozitoa, wakati mwingine asipewe; asichaguliwe tena kwa sababu aliwadanganya wananchi, wakampenda, akapewa na sasa ahadi alizotoa hakuna hata moja; nitatia barabara lami, na hatii; atolewe kwa sababu hana kazi.

La sita, ndugu ma-commissioner' swala lingine ambalo naona ni nyeti sana ni kuhusu wanyama. Wanyama wa porini sisi tunachukulia ni wanyama tu lakini wanapotia hasara kwa mfano mtu akienda akiua ndovu kwa sababu yaliingilia mahindi yake, yule ndovu ndiye anachukuliwa kuwa ni zaidi kuliko mahindi yale yaliyoliwa katika serikali hii. Ninaomba pendekezo, ushuru ambao unapatikana katika wanyama ufaidishe wananchi; 'the locals' kwa sababu hawa ndio wanasumbuliwa na wale wanyama. Kama ushuru unapatikana kutokana na watalii, wale 'locals' wafaidike zaidi na sivyo ilivyo sasa kwamba wanyama ni muhimu zaidi kuliko binadamu aliyeuwawa katika nchi hii.Ningeomba tena katika tume hili, tume zinazobuniwa kutoka mwanzo, tume hizi ningependekeza ziundwe na kamati maalum kutoka mbunge. Kwa sababu tumeona mbunge nyingi zimebuniwa na faida zake hatuyaoni na tumeona hazina matokeo yoyote. Nikitoa mfano Bombolulu tume iliundwa, tunataka kujua ni kwa nini haikutoa mazao yoyote.

Namaliza nikisema, sisi watu wa Kinango; watu wa Pwani 'cash crops' zetu ni kidogo sana. mnazi kama cash crop na tunataka tembo ya mnazi ihalalishwe. Wenzetu wakionekana na coffee mfukoni kama cash-crop zao hawashikwi lakini sisi tukionekana na mnazi tumebeba tunaenda kuuza, tunashikwa. Katiba iangalie haya, ahsanteni sana.

Nina maoni ya wenzangu wengine ambayo sitaisoma, nitapresent tu.

**Com. Barasa:** Unasema hiyo 'income' inatoka kwa wanyama wa pori iwe inafaidisha watu wa hiyo 'locality' kama percentage gani ipewe kwa hiyo location?

**Com. Barasa:** Jonathan Ngumbao awe tayari na afuatiwe na Benjamin Wambua.
**Jonathan Ngumbau:** Kwa majina naitwa Jonathan Ngumbau.
**Com. Barasa:** Ngumbau ile ya wakamba?

**Ngumbau:** Ile ya wagiriama. Ni mkaaji wa Kinango. Mimi mapedekezo yangu ya kwanza ni kuhusu hii kiti ya rais. Ningependekeza kuwa kuwe na katiba ya kufanya rais asiwe above the law. hapa ni kusema kama kuna wakati atafanya makosa yaani sheria imwandame.

Pili, katika hii multi-party era hii serikali ya vyama vingi ningeonelea hivi, ile party ambayo itashinda alafu kuna ule wakati alafu kuna ule wakati wa kuchagua mawaziri at least wachague kutokana na vile kwa ufupi kuwe na coalition government. Alafu pili nitaenda huko katika local government. Wenye kiti wa maBarasa ya ulaya ama mamayor kuna wenzangu wamesisitiza na kusema kuwa wale madiwani at least wawe na cheti cha darasa la saba ama la nane sawa sawa. Hapo ninaongezea nikisema kuwa mayor au chairman wa county council awe ni wa form four ama above ,alafu nikija tu kwa hii kiti ya rais ningeonelea kuwa yani kwa sababu kuwa na mikoa minane na mimi ni mtu wa hapa Pwana na mimi ningependa hivi kile kiti kina rotate yani kwa mfano kama mwaka atatokea Rift Valley atawale kwa term mbili yani zikiisha asahau twende mkoa mwingine. Vile kutakua na ile tunaita mshikamano wa taifa. Nafikiri kwa hayo machache asante sana kwa kunisikiliza.

**Com. Barasa:** Benjamin Wambua atafuatiwa na Raphael Kazibe ajiweke tayari.

**Benjamin Wambua:** Asante sana bwana mwenye kiti. Kwa jina naitwa Benjamin Wambua kutoka kule chongo mundu Kinango location na maoni yangu nikama yafuatayo elimu ya msingi Kenya iwe ya bure kwanzia darasa ya kwanza mpaka la nane.

Pili polisi wote wavae sare moja hakuna GSU, hakuna anti-drug unit, ama nani wote wavae sare moja kama ni samawati na nyeusi chini wote wavae namna hiyo na namba zao badala ya kuzibandika kwa shati waweke kwa kofia ili kabla haja "kunini" upate kujua namba yake na crown.

Tatu, machief wote na manaibu wao wapigiwe kura kama vile rais ama wabunge. Wakae kwa kipindi cha miaka mitano akiteuliwa tena hivyo hivyo.

Nne, wagonjwa waliyo mahospitalini wapewe huduma za kisawa sawa na mahospitali yawe yakisafishwa maana ukienda hospitalini unapata ni chafu wagonjwa, madaktari hawafiki katiba hii ijaribu kuangalia pande hiyo.

**Com. Barasa:** Na matibabu yenyewe?

**Wambua:** Matibabu; kuna magonjwa ambayo dawa zake kama vile kifua kikuu ziko ghali na magonjwa mengine yawe ya bure na kwa upande wa watu wazima iwe kiwango ni asili mia kumi cha kulipa zile dawa na watoto chini ya miaka kumi watibiwe bure.

Tano, kiongozi wa nchi awe chini ya sheria. Iwe anaweza kukabiliwa na sheria na judge kukua akipitisha kitu kama kuna jambazi anaua mwenzake na amehukumiwa kifo pia iwe ifuatiliwe namna hiyo si ati amehukumu alafu kiongozi wa nchi anasema amemsamehe free atoke la. Judge mkuu akipitisha iwe namna hiyo hiyo.

Sita, elimu ya wabunge – kila mbunge awe na shahada – degree ndiyo aweze kuingia bungeni. Miaka ya rais kuingia kama rais hapa sheria inasema ni miaka thelathini na tano kwanzia thelathini na tano ipunguzwe iwe thelathini. Na ya uzee iwe sitini. Councillors wawe form four sio mtu wa darasa la saba, la sita ata jina hajui kuandika.

Saba, uridhi uwe kwa wavulana ama watoto wa kiume. Sio kwa watoto wa kike. Mtoto wa kike ataolewa ataenda kwa bwana yake ataishi huko. Leo hii kuna nyumba mbili ya mzee, atapewa moja.Ile faida yote mzee alioyopata shida nyingi kwa kujenga, kwa kununua ngombe leo iende ikaliwe na watu ambayo hawajui uchungu wake. Tena kama hakuolewa wazee wa mtaa, machief wako wataangalia maana pia tuko na serikali imeanzia chini. Mzee wa miji sub-chief, D.O, D.C., P.C and even President apate ule uridhi uliyo pale na mzee ile mali ule msichana apate kupatiwa kama asili mia tano hivi kama hakufanya nini, kama hakuolewa. 50% of the total of whatever is there. ni mtoto lakini pengine akaolewa ataenda kuasi kule, akae area pale ama kama hajaolewa mtoto wa kike apewe urithi. Kama hajaolewa apewe kama asili mia tano. Sawa tuko sote

**Com. Barasa:** Tumbo yako ni kubwa kuliko tumbo yake? Au? ndiyo apewe 50%. Tumbo ni ndogo au ni nini.

**Wambua:** Hiyo 5% sio ati tunaangalia kwa upande wa tumbo it is first supportive life. Si ati kwa ajili ya tumbo wala nini. Yaani ile maisha yake ajisaidie na hiyo 5%. Kama mzee alikuwa na ngombe kumi apewe ngombe moja tu. Hiyo ingine ipewe wenye mji. Na sheria zote zichapishwe ili wananchi wapewe wagawiwe zile sheria zilichapishwa kama kitabu ama kwa magazeti wananchi wasisome wapate kuzielewa. Ngoja kidogo tafadhali, na customary laws, sheria za kienyeji zifuatiliwe

maana siku hizi hazifutiliwi kabisa. Na kama vile kumuona kiongozi wa nchi siku hizi ata mimi nikatoka hapa nataka kwenda kumuona kiongozi wa nchi siwezi kumuona. Mambo yangu nitaiachia tu hapa kwa D.C. hiyo sheria irekebishwe kama ni mwananchi wa Kenya aweze kumuona rais kama ako na matatizo kwa urahisi.

Na watoto wa mtaani wale ambao siku hizi wanajulikana kama chokora. Katiba iyaanglie hali ya watoto hao; wakamatwe waregeshwe makwao maana kila mtu ako na kwao. Na kama hana kwao msitu ni mingi wafanyiwe mahali walime na chakula hicho zinaweza kupatikana kulisha walemavu, wagonjwa, prisoners na pia itaweza uzwa na ile pesa itapatikana ikaelimisha watoto wa masikini maana watoto wa masikini siku hizi wanasoma na kufika elimu ya nane hawaendi mahali huko kwetu wako wengi sana na serikali haiangalii upande huu.

**Com. Barasa:** Hayo ni maoni ya bwana Benjamin Wambua. Sasa tuna Raphael Kazibe na Joseph Nguta awe tayari.

**Raphael Kazibe:** Mimi kwa jina naitwa Raphael Kazibe. Niko hapa kutoa maoni kwa hii commission yetu ya katiba uzuri naomba. Tunayoongea muifuate kidogo, muifuatilie msituache hapa.

Langu la kwanza ambalo lasumbua sana na sijui kwa nini wengi hawataki. Kuna watu hawataki Federal government; wengi tunataka serikali ya majimbo, federal government. Hii makosa yake sijui ni nini kwa sababu majimbo ni kuleta utawala karibu karibu na mwananchi. Yangu ni majimbo sasa na hata hayo majimbo tukileta hawa wengi serikali hii, viongozi wanatatua, hawa wetu rahisi kuwapatia maoni na wale viongozi tutakawachagua kama wajumbe wetu wanaenda huko wanaketi pamoja wanaongea pamoja wanapitisha kitu, na ukiwa ni matractor kumi kwa mfano sasa kuna wengine huko wanachukua matractor ya kulimwa mashamba yao bure alafu ulipe. Hapa kuna yapi hapa kwetu? Hakuna. Si yote yalienda mahali kwingine, lakini ikiwa ni majimbo tutapata pengine matano hapo kule wengine. Rahisi kuyapata na njaa nayo tutaipunguza kidogo na mambo mengine.

Elimu sasa. Hii elimu yetu zamani ilikuwa ni bure kutoka mtoto mdogo, kutoka nursery walikua nursery cha kuruka ruku, lakini kutoka class ya kwanza mpaka seven ilikuwa bure na yule mtoto hawezi kutafuta pesa. Hivi inasemekana cost sharing, hivi tunaambiwa ni bure, si bure. Shule hazinjegwi, vitabu hakuna kila kitu kwa hivyo hii cost sharing iondoke kwa mtoto wa class ya kwanza baada ya darasa la nane. Na iwe lazima ata mimi nitafanywa kulazimishwa na assistant chief, singelikuwa hapa.

Nilikuwa shambani nikafika ni kapimwa na baba alikuwa hataki. Nikapelekwa na sasa si nilisoma. Irudi ile elimu ya lazima ilikuwa iko. Hivi tusipofanya hivi mduruma hasomi. Hasa kwa sababu wengine wanatoroka toroka hawataki wamekua wakubwa, kwa hivyo iwe ya lazima.

Tukirudi upande wa hospitali. Upande wa hospitali naye mgonjwa hatafuti pesa nizitafutwe na mwingine na wengine waliwachwa hapo. Kuna watu ambao wenyewe ni kama hawana mwenyewe. Ni mama hakuolewa, anategemea mwenyewe.

Akishikwa na ugonjwa atasema jibu tu, sina pesa ya hospitali alafu anaenda. Kwa hivyo ile hospitali nayo matibabu yawe bure. Ikiwa cost sharing ifanywe lakini yawe bure. Ikiwa cost sharing ifanywe lakini kwa education na hospitali iwe huru. Tutaua wa wengi, sababu nasema siwezi kwenda sina pesa, iwe huru.

Lingine ni chief, utawala sasa, hawa machief tunaomba serikali; ati serikali katiba yetu mpya, muwafanyie interview wale wanaotaka ata kama ni ishirini si wote wananganganía wafanyiwe interview na hatutaki mtu ambayo ana darasa ya chini ataturudisha tena nyuma. Waanzie form four kwenda mbele. Wakafanyiwe interview kama Kwale pengine kokote wanaohusika mkipata hawa wako sawa si wa bunge hufanywo hivyo? Wawekwe kwa raia kwa sababu wengine wana macertificate makubwa wanaishi Mombasa, hajui nani wala nani. Akirudi huko tunamfundisha kazi tena. Hapa sheria yetu ni hii. Hii sheria yetu ni hii yeye alipotea huko na tukimpatia nyinyi mkisema huyu ndiye sawa tumekufa.

**Com. Barasa:** Mnataka awe elected au?

**Raphael:** Afanyiwe interview kule kama hivi wabunge wanaenda wakatoe vyote. Wakiwa wako sawa ile kazi anaweza akaifanya sasa waeletwe huko tuwapatie moja kwa election kama zamani ilikuwa hivyo. Niliona mlolongo ya assistant chief wangu na wengine nilipokua mdogo sasa ikaondoka twataka irudi.

Nyingine tuna hii land imeguswa na wenzangu lakini nayo inasisitiza kutoka mimi nikienda Mombasa nikitaka kujenga pale majengo pale ni ya mtu alitoka huko Oman. Tunalipa yeye mweupe na wetu sijui walikuwa wako wapi. Kutoka hapa tayari Likoni kwenda hivi kuna wengine nao ni weupe, kutoka nje isio ya wageni. Title deed isio za wageni kutoka nje ziwe zetu. Wale zile za zamani ziondolewe bali. Ipewe state, state itagawanya najua itafanya nini kwa raia.

Report kwa polisi. Hii sijui iko hii sheria lakini nayo twataka isisitizwe katiba yetu ifanyie marekebisho. Mtu akishikwa na polisi kuandika statement, awe na shaidi wake. Ndivyo ilivyo na haifanyiki, unaenda pale anafinywa finywa unaandika report ambayo haiwezi kugeuka. Unapelekwa kortini, aliandika hii. Saini ni yako mwenyewe pekee yako we maskini umetoka shambani utandika nini pale. Kwa hivyo polisi wakishika mtu aitwe ule amekuja atasema nijue nani awe shaidi aandike ile maneno yake,aende kortini akiwa na shaidi pale. Asiseme nilifinywa finywa ni nini na kumshika na kumtesa, tesa si vizuri. Akimshika aite shaidi yake, kesho yake peleka kortini.

Nikiendelea na pamoja ni hii carnal knowledge. Mtoto wako anafundisha seven anabandikwa mimba. Akibandikwa mimba ama ata hakuenda shule anabandikwa mimba. Ukiyafuata fuata hivi hayaendi mbali yanafuaytwa tu ya mwalimu wa mwanafunzi. Hapo mwalimu atafutwa. Lakini hawa wote yanaachwa. Kwa hivyo hatutaki. Iwe sheria ukiweka mimba mwanafunzi ustakiwe ufungwe kwanza na uje umuoe kama hajaondoka kwa sababu unamwachia maisha mabaya. Na nyingine ni uchumi wetu nikimalizia. Uchumi wetu unashida, masoko sisi yote yako Nairobi. Tukilima mahindi yetu, tukilima pamba ama tuletewe mimea yetu ni mnazi, mkorosho, mwembe na michungwa; hatuna soko, mashine zote ziko huko. Sasa hata huu mnazi

tuna masoko kidogo, wengine walikua wakisema tuwaachie nazi tutalewa sana. Zamani ilipokuwa na babu kunajengwa nyumba kama hii wanaanza kunywa saa kumi. Pale ile nyumba, pale mwisho ya ule uwanja wanakunywa saa kumi hata ukilala hapo shauri yako. Lakini asubuhi hafunguliwi hayo, ukishikwa unashikwa sasa wale wanawachukua wote kule nyumbani wanawalete hapa Kinango mpaka saa kumi kule watakunywa nini. Si watu waende shambani urudi kama vile aliyekuwa Kenyatta huko mwanzo. Mnazi huru lakini iwekwe sheria na mjenge mabar, nyumba kama hii licence ziweko upate pesa. Kwa sababu kufukuzwa kwa nazi kwa haya mapombe mengine. Hizo whisky zetu ni kali. Unkinywa whisky humalizi glass. Kwa hivyo ni huru.

Pili, namwambia, hii tume yenu kwanini isifike kule vijijini?Tuanaambiwa ati kuna tume.Si ingefika kama kwenye village, kwa machief na watu. Twamuomba mfike huko……

**Com. Barasa:** Joseph Nguta, halafu Mwangoka Mapengu haya jitayarishe.

**Joseph Mwaochi:** Kwa jina Joseph Mwaochi, mimi maoni yangu ni kuhusu mila, mila hasa hapa kwetu, mila zetu zimepunguka kwa sababu ya madini. Dini imepoteza mila kabisa. Sisi kikwetu hasa hatulimi,tunalima siku tatu, siku ya nne tunapumzika twaiita Juma. Leo mtu wa dini hajui mila na dini. Ana vunja ile mila anafuata dini. Na dini pia ni mila ya wenzetu. Sisi twataka mtu yeyote hii siku ya nne inaitwa Juma anayelima anayelima achukuliwe hatua.

Maoni mengine ni mambo ya mnazi. Mnazi ni kitu cha kwanza hasa hapa kwetu. Tunapata pesa na hiyo mnazi. Leo kinacholeta pesa ni mnazi wenyewe. Leo mnazi wenyewe unataka kuuzwa. Hiyo nazi yenyewe huko kwetu hakuna soko ya mnazi. Na hakuna mtu ananunua nazi.

Kitu kingine ni korosho. Hapa kwetu hakuna mtambo wa korosho. Kingine ni chungwa, hapa kwetu hakina mtambo wa chungwa. Sasa mimi napendelea kama huyu Governor, President awe huko na Governor awe hapa. Kwa sababu Rais Moi, kama atafika ata. Tuko na Governor si lazima aende huko. Mimi napendelea majimbo tupate governor wa Pwani, mambo yangu ni hayo.

**Com. Barasa:** Hayo ni maoni ya mwananchi huyo. Tafadhali mpatie aseme anavyotaka. Kama anasema mambo ya korosho, mambo ya mimi mnajua ni kawaida lakini ni lazima tuandike watu wantaka nini. Msione kama anasema mambo inafinya. Aaah, ni lazima tuandike kila mtu anavyotaka na sheria inawaruhusu watu kusema vile wanavyotaka. Kwa hivyo msinugunike kama mtu antoa maoni kama hayakufai. Haya mwingine ni Mwangoka. Alafu nani ajitayarishe – Noma Asikali.

**Ngoma Asikali:** Natoa shukrani kusikia habari ya katiba kwamba inakuja kwa wananchi. Hiyo, shukrani kwanza. Mimi naitwa Mapengo wa Mwangoka Mapengo Mwanauli. Jina la tatu Mapengo. Tatizo langu kichwani kuhusu ni ndovu tu. Kutoka siku hizo zote kulikua hakuna ndovu lakini kwanzia mwaka wa hamsini na mbili ndovu wameanza kuja ama kuletwa.

Sasa ndovu hawa kulikua hakuna wire, wanatembea kila sehemu. Watu wanuwawa lakini ukijaribu kufanya nini. Kujaribu kmfuma ndovu hata usijuwe hapa sijui utakwenda kuchinjiwa sijuwi wapi.

Sasa maoni yangu kwamba ile ilinifanya nije nitoe maoni ndovu akila mahindi yangu nilipwe laki moja. Ameua mtoto wangu au mimi mwenyewe nimeuwawa na ndovu, laki ni mbili nilipwe wale watoto wangu nami. Nami nikimfuma ndovu akifa na mimi nina haki nitozwe hizo laki mbili. Haki kwa haki isije ikaonekana ndovu ni kitu cha maana, mimi si chochote. Hilo nilisikia kwenye gazette ya ndovu kwamba ndovu akiua mtu alipiwe na ndovu akiua mtu alipe. Haya,hilo ni la kwanza.

La pili, natatizika kuna kuja maloan, pesa zikopeshwe sisi masikini. zikopeshwe sisi masikini hizo pesa na hakuna hata mtu moja ambaye atakopeshwa katika area hii. Pesa hizo sijui zinaenda wapi, sasa basi zikija pesa hizo, kama hapa ni hakikishe hata kama nimekosa mimi lakini amepata ndugu yangu, shemeji yangu, sijui mama fulani. Nijue pesa zimeletwa Kwale kuja kusaidia wenye kule bomani. Tuhakikishe kwamba amekopeshwa lakini sasa sababu kwamba hakopeshwi, maskini hana kitu ya kushika. Sasa akiwa hana cha kushika basi kunatakiwa Title deed, mimi sina title deed mkopo huyu nitaipata? Halafu mashamba yapimwe niwe nikipata mkopo. Hilo ni neno la pili. Sasa kwa hivyo najua wenzangu hapa wanayo ya kusema, muhakikishe mimi nimesema ya ndovu alipiwe na mimi nilipwe na loan nipate. Asanteni.

**Com. Barasa:** Ngoma Asikali. Ngoma atafuatiwe na Mwachi Mwauche.

**Ngome Asikali:** Mimi kwa majina naitwa Ngoma Asikali Hamisi kutoka Puma Locaton.Nina maoni mawili ya kuwasilisha mbele ya tume hili. Oni la kwanza mimi kimaoni ningependelea kwamba mwananchi wa Kenya hii huru anapokua na matatizo, anapokwenda katika ofisi ya chief aweze kupeana hiyo ripoti bure bila yakuitishwa kitu chochote ati akidaiwa ni garama ya mashtaka. Maneno ninavyoelewa ni kwamba chief yule hangeandikiwa kazi hiyo ya uchief ni kwa huduma ya raia wa nchi hii.

Pili tukirudi katika ngazi ya Assistant Chief ama chief mdogo tunaona ya kwamba katika ofisi za chief zinajengwa katikati ya location ama katika pembe moja ya location hiyo. Na kama serikali ilionelea kuna umuhimu ya kumwandika kama Assistant chief ili aongoze sub-location, kwa nini haingemjengea ofisi katika pembe ya sub-location hiyo? Hiyo ndiyo maoni yangu nimemletea leo. Nasema asante.

**Com. Barasa:** Asante sana kwa maneno hayo mafupi lakini ya wazi kabisa. Mwauchi Muluche na atafuatiwa na John Chimandu.

**Mwauchi Muluche:** Jina naitwa Mwauchi Muluche kutoka Puma location. Mimi kwa kuunga mkono mengine yaliyosema na katiba hii ya leo, mimi sina mambo mengi .Kwa vile sisi hatukusoma tumewekwa nyuma siku nyingi ndiyo maana tukipelekwa polisi tunapigwa mpaka kufa. Hilo ambalo tukilifanya ifanywe, kwa sababu hii Kwale yetu tuseme vile unavyoteswa hakuna nchi ingine inateswa kama Kwale. Hasa wazee wanaonewa sana. Ukishikwa na kosa kidogo unateswa sana kutoka kwa polisi

yaani utumishi kwa wote.

Hii utumishi kwa wote ni mbaya sana sisi tunakufa kwa sababu hii wanawake watatoka huku Mkongani kuleta tembo Kinango apate riziki. Walifungiwa kila kitu riziki apate riziki huyu mwanamke atafukuzwa polisi mpaka ashikwe, akishikwa bila kutoa mia mbili tembo litanywawa bure na hatapata chochote. Kusema mwananchi kawaida hana haki katika Kenya yetu. Kuhusu mambo ya elimu ndiyo iko juu sana tuseme Kenya nzima lakini kuna Kwale kwa vile hatujui kusoma ndiyo mambo imezidi. Katika Kwale yetu kwa hivyo tunataka kutoka class ya kwanza mpaka ya nane iwe ni bure. Na ilikwako sijui ni nani katiba ilikuja geuzwa ikawa ni pesa sasa. Wata wanalipa pesa. Kwa mtu kama amepeleka mtoto wake Secondary asitaabishwe kama mimi sina kibarua na ni mzee tu. Wazee sasa utataabishwa ulipe elfu ishirini kwa mara moja. Hiyo inalemea watu wa Kinango na hiyo nafikiri kwa katiba iyangaliwe ukirudi kwa mambo ya hospitali, tukiambiwa tugawanye gharama, sijui gharama hiyo ya nini, hatujui sisi, ukifika pale kuhudumiwa pia huhudumiwi vile vinaendelea kwa jumla tunataka ile hospitali iwe ni bure. Kutoka ukilala ata nini iwe ni bure.

Tukirudi upande mambo ya maendeleo, katika Kinango hakuna, we mwenyewe, nyinyi, watu wa katiba mkitembea hasa kupita hizi njia mtaona watu wamebebwa kama makopa kwa sababu inatakikana wafe wasiendelee. Kwa hivyo hiyo katiba iangalie mamboyetu ya maendeleo yetu ya Kwale, kwa hivyo sina mengi nashukuru, asante.

**Com. Barasa:** Nikuulize swali? Hii mnazi hata ingawaje ni haramu, naweza kuona kidogo namna gani?

**Ngoma:** Pombe ya mnazi si haramu.

**Com. Barasa:** Nataka kuona kidogo kwa glass. Nataka kuona tu.

**Ngome:** Kama utarudi hapa nitakuletea.

**Barasa:** Nataka kuona leo. Leo.

**Com. Barasa:** Na uulize glass mbili, hata Bishop anataka.

**Com. Barasa:** Nataka kuwambia tu mzee Mulache hakuna sheria inasema watu wa Kinango tu wawachwe wafe tu hivi hivi hakuna.

**Mulache:** Iko. Iko.

**Com. Barasa:** Hakuna sheria hiyo. Kama kuna watu wanakuambia hiyo basi wanakudanganya au kama we unaona hivyo sio

kweli.

**Com. Barasa:** John Shimandu atafuatwa na Asha Saidi.

**John Shimandu:** Mimi kwa jina naitwa John Joseph Shimandu Mudoe kutoka Puma location kisonzu sub-location. Mimi ni mkulima, maoni yangu ni kwamba nataka serikali moja under one president na huyu president qualification zake hata elimu mimi ile ambayo atakua nayo haina neno. Lakini nataka awe millionaire nina sababu. Sababu nikwamba akiwa president ni millionaire, hataweza kuwanyasa wananchi kwa sababu yeye anayo mali lakini akiwa hana mali ndiyo ananyemelea zile za wananchi zaidi.

Pili, veterinary department, niko kwa idara hii ya wanyama. Hii idara mimi ningepedelea irudi kama zamani. Na sababu zake ninazo kwa sababu hapa katika jimbo la Pwani, Coast province sisi ni wafugaji na ikiwa ni wafugaji kuna magonjwa mbali mbali inaaffect hawa wanyama. Na sisi kwa mfano, mimi mwenyewe nilielimika ya kutosha lakini sikusomea upande wa utabibu wa wanyama nilisoma in general. Kwa hivyo magonjwa mengi siwezi kuwajua na ndiyo tunakua wakosefu kwa sababu ya wanyama wanakufa zaidi ile tunawatibu bila mpango.

Lingine, la tatu hilo ni hii upande wa Judicial department, yaani upande wa korti. Wananchi wanapata taabu ya kutravel, kutembea mwendo mrefu kutoka Mwanguru mpaka Kwale, kwa saababu ya mashtaka. Mimi ningependa irudi kama zamani yani part time court.

Nne, ni upande wa land. Hiyo imesemwa na wenzangu lakini mimi nasisitiza hiyo. Macase mengi hayaishi hasa hapa katika Coast province ama Kwale district kwa jumla. Ni sababu ya ukosefu wa kumiliki ardhi, kila mtu anasema hii ni ya babu, hii ni ya sijui nani sasa mwingilio huu unakuwa hauna maana lakini kila mtu akipata namba yake, kwa mfano mimi nina namba, labda mbili kwa sehemu ya mji wangu ambao uko Kilasini “A”. sasa hiyo shamba hata nikisha mwaka moja, wewe lima lakini mimi mwenyewe nikija nitatuondoa na hakuna maneno mengi mimi nitaonyesha namba, we utakuwa huna namba. Hii ardhi ya serikali yetu tukufu tutaiunda hivi,karibuni iliangalilie hizo zaidi.

Tano, ni upande wa idara. Siingili mtu lakini nasema kuna ujumla upande wa hawa wasimamizi wa usalama wanachelewa mahali ambapo kumetokea danger ama accident ama habari chafu fulani. Hii iwe kama zamani ,yaani zamani tulikuwa tunasema haraka, yaani haraka ni upesi.Jambo linatendeka na polisi achukue hatua haraka iwezekanavyo bila jambo kuongezeka.

Mwisho, nasema kwamba utaratibu wa masoko; utaratibu wa masoko ikiwezekana serikali tukufu ambayo tutaiunda iweze kuwakumbuka wananchi kwa masoko zaidi, kwa mfano mimi ni mzee hapa, nilisoma nilifanya kazi ya serikali niliretire, sasa nimfugaji sasa mazao yangu hayana mahali, unafikiri naweza kuishi namna gani? Masoko zaidi yapanuliwe. Asanteni sana.

**Com. Barasa:** Mwingine. Sasa ni mwana Asha Saidi. Njoo mzungumzie. Na J. Nzalila awe tayari.

**Asha Saidi:** Mimi ni Asha Saidi kutoka Kinango ninasema mama, mzee akifa watoto wapate urithi na mama apate urithi. Mtoto msichana apate urithi wa baba yake, ya kwanza.

Ya pili, nasema hospitali ziwe za bure kwa sababu watu wanakufa. Mtu anashikwa na ugonjwa na anashindwa na kwenda hospitali kwa sababu anajua kunatakikana pesa na yeye hana. Mtu anakaa tu nyumbani akijikaza tu kwa vile hana pesa.

Ya tatu, nasema wale akina mama waliachukuwa vitambulisho.kitambo kulikua na sheria ya hapo kwanza kwa akina mama kuchukua vitambulisho na majina ya waume zao. Wakiachana inakua shida kubadilisha hiyo kitambulisho tena kwa kurudisha jina la baba yake. Kwa sababu waume wenye wako hai na pengine hataki. Kila ukienda kufuata kitambulisho unaambiwa ukalete agreement ya huyo bwana ile amekwandikia ni kweli amekuacha. Na ukifuata wanaume wanakataa. Kwa hivyo akina mama wanapata shida wanakaa na majina ya waume ambao hawako nao. Na yanaweza kuwa hatari kwa sababu anaweza kuwa anafanikiwa baada ya kuwachana na huyo bwana, amenunua hata gari, amenunua hata nyumba, amenunua hata shamba halafu akifa yule mama, bwana anakuja kutaka ile mali kwa sababu ya ile jina lake. Itafutwe sheria ya kuondoa ili jina kwa urahisi bila kusumbuliwa. Kwa maana mtu ameachwa karibu miaka thelathini na mtu jina ni la huyu mtu ambaye amekuacha.

**Com. Barasa:** Hukupindua jina lako ukiolewa. Ukiwa tu na jina yako kwa ID ndiyo mzuri.

**Asha:** Ndiyo nasema kwa sababu hapo jana,jina tulikuwa tunaambiwa tuchukuwe kitambulisho na jina la bwana. Ulikuwa ukiambiwa bwana wako anaitwaje, unasema inaandikwa hapo, wanaandika jina lako na la bwana kwa kitambulisho. Baada ya kuwachana naye inakua shida sana kulibadilisha hiyo jina kuliita la baba yako. Kwa sababu uliandika kitambo. Halafu baada ya kuendelea kuishi wewe, yeye akifa ukienda huko hupati kitu utaambiwa uliachana naye kitambo. Lakini wewe ukifa atakuja kwa sababu atasema ni bibi yangu kwa sababu jina yangu iko kwa kitambulisho.

Kwa hivyo iwe ni sheria ambayo inaweza kuwa rahisi kwa mambo ya kitambulisho kutubadilishia akina mama majina ya mabwana zao wale wameachana nao. Tume isaidie. Asante.

**Com. Barasa:** Nzavila atafuatiwa na Kilawa Mathaka.

**Nzalila:** Asante bwana commissioner. Mimi naitwa Joseph Nzavila Nzua. Ni diwani maalum kutoka Kinango location. Maoni yangu ya kwanza bwana commissioner ni hii memerandum yangu nimeandika kwa lugha ya kingereza lakini nitatafsiri haraka haraka ili nijaribu kumaliza kila mahali nilikuwa nataka katiba irekebishe.

Yes, ya kwanza ni hii citizenship yaani uraia mimi nasema kwamba ikiwa mtoto ambaye mzazi wake moja si mtu wa Kenya

isiwe kuwa automatic citizenship. Isiwe automatic kwasababu kuna wazungu wamekua hapa wakisema baba alizaliwa hapa tukampatia citizenship na baadaye anatwambia anawacha watu wake hapa. Ndiyo sababu asiwe na automatic citizenship.

Ingine ni documentation. Documentation ni kwamba raia wa Kenya yeyote sio lazima sana awe na kitambulisho ndiyo atambuliwe ati yeye ni mwanaKenya. Ata akiwa na leaving certificate ikithibitishwa kwamba yeye ni mwanakenya awe anachukuliwa yeye ni mwanakenya. Na awe na ruhusa ya kuweza kupiga kura awe amefikisha miaka kumi na nane aruhusiwe kupiga kura sio awe na kitambulisho ndiyo apige kura.

Basic Rights. Hapa mimi nasema kwamba wafanyi kazi wote wa Kenya wawe na ruhusa ya kuwa na chama chao cha wafanyi kazi, Trade Union ili waweze kulindwa. Civil servants hawana, kwa hivyo wawe na chama chao wasiwe wakinyanyaswa. Wafanyi kazi wa serikali ile civil servants yao irudishwe. Tukija kwa upande wa education, serikali iweze kuwa guarantee wananchi elimu kutoka darasa ya kwanza mpaka secondary level bure.

Tukija upande wa kurekebisha sheria upande wa kurekebisha sheria wa bunge wasiwe na uwezo wa kubadilisha sheria kule bunge kwa sababu hivi sasa wabunge wanaweza kurekebisha sheria kule bunge bila kulete kwa wananchi. Mimi nasema ikiwa wanataka kurekebisha sheria kule bunge iletwe kwa wananchi kwanza. Wananchi wasikie ili mwananchi akubali kwamba sheria inarekebishwa. Ndiyo kwa sababu watu wengi wanazungumza habari ya ndovu hapa, wao wabunge ndiyo walipitisha kule parliament mwananchi akiuawa na mnyama ama ndovu, akila mimea ya watu wasiweze kulipwa. Hivyo basi sheria irudi hapa sisi tusomewe turekebishe sisi wenyewe pia.

Na power za kurekebisha sheria kule ni 65% tunataka iwe 75%.

Na protection of security sasa. Hii security mimi na amini kwamba polisi wetu. Tunataka polisi wote wawe wanaishi katika kambi yao. Hivi sasa serikali hata watu wa hospitali, wafanyi kazi wa hospitali wanaambiwa wapangize nje, wavacate government houses. Sasa kwa wakati huu hakuna tena emergency cases. Unachukuliwa we mgonjwa umepata accident unapelekwa hospitali ukifika pale wauguzi hawako kwa sababu wamepangiza nje. Sasa tunataka hii polis department and ministry of health, ministry of education, zichukuliwe kama essential services. Wabaki kwa compound zao. Ndiyo naona pia nikija kwa education ukisikia watoto wetu wanachomeka ni kwa sababu walimu hawako katika compound yao ya shule. Walimu walale katika compound zao za mashule ndiyo waweza kulinda watoto.

Kenya revenue – mimi nasema kwamba hapa coast tuko na hizi resources. The resources I mean kama Kenya Ports Authority; Kenya Ports Authority hi bahari ni bahati yetu sisi watu wa Pwani.Mungu alitupatia,kwa hivyo hii bahari, revenue yake ile inapatikana mapato ile inapatikana baharini pale, Kenya Ports Authority Pwani yenyewe ipate 70% hizo pesa, hizo revenue ziweze kufaidisha Coast hapa badala ya kuwa revenue zote sinaenda bara. Tunaimba miaka na miaka hapa kwamba barabara ziwekwe lami, ziwekwe lami hakuna. Lami inawekwa kule juu kwa sababu percentage kubwa ya mapato kama hizi, resources

zetu zinaenda upcountry. Tuje katika hizi resources ninasema Kenya Ports Authority , viwanda ya ndege Kenya Airways, Moi International Airport iko hapa kwetu na hizo resources kama hizo za railways na zingine zozote hata barabara ni resources.Revenue ziwe zinaweze kufaidisha Coast province. Mimi siwezi kujua ni percentage gani tunapata saa hizi lakini hizi resources bila shaka hatupati percentage kubwa sana. Na mimi karibu ninamaliza yangu.

Mambo ya lands; Mimi ninasema kwamba upande wa ardhi; Kila mwanakenya apewe shamba na kusiwe na malandlords wale ambao, mtu yuko ulaya na ana shamba hapa Pwani na yeye hata hiyo shamba hailimi lakini ameilease, kule kulease hizo shamba kwa muda wa miaka mia moja ni nani ataishi miaka mia moja hapa? Hiyo lease iwe reduced to thirty years only. Ikiwa huyo mzungu amelease hiyo shamba kwa miaka mia moja naye hayuko ako ulaya basi mwananchi mwenyeye apewe hiyo shamba alime. Ni sawa sawa, kidogo tu.

Now culture. Culture watu wamezungumza sana hapa. Culture mimi ninasema vile vile, utaumanduni wetu uhifadhiwe. Sio kuua, Waswahili wanasema, mwacha mila ni mtumwa. Kwa hivyo culture izingatiwe na vile inafanya kazi. Ya mwisho kabisa,watu wanazungumza sana kuhusu kinywanji cha mnazi. Mimi nasema ifanyiwe research, sio kunywa tu tunakunywa peke yake ama makuti ama fagio lakini ifanyiwe research mnazi. Inaonekana mnazi ni kitu cha faida kubwa ifanyiwe research isije kudharauliwa. Iwe ni mti ambayo kwamba itakuwa inapewa hesima kubwa. Ifanyiwe research na ikiwezekana hata hiyo pombe iwe itaweza kuuzwa katika ma bar. Kenya ipate pesa na coast yenyewe vile vile ipate percentage kubwa kwa hiyo mnazi. Asanteni.

**Com. Barasa:** Asante sana mzee Nzavila. Kilawa Mathaka atafuatiwa na Monica Mohanji.

**Kilawa:** Leo kuna mambo.Asante sana tume ya uchaguzi. Wenye katiba ,hatujazoea kwa namna hii kuongea lakini tutajaribu. Mimi kwa majina naitwa Kilawa Mathaka. Sina mambo mengi ya kuongea kwa sababu mengi ni yale yameongewa na wenzangu. Lakini kuna mahali tu naona niko pekee yangu maana sikupasikia. Mimi maoni yangu nimeonelea kupunguza mamlaka ya rais. Alafu Kenya kwa serikali inaokuja kuwe kuna waziri mkuu. Na sababu yake;nimeonelea mambo mengi yameongewa ,tunazunguka lakini ninatafuta ugonjwa ama kiini ni nini. Tukaonelea ile serikali ilikua inaweza sisi wananchi tuwe sawa iko mikononi mwa mtu mmoja. Kwa hivyo lolote mbaya, nzuri inatokea kwa sababu ni yeye. Kwa sababu hiyo si kuweza kufundishwa vizuri na hii tume ya katiba. Lakini ningepegua nikajua huyu waziri mkuu kazi yake ni nini? Lakini nikiulizwa naweza kusema mawaziri ndiye atakayewateua. Ndiyo atakayewateua judge mkuu. Unaona sasa huko kwa sababu sikuingia huko ndani sikufundishwa ni kauliza maswali nikaelewa. Kwa hivyo kuko wengi kuna kitabu juzi tuliambiwa kilikusanya mambo ya ulimwengu sheria mtanisaidia na hapo.

Kwa hivyo yule waziri mkuu atachaguliwa na wananchi wenyewe. Ili mwananchi awe na sauti. Hayo nimemaliza narudia tu kuunga mkono. Ata kasehemu kalikotajwa na jua ni aibu lakini lazima kaongewe kwa sababu kalikuwa na maana yake. Malu, maana ya malu ama pale palipoanza chanzo cha malu kulikuwa mtu alipatikana na bibi ya mtu anaenda uwawa. Wazee

walipoketi wakionelea tutafanya nini ili tusiuane. Akaonekana yule mzee ambaye bibi yake amepatwa na yule mukilawa akapewa kitu chochote si anaweza kuridhika. Unaona wakakubaliana kwamba anaweza kuridhika. Mafaa ikaisha wakati huo. Sasa kuondoa nikua tunarundisha uuaji. Kwa hivyo ile ilikuwa ni sehemu ya coast province. Yaani nasema kwa Kenya nzima lakini hiyo ndiyo ilionekana na wazee wa zamani kuwa ilikuwa ni kinga kuzuia maafa. Kwa hivyo malu isiondolewe. Mimi vile navyoinelea kwa sababu hiyo natukiondoa tukumbuke tumeondoa watu wauwane. Naongezea tu ni kuunga mkono. Nikikumbuka serikali ile ya Kenyatta na hii ni serikali ndiyo moja isio na tafauti na kwa nini tulikunywa dawa bure na shule tukasoma bure lakini hivi leo hospitali tunalipa, shule tunalipa, wengine wanashindwa na kufundisha na serikali ni hivi moja. Kwa hivyo shule ziwe bure na hospitali ziwe bure. Kuna mahali ambapo kama ningefundishwa zaidi ningeingia ndani mpaka nikajua ninaongea nini. Lakini mtanisaidia nyinyi kupitia kwa kile kitabu kile mlitwambia kilikusanya mambo yote. Ilikuwa kila baada ya mwezi wa nne miaka hiyo 1963 mpaka kuja kushika 1979 ilikuwa budget ya vitu ilikuwa badala ya kupunguzwa peni, inaongezwa ndururu.Ndivyo ilikuwa na hiyo ilikuwa serikali kama hii unaona. Maoni yangu, yule alikuwa ameshikilia mnamjua nyinyi ambao mmesomea katiba kutoka huko mpaka mnatuletea mnajua hayo ilikua ya nani. Na tayari nilijua kwanza ilikua ya Kenyatta mwenyewe kama rais unaona. Alikuwa yeye akisema nimepunguza ndururu imepunguzwa Kenya nzima. Leo imekua pale ni shilingi kumi hapa ni shilingi mbili.Yule ni shillingi tano. Tuko wapi? Unaona. Mwananchi anateseka sasa. Na hakuna kitu kikubwa vile naonelea, hakuna kitu kikubwa ama hatari kuliko chakula. Chakula kikiwa juu mwananchi anakufa. Hospitali na chakula. Mwananchi anakwisha. Maoni yangu nilikua nikija hapa niseme, twache kundanganywa tukiambiwa ati mwananchi ndiye tajiri hilo liondoke. Mwananchi ndiye tajiri na hadi mwananchi anakufa na jaa. Ule aliyemwajiri yeye tumbo iko hapo. Tuko wapi? Tumepotelea wapi wala tunapoteswa wapi? Wale wanaohusika.Yangu ni hiyo machache.

**Com. Barasa:** Mzee anasema yeye hakupata civic education lakini maneno anayosema ameyafikiria sana. Haya Monica Mwahanji. Halafu huyo ni mwana chama wetu wa CCC halafu atafuatiwa na Keya Dalu Mwahanji.

**Monica Mwahanji:** Kwanza ninashukuru kwa kupewa nafasi hii. kunayo mengi nimeandika katika hii karatasi lakini nitagusia tu points kidogo. Na nitaanza kwa kusema hivi ,katiba ijayo kwanza iwe na utangulizi na iandikwe katika lugha ambayo kila mwananchi itakuwa rahisi kuisoma na baada ya katiba hiyo kutolewa kila mwananchi aipate ama aipitie ili ajue ni kitu gani kinamlinda na wapi aendelee. Kwa sababu hata kwa sasa tunasema mwananchi atoe maoni lakini ile elimu kidogo aliyoipata kwa civic education haitoshi mwananchi kutoa maoni lakini wakati hiyo katiba ikitoka na akiwa nayo mkononi basi ataelimika zaidi ama atajua zaidi ni sheria gani zinamlinda akiwa mwananchi.

Neno la pili nitakalolizungumzia ni kuhusu elimu. Elimu kwanza ningetaka urudi mfumo ule wa zamani, saba-nne-mbil-tatu na iwe ya bure nikisema ya bure ninamaanisha ya kwamba serikali igaramie upande wa vifaa vya shule vya masomo kwa sababu mzazi anagaramika sana analipa pesa nyingi anashindwa na kununulia hata mtoto na vitabu ama vifaa vile vinahitajika na hio inazorotesha hali ya kielimu. Pia kuhusu elimu ningeomba kuwe na sheria maalum inayomlinda mtoto msichana, kwa kusema kweli watoto wetu wasichana wamegandamizwa na ni kwa sababu hakuna sheria ambayo inasimamia hasa kuhakikisha huyu mtoto wa kike pia naye anapewa elimu sawa na mvulana, hasa upande huu wa kwetu inakuwa mtoto wa kishicana ni rasili mali

ya kusomesha mvulana.

Ya tatu, eeh nitazungumzia kuhusu akina mama ninataka kuwe na sheria ambayo itamlinda mama mwenye uwezo wa kuweza kupata nafasi ya kazi popote pale apatiwe isiwe kwamba tunakaliwa na hawa kina baba kiasi cha kuwa hata kama elimu yangu ama uwezo wangu unananitosha kupata kazi kiasi fulani, ama jukumu, ama uongozi kiasi fulani basi inakuwa kimila ama labda wanaume wanaona mwanawake hawawezi kutuongoza.Ndiyo pia nasisitiza kusema kwamba hasa katika nafasi hizi kwa mfano za udiwani, ubunge na eeh udiwani na ubunge hasa na hata urais. Ikiwezekana kama nafasi kwa mfano kwa ward za udiwani ni kama ishirini basi kumi ziwe za mama na kumi ziwe za baba na hata pia ikiwezekana kuwe na hazina ambayo itamsaidia huyu mama kusimama kisawa sawa kisiasa na aweze kunyakua nafasi hii, kwa maana si rahisi mama kutafuta njia za kujipatia hali ya kujisimamisha maana tuligandamizwa kutoka kitambo.

Ya nne serikali iwe pia itakuwa na sheria, ama kuwe na sheria ambayo itamlinda huyo mama kiasi cha kwamba atakuwa na haki ya kurithi mali ya mumewe. Katika mila zetu ama desturi nyingi nikwamba mzee anapofariki pengine mama huyu inakua ati ile nyumba niirithiwe na ndugu ya mumewe. Na mama huyu inakuwa ni wa kunyanyaswa saa zote. …..

**Monica:** Ile nyumba iridhiwe na ndugu wa mumewe na mama huyu amekuwa wa kunyanyaswa saa zote. Mali ni ya bwanake lakini hana hukumu nayo.Hata ikizidi anafukuzwa; mara anaambiwa hataki kutii yule bwana ameachiwa nyumba, kwa hivyo ninawaomba serikali hii itoe sheria itakayo msimamia mama. Mali ile iko pale nyumbani ni mama na mzee wake ndio walitafuta; kwa nini leo iridhiwe na mzee na ana nyumba yake nyingine? Mama huyu abaki kuteseka na wale watoto?

Pia nikiongezea upande wa akina mama, watu wakiwa wazazi na mimi nikiwa mmoja wa wale wazazi, wazee watukubali kwamba hata mtoto wa kike ana haki ya kurithi mali ya wazazi wake. Nikiwa mimi ni mzazi; labda pengine nilielimisha mtoto wangu wa kike, ameolewa; awe ana kazi, hana kazi ,hata hakusoma lakini mahari nilipata. Nafurahia kule kupata mahari; mtoto wangu akiteseka, sioni vile kwa nini na mtoto wa kike ni mtoto kama mwingine. Ukitaka mtoto wako wa kiume aishi vizuri hata wa kike ni mtoto wako kwa hivyo ni haki uyajue maisha yake na ni haki umpe urithi.

Kwa vile muda umeisha nitaenda haraka haraka kidogo. Kuna ‘point’ muhimu sana ambayo nilikuwa nataka kuzungumzia. Iwapo, nilikuwa naonelea pia bunge ipewe mamlaka ya kuangalia hawa watu wanaoteuliwa katika nyadhifa mbali mbali kwa sababu wakati mwingine kunateuliwa watu ambao labda kimasomo au kiutaalam ile kazi aliyopewa au ile wizara aliyopewa hawezi kuisimamia vizuri. na wakikuta mtu kama huyu,waziri kama huyo asiweze kupewa wizara nyingine nayo pia akaiharibu. Ahsanteni!

**Com. Barasa:** Haya asante sana mama. Ametoa maoni yake; nasikia kuna wazee huko nyuma wananug’unika nung’unika lakini leo ni wakati wa kuambiana vile tunavyotaka. Sasa baada ya hapa, sisi wenyewe tukae chini tuangalie tumekuwa tukifanya nini na lazima turekebishe wapi. Baada ya Monica, ni Bwana Kea Dulu atafuatiwa Rev. Samuel

**Kea Dulu:** Maoni yangu kuhusu katiba ijayo; ningependa ishughulike sana hili swala la umaskini. Umaskini kwa sababu gani? Kwa sababu gani watu wamekuwa maskini sana? Kwa nini? Wakati ule wa pale mwanzoni kidogo hali ya maendeleo ilikuwa bado iko chini sana na kulikuwa na sababu ya watu kuwa maskini lakini kwa wakati huu wa sasa ambapo Kenya imepiga hatua; ajabu ni kuwa watu wamekuwa maskini sana kupindukia. Kwa nini watu ni maskini?

Mimi nafikiri kuwa hii serikali ndiyo inalazimisha watu wawe maskini ili waweze kutawalika kwa urahisi.
Angalia mfano, kina mama wengi hapa Kinango ni wafanyi biashara wadogo wadogo; pengine mtu 'stock' yake ni ya kama 200/-, anauza uza kidogo apate 40/- kwa siku. Hapa unaona asubuhi anakanygiwa na mtu wa county council ambaye ni 'agent ' wa serikali. Anaambiwa toa 22.50. sasa hii 22.50 itatoka wapi kama mali yenyewe haifiki hata 500/-? Kama mama hatatekeleza hatua hii, hata leso yake inachukuliwa. Kesho mtu wa 'county council' tena huyu anataka 22.50. serikali ndiyo inachangia katika hali hii ya umaskini; kwa sababu gani tena?

Angalia kulikuwa na mtambo wa kusaga sukari 'kuramisri' ulikuwa unaajiri watu wengi ambao wanasukuma mbele hali zao za maisha. Uko wapi mtambo huo sasa? Serikali naipendekezea kuwa ije na 'policies' ambazo zitahakikisha kuwa masilahi ya huyu mtu wa chini kabisa yanaangaliwa kiasi cha kuwa anasaidiwa kwa njia yoyote ile katika kuupunguza huu umaskini ili na yeye aweze kufurahia the 'fruits of independence'.

Education; napendekezea kuwa serikali ihakikishe ya kuwa education inakuwa 'free' and 'compulsory'. Iwe lazima na sio serikali kusema tu "iko huru, iko huru", lakini kidogo mtoto amerudishwa nyumbani. upto Std. 8 iwe free halafu baada ya hapo kama mtoto ni bright na anatoka katika familia maskini, kuwe na njia za kuhakikisha kuwa mtoto huyu haswa hawa kutoka hizi area za maskini anasukumwa sukumwa mbele ili baadaye aje asaidie katika ujenzi wa kusukuma mbele maisha ya wengine.

Health: Hii mambo ya kusema mambo ya 'cost-sharing' imeleta hasara kubwa sana hasa huku ambako watu ni maskini. Watu wanakufa kula siku akina mama wanajifungulia nyumbani wanakufa kwasababu ya 'cost-sharing'. Hii mambo ya 'cost-sharing' ipigwe marufuku kabisa kwa sababu tayari tunalipa ushuru; hiyo tayari ni 'sharing'. Tunalipa ushuru sasa wakileta tena cost sharing that is double taxation. Tunalipa ushuru mara ya pili. Kwa hivyo mambo ya health - hospitali ziwe bure. Mwisho serikali pia tuanipendekezea ije na njia ya kuhakikisha kuwa wale ambao wanatembea tembea huku na kule wakiwaharibu watoto wadogo-watoto wa shule za msingi, watoto wa shule za sekondari na kuwapatia AIDS wao wapelekwe mahakamani na kunyongwa, ikifanyika hivi wale wengine ambao wantabia kama hizi basi watakuwa wamepata funzo na watalazimika kubadilisha tabia zao. Yangu ni hayo.

**Com. Barasa:** Ahsante sana Bwana Dulu. Reverend Samuel Kiondi,I give you five minutes.

**Reverend Kiondi:** Asante sana mwenyekiti. Mimi yangu ni kwamba katiba iweko ama isiweko marekebisho, uchaguzi uweko

kwa sababu hata ile katiba ya zamani inasema vizuri sana lakini wale watu wa kuifuata hawako kwa sababu inakataa hata hongo lakini ukipatia kila upande kitu kidogo kiko.Hiyo nikumaanisha wale ambao wanatakikana kuilinda ile katiba hawailindi sawa sawa.Yangu ni kusema kwamba mamlaka ya Rais inatakikana ipunguzwe kabisa ili Rais asije akawa na mamlaka zaidi sana ili watu wasije wakafanya kazi chini ya huruma zake. Kwa mfano ile maneno ya ku-appoint anasema amemchagua fulani managing director itoke kabisa. Ile maneno ya kusikia kuanzia leo ni fulani anasimamia kampuni fulani hiyo mamlaka iondolewe mara moja ili watu wawe wakifanya kazi wakijisimamia ili Kenya iwe tofauti.

Na pia ardhi zote nchini Kenya, wale watu wana ardhi maelfu ya maeka, elfu 300 na zaidi wapokonywe hayo mashamba mara moja ili kila mtu tajiri awe akiwa na shamba eka 50 na yale mashamba mengine yapewe makanga wote wale wanaotusumbua katika town zetu za Kenya. Wawe wakipelekwa huko mashambani kulima na wapewe hayo maploti.

Pia commissioner wote wale wanaongoza, wasiwe wanateuliwa na Rais. Tuwe sisi wananchi kama ni Kinango constituency tuwe tunachagua commissioners wetu ili kazi ikiharibika, tunang'oa tena tunachagua wengine na wale macommissioners kutoka constituency yetu ndio wanaenda;kama ni National Delegate Conference wanaenda wanajichagua, wenyewe wawe na mwenye kiti ambaye watakuwa answerable na parliament through the Attorney General badala commissioner ama enquiry ama nini kuchaguliwa na Rais. Tena matokeo yao hatujui yanakomea kule vichakani, hatuelewi. Kwa hivyo tunataka sisi wananchi kama ni mkopo ilikuwa ya maskini wa Kinango kama tulichagua ile commission yetu ya Kinango kuchunguza pesa zetu zimetoka Amerikani ama Nairobi, tujue ni huyu ameharibu tumuondoe tuchague mwingine ndio tutakuwa tunajua pesa zetu zinakuliwa wapi. Kwa hivyo mimi nimeonelea hata election (uchaguzi) uwe ukihesabiwa katika station hapa katika Kinango tujue Rais alipata ngapi, vice president alipata ngapi hapa kila station badala ya kusafirishwa. Kule kusafirishwa kunapatikana mwanya ya kuiba.

Kwa hivyo mimi naonelea hospitali zote za private zifungwe zisiendelee kwa sababu wanaua watu wengi sana. familia ambazo zinakuwa hazina pesa, maskini watu wao wanakufa kwa sababu hawawezi kulipa pesa zile zinatakikana kwa hospitali ya private kwa hivyo hospitali za private zote zifungwe tuwe na hospitali za serikali pekee.

Pia education; mambo ya elimu iwe ya bure kutoka secondari, primary mpaka university.. Kwa hivyo education yote iwe free.Attorney General asichaguliwe na Rais awe akichaguliwa na bunge na pia chief justice asichaguliwe na Rais achaguliwe na bunge. Ata governor wa central bank kamwe asichaguliwe na Rais, awe akichaguliwa na bunge, akiharibu kazi, bunge inamng' oa mara moja.

Pia, kitu kingine, mishahara yote ya wafanyakazi katika Kenya iwe inachunguzwa sawa sawa. si wengine wanapata 300,000 wengine wanapata 400,000 wengine wanapata sh. 600. kwa hivyo sheria iweko kwamba awe maid awe nani apewe kiwango fulani ya pesa katika Kenya na pia yule alikuwa akisema mtu akikufa kama ndovu imeua mtu, ile pesa amesema ni kidogo sana life ,lawyers as you know life ya mtu is worth more than a million not 200,000. Mtu akikufa kama ni ndovu imeua mtu, hiyo

family ilipwe 5 million and above.

**Com. Barasa:** Question from Commisisoner?

**Com. Bishop Kariuki**: Sasa ningetaka kukuuliza kazi ya Rais itakuwa ni nini? Umesema appointment ifanywe na bunge, kila kitu kifanywe na bunge. Kwa nini tuwe na Rais?

**Reverend:** Aah, I don't understand the word ceremonial but I say the president must follow what parliament tells him not what he wants. Tena pia Rais ajulikane kwamba ana bibi ama hana.

**Com. Barasa:** Ata mkicheka mcheke tu 1 second halafu tuendelee. Tunataka James Ohala.

**James Ohala:** Maoni yangu nitatoa kwa ufupi.

Majina yangu naitwa James Ohala. Mimi ni mfanyikazi wa hapa. Kwanza nina maoni kwa wizara ya elimu ninaonelea kwamba minister wa elimu awe ni mtu ambaye ana uzoefu na ujuzi kuhusu mambo ya elimu.

Pili, kwa hayo mambo ya elimu mabadiliko katika mfumo wa elimu au taratibu ya mafundisho yasifanywe na wanasiasa. Pia tupate mashauri ya wale professionals kwa mambo ya elimu Tumepata shida mifumo inabadilishwa halafu baadaye inaonekana kwamba haifai.

Tatu, vile wenzangu wamesema elimu ya msingi iwe ya bure lakini elimu haiwezi kuwa ya bure kabisa kabisa maanake wale wanafunzi wanahitaji vitu ili wapate elimu nzuri kwa hivyo kuwe na tax au levy ambayo itasimamia elimu ya bure kwa shule za msingi na hiyo inawezekana.

Upande wa pombe, mimi napendekeza kwamba pombe zote ambazo zinaitwa kwamba zimeharamishwa ziwe legalized. Hizo pombe za kienyeji ni pamoja na urithi wetu wa kitamaduni na hizi pombe ikiwa zitakuwa legalized halafu mtengenezaji wa hizi pombe na mazingira ambazo zinatengenezewa ziwe monitored na hata kuwe kunatolewa licenses. masaa ya kunywa pia yawe controlled. Nafikiri hakutakuwa na shida na pia zitachaangia katika uchumi.

Upande wa administration; nasema hivi kuna watu wanaitwa maheadmen.Hao watu kama serikali inatambua utumishi wao na bado inahitaji utumishi wao walipwe kwa maana wametumiwa miaka mingi sana bila kupewa chochote na ndio sababu ukienda pale kuleta kesi yako mpaka akuitishe kitu maanake atatumia muda wake wote kusuluhisha kesi yako na baadaye pia ana mahitaji;walipwe.

Pili, hawa maministers' wa bunge wasiwe na mamlaka ya kuamua mishahara na allowances zao wenyewe.Hayo mambo yashughulikiwe na tume yoyote ambayo itachaguliwa lakini wasiwe na hayo mamlaka maanake wameyatumia vibaya. Na mwenzangu ameongea kitu kuhusu hawa watoto mnaowaita chokora. Hawa watoto mimi napendekeza kuwe na sheria ya kuwashughulikia haswa kuwatoa mitaani huko mijini kule wako na kuwaweka kwenye camps ambako watakuwa rehabilitated na kila mtoto afuatiliwe kujulikane wazazi wake na wale ambao wazazi wake wako, hao wazazi wafanywe walazimishwe kusimamia maisha ya huyu mtoto maanake wengi wa hawa watoto wazazi wao hata ni watu wenye busara sana.

Na nikimalizia kuhusu uchumi; ninapendekeza kwamba serikali isiongee tu mambo ya kuwa na clear policies za kurekebisha uchumi au kuondoa umaskini lakini waonekae kufanya hivyo. Kwa hivyo waongee lakini pia watende vitendo vya kuonyesha kwamba vinamaliza uchumi. Sio vitendo kama vya kuangushia watu maviosk alafu kusema unaimarisha uchumi. Hapo hapo pia zile viteka uchumi ambavyo vimeanguka kama schemes zirekebishwe na zisimamiwe vilivyo na mtu yeyote ambaye anataka kusimamia akiangusha afutwe kazi asihamishwe kupelekwa kwingine.

**Com. Barasa:** Thank you Mr. Dhala. You talked about a levy to finance free education. Who should be levied. That's one question. The other one is on the rehabilitation of street children. Can you say the parents should be followed to support them? Do you want the re-introduction of Affiliation Act?

Mwalimu ametuambia kwamba tuwe na masomo ya bure kwa primary schools lakini tuwe na levy ambayo italipa hayo masomo. Sasa mimi namuliza nani ataweka pesa kwa hiyo levy. Wajua tunaenda kuandika sheria.Lazima nielewe nini ninaandika na swali lingine ni kwamba umesema hawa watoto wa mitaa hao tunaita vibaya sana kama chokora na hali ni watoto. kama iko watu wanahitaji kuitwa chokora ni parent ya hao watoto si hao wenyewe. Sasa amesema kwamba wazazi wao wafuatiliwe wasaidie hawa watoto. Namuuliza tulikuwa na sheria ambayo ilikuwa inaitwa Affiliation Act zamani ikavunjwa 1969 ambayo ilikuwa inahitaji kwamba mtu akimtia mtoto wa wenyewe mimba alafu apate mtoto. Watafuata yule baba mpaka pia yeye alipe kumtunza huyo mtoto; hiyo sheria ikatolewa sasa namuuliza turudishe ile sheria?

**Mr. Ohala:** Kwanza ni kwa ile levy.Hiyo nikitoa kwa mfano tumekuwa na levy moja ambayo ilikuwa inaitwa 'local authority tax'. Levy hiyo imechukuliwa kwa muda mrefu sana na wengi hatukuona vile pesa zile zlikuwa zinasaidia local authority. Levy kama hiyo kama ingebadilishwa iitwe education levy, tayari ingeleta pesa za kusaidia kununua vitabu na vifaa vingine ambavyo vinalitajika kusomesha hawa watoto.

Street children: kile naonelea ni kwamba ukiangalia kwa sasa kuna mashirika ambayo yanajaribu kurehabilitate hawa watoto kuwatoa mitihani lakini pia haya mashirika hayapati kuungua mkono na serikali.

**Com. Barasa:** Turudishe ile sheria?

**Mr. Ohala:** Si haswa irudishwe lakini kuwe na 'camps' ambazo ziko 'sponsored' na serikali, wawekwe huko wakifundishwa na kulindwa huko, kuna wale wenye bahati ya wazazi wao kupatikana na kurudishwa kwa wazazi hawa.

**Alice Atalala:** Maoni yangu inaenda upande wa wafanyikazi na shida kubwa leo, nilikuwa nataka katiba iangalie wafanyikazi ni upande wa kuongezwa mishahara. Kila mfanyikazi aangaliwe kihaki kutoka kwa yule mdogo, 'subordinate' mpaka kwa yule mkubwa 'PSC' kwa vile bila yule mdogo, yule mkubwa kazi yake haitakuwa. Lakini serikali wakati inapata pesa kidogo, wale wakubwa ndio wanajiangalia pekee yao. Kama ni kidogo, kila mmoja apate kile kidogo na kama ni kingi tupate vivyo hivyo. Hilo ndilo lilikuwa wazo langu kubwa.

La pili, kumekuwa na kitu kama 'retrenchment'. Wakati mwingine watu wanaandikwa kama Permanent na baada ya muda mtu anakuja anachukuliwa, kazi imeisha. Huyu mtu hakupewa 'notice' ya kujitayarisha. Labda hajajenga nyumba, mwingine ni kijana mdogo ameoa saa hizi, anaambiwa kazi imeisha. Kazi inaisha anasema wanataka wale wafutwe ili uchumi utengenezwe. Uchumi utatengenezwa vipi kama mmoja wetu amekosa kazi? Atasomeshaje wale watoto wake? Kwa hivyo pale sio kutengeneza uchumi. Kama mtu ameandikwa 'permanent' iwe hivyo mpaka vile atakuja 'ku-retire' na kama ni kufutwa, waangalie ni mtu gani anatakiwa aende.Unapata mtu ametolewa mbali kwa mfano Kisumu anapitishwa Mombasa mwishowe anapelekwa mpaka Lamu ama analetwa kama hapa Kinango halafu anapelekwa Nyango. Kule kufika hapa Kinango mpaka uchukue siku mbili; hakuna 'means of transport' huyu mtu mmetoa mbali tayari na huu umbali pamoja na mashida mengine, amepelekwe ndani zaidi ambapo hata maisha ya kule hajayazoea. Ndio pale nasema kama mtu kweli ametoka mbali, awekwe pahali ambapo unaweza 'adopt' na yale maisha. Wale wenyewe wawekwe katika maisha aliyoyazoea. Ni hayo tu.

**Com. Barasa:** Juko Mwarizo.

**Juko Mwarizo:**
(kiduruma translated into kiswahili by interpretor)
Mimi ni mkulima .hakuna mfanyikazi katika ofisi zetu za serikali. Kuna wale wakristo, siku ya jumapili utawakuta kanisani lakini siku za wiki hutawakuta kanisani. Kiimila chake yeye ni yule anayeabudu mizimwi na ikifika siku zake za mizimwi, mkristo anafika pale pahali na anaomba amefunga macho, yeye mwenyewe siku hiyo hakulima anaenda kuomba, mwenyewe akiomba mvua, mvua hawezi kupata kwa kuwa mkristo ameenda pale kuomba. Kwa hivyo anasema yeye siku ya ijumaa, kwake ihalalishwe iwe ni siku ya kupumzika, isifanywe kazi.

Mkristo jumapili haendi kazini kulingana na mila zake, mwislamu haendi kazini siku ya ijumaa anaenda kuomba, je mimi ambaye ni mwenyeji natumia mila zangu, nataka siku ya juma ihalalishwe hapa na katiba iwe ni siku ya kupumzika pia, nikataabikie mizimwi wangu.

**Com. Barasa:** Asante sana mzee. Gome Magongo.

**Gome Magongo:** Nyumbani ni Bango, Kinango divisiion. Langu la kwanza kuhusu mila, mila kikwetu ndiyo ambayo inatuweka mpaka sisi wenyewe tunajua tunaishi namna gani. Kwanza tunaona tunashukuru tulipata shirika lingine kuja kutusaidia kuhusu mila yetu jina lake 'museums'. Sasa katika shirika hilo watu wengi kama hawa wa dini ya wakristo wanadharau na hiyo ni mila. Waswahili walisema 'mwacha mila ni mtumwa'. Leo hii unakuta mahali mna kidimbwi cha maji. Ile maji imekaa pale karibu miaka ishirini. Unaona yule mkristo anaenda kulima pale karibu, karibu anafunika kile kidimbwi. Ndio inatufanya sisi tunakosa mvua kila wakati. Kuna sehemu kama mizuka ile ambayo tukienda huko wakati wa matatizo ama magonjwa, tunaenda tunaomba ugonjwa huu upitie sehemu mbali mbali isifike hapa kwetu na hiyo inakuwa namna hiyo. Lakini Wakristo wanaenda kukemea ile pepo, wanatoa pale ile mizimwi ambayo sisi inatusaidia.

Tungeliomba katiba hii inyokuja, jambo la kwanza lisisitize kuhusu mambo ya jumaa. Kama yule mkristo jumapili haendi kazi, sisi nasi tuna siku moja ya kupumua kama siku ya jumaa. Ukipatikana kwa shamba unalima jumaa, yule ameasi sheria anafine ya ng'onzi yaani kondoo na kuku mweusi. Sasa hiyo imekataliwa na wakristo wanasema haturudi nyuma, tunaenda mbele na bali yeye ni mzaliwa wa hapa, asili yake ni mduruma kama mimi. Leo anaiga mambo ya kigeni, anaacha ile mila yake na yeye ukimchunguza zaidi utamkuta ana chanjo kwa mwili wake kwa maana alikuwa kwa hiyo mila.

Pili, tungeliomba mambo ya hospitalini. Tunalipa kodi hospitalini, kule kwa damu unambiwa shilingi kumi. Kwa mfano kama umeumia, unaambiwa hutibiwi mpaka utoe pesa. Hiyo pesa unalipa na dawa hupati, unalipa karibu shilingi mia sita na utaambiwa uende tena ununue dawa. Sasa pesa ninayolipa mimi inaenda wapi? Hiyo pesa nitatoa wapi mara mbili? Tungeliomba sheria hiyo itolewe. Hospitali iwe ya bure.

Mwisho, ni shule tunatatizika kwa sababu ya watoto hawa wetu. Unaambiwa na serikali lazima mtoto asome, mtoto anasoma mpaka darasa la nane, anafanya mtihani wake vizuru anapita lakini baada ya kuptia, unaambiwa hakuna nafasi kwa shule ya sekondari. Tungeomba kwamba kule ametoka, ametoka na mzigo mkubwa kwa maana hakuna karo, mambo ya 'bursary'. Tungeliomba pia shule iwe ya bure. Zamani mtoto akipita tuseme 'form four' serikali inamchukua na kumsomesha mpaka amalize. Leo hiyo sheria imeondolewa. Ningeliomba katiba iangalie kuwa sheria hiyo imerudishwa, mtoto asome university mpaka amalize.

**Com. Barasa:** Asante sana. Itsika Ngala na mwingine Nenza B. awe tayari.

**Itsika Ngala:** Mimi nilikuwa na katiba yangu nilikuwa nataka kuitengeneza lakini kiswahili changu si kizuri kwa hivyo mtanisaidia. Changu ni kusema katika hii 'County Council' ninaona kwamba haifanyi kazi ,inakaa kungojea pesa na ndio serikali inasema hakuna pesa. Mimi ningependelea hii county council iondolewe iwe manispaa.

Jambo la pili, tunapata taabu kuambiwa kuwa Moi anasema shule ziwe za bure lakini maafisa wanakuja wanasema tupeeni pesa

zetu. Sijui ile bure iliyotajwa na Moi ni nini? Na ile inayotuambia tupe pesa zetu ni ipi? Kwa hivyo Moi anasema haki lakini wale wadogo wake wanamdharau sana hawamtambui yeye ni nani? Wao wana mitindo yao wanayozungumza nyuma baada ya Moi kuzungumza. Wadogo wa Moi wote wafutwe sababu wanazingatia pesa zao wenyewe wapate kushiba, wawe matajiri kwa hivyo naona wafutwe waandikwe wengine wapya. Elimu iwe ya bure.

Lingine ni hospitali, hospitalini tuna taabu. Moi anavyosema sivyo anavyochukuliwa na wale wadogo wake. Wanasema kwamba Moi anatafuta kura lakini hawasemi ukweli, wanasema hapa hapa mdomoni. Kwa hivyo hao wanazingatia pesa. Ukija hospitalini, unaambiwa hakuna dawa lakini ukienda na mlango wa nyuma, utapata dawa. Naonelea hizi hospitali ziwe za bure kama zamani. Wakubwa ambao ni wabunge wanasema hakuna pesa ambazo zinaweza kulipa wafanyikazi lakini ukiangalia mbunge mmoja anachukua mshahara karibu shilingi millioni mbili au nne. Kwa hivyo anamaliza pesa, nataka wawe sawa sawa na wengine. Wabunge wanamdharau Moi kwa hivyo wanaonelea wote watakuwa wanamdharau hata wale wa miaka hamsini.

**Com. Barasa:** Nyenza Baghala atafuatiwa na Caroline.

**Caroline:** Ninafanya kazi na shirika ambalo si la serikali. Nitatoa maoni kuhusu watoto, sisi kama mashirika ambayo si ya serikali tunaoshughulika na haki za watoto, tungependa kuwe na kipengele maalum katika katiba mpya ambacho kinaangalia maslahi ya watoto katika nchi yetu. Nitasoma kwa kizungu.

A distinct recognition of children in the constitution. Wasiwe kama watu wote kama youth ama watu wengine na haswa mtoto ajulikane kuwa mtoto kutoka kuzaliwa kwake hadi 18 years (below 18) ili tukiweza kuwa na shida kama kutiwa mimba mapema na ndoa za mapema tujue haswa nani ni mtoto isifike kortini alafu ukasema na miaka 15 ingine haisemi hivyo. Kuwe na ufafanuzi maalum ya kusema mtoto ni wa miaka 18 ili wazingatiwe haki zao na pia kila mtoto anayezaliwa Kenya awe na haki ya kuwa Mkenya awe amezaliwa na aliye Mkenya ama mama aliye Mkenya kwa sababu amepatikana kuwa mtoto wa Kenya asiwe ameachwa abandoned. Awe na haki ya kuwa na jina, nationality na automatic citizenship kuwa Mkenya.

Nikiangalia pia haki za mtoto kimaisha tunaangalia kama vile nutrition, basic needs kama vyakula, healthcare (mahospitali) tuhakikishe pia watoto wetu wanapata angalau matibabu ambayo kama mtoto wa miaka 5 kurudi chini awe na free medication alafu pia aweze kupata maji masafi na pia kuishi katika mazingira safi na tamaduni ambazo huzingatia haki za watoto kama elimu, kupata matibabu sawa, kujiendeleza kimaisha. Mila zinazowadhulumu watoto wasiendelee kimaisha zafaa kutupiliwa mbali. Tuhifadhi mila zitakazo tusaidia na kutuendeleza katika nchi yetu. Kwa kimasomo, tunasema every child should be entitled to free and compulsory basic education. Yaani elimu ya bure kutoka nursery hadi standard eight na ikifika secondary, kuwe na affordable subsequent education yaani wazazi waweze kulipizwa karo ambazo wanaweza kulipa. Watoto wazingatiwe yaani wawe protected from abuse and exploitative measures.

Culture/mila ambazo huwakataza watoto kuendelea kama vile ndoa za mapema na zinginezo ambazo zinaadhiri masomo yao watoto wasiweze kuendelea, haswa mtoto msichana wasisahaulike hata kama ni urithi mtoto msichana pia ana haki ya kupata urithi kutoka kwa huyo mzazi wake kwa sababu pia yeye alizaliwa kama watoto wengine na pia anastahili kupewa nafasi pia ajiendeleze kimaisha na pia ningependa kusema kuwa kila jambo ambalo linafanywa katika nchi yetu kama ni sheria ambazo zinafanyika ama mambo yoyote kuhusu watoto kama ni kortini mtoto lazima sauti yake pia isikike. Atoe mawazo yake asichukuliwe kuwa ni kama ni kiumbe ambacho kimewekwa tu hapo na hana sauti ama nini. Pia yeye atoe mawazo yake; kama ni kortini awe na mtu msimamizi ili kesi yake isitupiliwe mbali kwa mfano watoto wasichana tunaona vile katika kesi za kunjisiwa unaona polisi tu ndio anachukulia hiyo kesi juu juu hakuna jambo linasikiliwa alafu linatupiliwa tu mbali mbali huyo mtoto anafaa kupewa nafasi ya kuongea na atoe mawazo yake. Ninasisitiza kuwa kama ni budget; pesa ziwe channeled to children issues, kama ni mahospitali ama masomo, rasilimali ya nchi yetu ya Kenya iangalie sana mambo ya watoto ipelekwe kwa miradi kama ya shule, hospitali, maji ili watoto wetu pia wasisahaulike.

**Com. Barasa:** Samson Njera atafuatiwa na Mejuma Idi.

**Samson Njera.:** Mimi ni mkaaji wa Kinango nimezaliwa hapa. Kwa kabila ni mduruma na kwa kazi ni mwalimu. Niko na mambo machache ambayo mtayasikia. Kwanza tunaanzia kule kwa President kwamba katika yale yaliyopitishwa kuhusu mamlaka yaweze kuondolewa na katika hali ya wale wabunge wapewe uwezo wa kuweza kuwasiliana. Mwishowe waweze kukubaliana kabla hawajatangaza. Rais atakuwa pale kama kiongozi ama mwenyekiti on behalf of the MPs kama watakuwa wamekubaliana. Katika village level, katika vijiji mimi ninaona kwamba katika kila kijiji kuna wazee. Katika kijiji fulani kupatikane wazee ambao watakuwa pembe kwa pembe wa pale. Wazee hao watakuwa wakisimamiwa na Chief wa location nzima kwa hivyo katika shida za pale village hawa wazee wanaita yule chief wanakaa wanazungumza hali zozote zile wanakubaliana halafu ndipo yaweze kuendelea hivyo. Kwa wakati huu kuna assistant chief, sisemi wafuatwe lakini katika katiba hii wale assistant chief waende mpaka wapate ile pension yao lakini kila assistant chief atakaye retire aende ili nafasi ichukuliwe na wazee wa kijiji ambao hao wanakaa na yule chief na halafu katika division level, kuwe na district officer ambaye atakuwa na wazee kutoka kila location yeye akuwe mwenye kiti na wale wazee wazungumze kuhusu ki-division.

Makubaliano yote yatakayokuwa ndio hayo yachukuliwe yaende kwa district level katika district level kuwe na wale wazee waliochaguliwa right from division level ambao watafanya kamati ile ya district wao wazungumze wakubaliane ndio jambo iendelee hata kama ni kwa province iwe katika system ili yule mzee mwananchi yule mwenye pale aweze kuhusishwa administratively.

Elimu irudiwe ile ya zamani kwa sababu inamtayarisha mtoto kukomaa kiakili miaka saba, miaka nne, miaka miwili ndipo aende university na hata akifika university atakuwa amekomaa kiakili lakini unapata kuna shida nyingi zinatokea kwa sababu watoto wanaenda ,akili bado zikitoto ndio maana shida hizi zinatokea kwa hivyo ile system ya zamani inafanya mwanafunzi akomee kiakili na baadaye atakuwa responsible kwa hali ya maisha yake.

Katika elimu pia, ikiwa kutakuwa na malipo, kuwe na malipo maalum ya mtoto wa primary ambayo hayo malipo yatakuwa uniform the whole country. If possible katika level ambazo zile shule zipo kama ni provincial level watu wote wawe na malipo maalum kiwango kimoja. Kutoka hayo malipo, itajulikana kama ni kununua vitabu na vitu vinavyohitajika ili kupunguza gharama wazazi wanapata, kuwe na hali itakayosaidia wazazi kwa pamoja kusomesha watoto wao katika hali nzuri. Tayari ninashaka wale macommissioners ambao wamechaguliwa ni nani aliyewachagua? Je, wananchi walihusishwa kila province? Ili waweze kuwakilisha kikamilifu katika ile commission kwa sababu tuna wageni hapa na kuna wageni wanaambiwa kiduruma ama zile lugha za hapa hawaelewwi hatukuhusishwa na tukajua ni nani atakayekuwa kwa commission. Kwa hivyo hawa ni wasomi, wasomi wanafuatia lugha zilizotungwa nje ya hapa kwa hivyo wanafuatia kile kisomo lakini experience ya hapa inakosekana. Hata ile commission iliyochaguliwa sijui kama wananchi waliusishwa vipi. Kwa mfano hapa Kinango, ama Pwani ama Kwale ninaona kule mbele wakati tunatengeneza hizi tume, kila district iwe na mtu anaye experience ya wale watu ili tukija mahali kama hapa tuzungumze mambo ambaye yeye anaelewa ni ya ki vipi wahusishwe. Nikirudi lile jambo la urithi, ni kweli kuna ile ya kuwa watoto wote wako sawa lakini swali ambalo lilikuwa linaendelea ni kwamba msichana ameolewa, anarithi mali ya mwanawake ni sawa. Msichana hiyo aje arithi sawa sawa na ndugu yake wa kiume anarithi tu ile mali ya babake. Na yule msichana anarithi mali ya mumewake tayari hapo kuna ile difference. Msichana arithi mali ya babake ata certain percentage tuseme kama ameolewa 40% na mwanamume 60%.

**Com. Barasa:** Tunamuambia kwamba tume hii ilichaguliwa na wabunge na wabunge wanarepresent watu wa Kenya. Mbunge wa Kinango akiwapo pahali ambapo panafanywa uamuzi si huyu anasikiliza anachukua mawazo ya watu wa Kinango. Maanake kiongozi anayetambuliwa na katiba ya sasa katika constituency ni mbunge na wao ndio walihusika sawa. Mujuma Idi atafuatiwa na George Ngoloko.

**Mejuma Idi:** Mimi ni mwakilishi katika kikundi cha mama. Oni langu la kwanza ni kuhusu watoto mayatima. Kufikia sasa kuna maradhi ya ukimwi na wazazi/watu wengi wameisha kutokana na ukimwi na tuna mayatima wengi kwa hivyo mimi nilikuwa napendelea kwamba kuwekwe hazina ya kusimamia watoto mayatima ambapo kama mtoto amefiwa na wazazi wote wawili awe mtoto hatakosa kwenda shule kwa sababu hana wazazi. Elimu ya mtoto wa kike – naonelea elimu hii iwekwe mbelezaidi yaani wasibaguliwe. Mtoto wa kike na mtoto wa kiume wawe sawa. Sio watoto wasome wote halafu pengine wapite halafu wakati wa kupelekwa shule ya upili achukuliwe mtoto wa kiume, wa kike awachwe – hiyo itakuwa si sawa.

Street children watafutiwe mpango kama ni wawekwe kule camps watafutiwe chakula na pia wapelekwe shule kuliko wawachwe waranderande. Mwenzetu amesema kuwa jambo la malu liwe litaachwa. Mimi sioni haswa liachwe. Kama ni malu si mwanaume pekee yake aende akamshike mwanamke mwingine amle malu hata mimi nikimshika mwanamke mwingine na bwanangu, mwanamke yule pia nitatka nimle malu.

**Com. Barasa:** Wazee mbona mnalalamika sana? hili swala tulisema tatizo la malu halitaisha mpaka tukubaliane ukiolewa,

mambo ya kwenda yameisha. Hakutakuwa na haja ya malu tena lakini mkikubali kuwa mkioa, mkiolewa nikitambulisha tu lakini una ruhusa ya kuenda kutafuta huko, malu lazima itakuweko lazima turekebishe sisi wenyewe, hakuna atakayeturekebishia.

**Mzee George Ngoloko M.:** Nimezaliwa hapa Kinango kama mduruma. Ninatoa maoni yangu kuhusu katiba. Sub-chief na chief zamani walikuwa wakichaguliwa na wazee wenyewe wa kienyeji ikawa sasa katikati ya miaka chini yake taratibu zile zikaondoka ikawa sasa wanachaguliwa na serikali. Kwa hivyo maoni yangu ninaomba katiba irudishe ule mtindo wa zamani, machifu na massubchief wachaguliwe na kura za wenyeji.

Ndovu: zamani tulikuwa tukiona ndovu waawaua watu na 'game' haikuwa bado imesambaa vizuri ilikuwa mtu hapo akiuwawa, na ndobu kulipwa lakini karibuni mtindo kidogo chini yake ikawa hakuna tena mtu kulipwa na ameuwawa na ndovu. Maoni yangu ninataka mtindo ule urudishwe kabisa ambayo akiuwawa na ndobu alipwe vile vile katiba iliyo hapa nanaiambia alipwe vile vile mwenye kuuwawa huuliwa mtu wako.

Majimbo: mimi maoni yangu katika serikali yetu inayekuja ninaiambia katiba kwamba iwe ya majimbo kwa sababu kuweko na rais mkubwa kam waziri Nairobi atakayekuwa nakipata malalamiko kutoka kwa majimbo yale yote. Jimbo la Pwani haswa liwe na uwezo wake kuelekea na majimbo yote yawe na uwezo wake isipokuwa kuwe na mtu mmoja atakayeketi kati kati yao kama Nairobi awe yeye atapokea ripoti zote za majimbo yale.

Kiapo: yaani mila ya kimijikenda. Zamani kiapo kilikuwa kinafanya kazi kabisa lakini sasa serikali yetu tukufu haitaki hata mtu akishikwa na kiapo wakienda kwa machifu ama kwa maD.O. yeye ataambiwa hakuna nafasi ya kupinga lolote ambalo ameshikwa na kiapo yaani, serikali yetu haitaki vile viapo na huu ni utamaduni wa zamani. Napenda sasa ifunguliwe kiapo; mtu akishikwa na kiapo na akienda serikali kizingatiwe kabisa, kupewe ukweli ule ambao uliwekwa kutoka utamaduni wa kiduruma yaani mijikenda.Nifikia hapo sasa imemaliza.

**Com. Barasa:** Hiyo kiapo ilikuwa inachukuliwa kufanya nini? Watu wanachukua kiapo kufanya nini?

**Mzee Ngoloko M.:** Kiapo maana yake ilikuwa watu kama wawili hivi na mmoja unasema wewe ni mchawi na ni mchawi kweli lakini hataki kusema mimi ni mchawi; yeye anasema mimi si mchawi halafu huyu anasingiziwa na msingiziaji wanapelekwa kiaponi, wakifika pale kiaponi, yule aliyekuwa kabisa, koo hawezi na anasema mimi si mchawi mbio mbio halafu serikali haichukui hatua pale.

**Com. Barasa:** Sasa mzee unonelea kwamba vile tumekuwa na hali ya uhalifu wengi sana tukitudisha kiapo, sasa kama ni mwizi, unashika mwizi? Je, mwizi ama mwenye kunajisi, anaweza kushikwa na kiapo? Na unaona tukirudisha hiyo itaweza kutusaidia kisheria?

**Com.:** Mwingine tumesema ni Musili na Rehema Kami.

**Rehema Kami:** Natoka kivurugani. Maoni yangu; serikali yetu itakayokuja baadaye, naomba kuwe na somo maalum ambalo litafundishwa mashuleni na pale ambapo patakuwa na mafundisho, hili somo liwe lipo ili hata unapoamka kutoka usingizini ujue ni sheria gani inayokulinda na inayokusaidia unapotembea barabarani au njiani. Uwe unaweza kulijibu swali lolote linalokulinda njiani. Tusije tukawa kama serikali yetu hata hatuwezi kujua tunyanyaswa kivipi wala hatuwezi kujitetea kwa njia yeyote. Kwa hivyo kila mmoja ambaye atakuwa amefundishwa; ikiwa amefundishwa kwa njia ya shule hata ngumbaru pia kuwe na haya masomo. Kila mmoj awe nayo akilini hata mtoto mdogo anapoamka pale nyumbani akute ile sheria wazazi wake wote wanajua ile sheria itakuwa rahisi yule kujikinga na zile sheria zinazoharibu na zinazomlinda.

Njaa: kuna wakulima wadogo wadogo huku nje; si wale wa mashamba makubwa. Ningeonelea watu kama hawa wawe na wasimamizi ili anapolimaeka yake moja na kile kijembe kidogo. Pia ujuzi wa kuweza kumsaidi ili tuweze kufukuza njaa. Tutakula mahindi ya kutoka nje mpaka lini? Kwa hivyo tungepata na usaidizi huu serikali hii iwe na mtu anayeisimamia haya mashamba madogo madogo ama hawa wadogo wadogo wa mwisho kabis kuwaonyesha jinsi ya kupata chakula, itakuwa na bora na itasaidia.

Mahospitali: naonelea yawe ya bure kwa sababu ya shida tulizonazo haswa upande wa ‘reserve’ kabisa. Tutakuta mama ameamka na mtoto ana homa na anakwambia hiyo homasi kali sana. sitaenda kwa kuwa sina pesa mpaka izidi kabisa kisha aende hospitali mtoto anahitaji pesa. Akitoa pesa mtoto apate shindano, mtoto anakufa kwa sababu ile homa imeanza na kwa kuwa haijamdhuru sana basi sitaenda na pengine ni pneumonia imeingia kwa mapafu mtoto anapewa shindano anakufa kwa kuwa mama hana pesa za kuenda hospitali. Ningeonelea iwe bure.

Mahari: ningeonelea kuwe na sheria maalum itakayosimamia hawa wasichana kupewa haki zao na wazazi wao kwa maana hawa ni watoto kama wengine. Tukisema kuwe ingawanywe sana niyakuwa yule wa kiume hatataka kuoa bibi yake atakuwa na nafasi atakuwa amepewa kwao pia atachangana na nafasi aliyopewa na ya mumewe. Sheria ijayo ningeomba isimamie wasichana kabisa hasa wanawake wapate utetezi kabisa. Tuwe na haki sawa na wale wengine.

Wabunge: ningeonelea hawa wabunge wetu wawe na ofisi kama machifu. Tunapowachagua, serikali ijayo tujue wanaochaguliwa na hawa raia wa reserve na hata maafisi yao ya huku huku ijulikane kuna usimamizi maalum kuwa hatuwezi kuwatafuta. Tunawachagua kisha wanaenda kuishi Nairobi au Mombasa halafu wengi hatuwezi kufika kule Mombasa kwani hatuna tikiti na tuna mahitaji ya kumweleza. Kwa hivyo kuwe na ofisi maalum zitakazo kuwa huku ‘reserve’ ili tuweze kutoa mahitaji yetu.

Kila mtu apewe haku ya kumwomba Mungu wake kama ni siku ya jumapili, mtu aende kanisani na kamani siku ya juma mtu

apumzike kwa kuwa anaombe Mungu wake. Na kama ni siku ya ijumaa, apewe haku yake aombe Mungu wake. Kwa hivyo ningeonelea kila mtu apewe nafasi ya kuomba Mungu wake siku anayoipenda.

**Com. Barasa:** Mtinda Nzikali, Manandu Kinago, Kanini Nyondo, Bashishi Tsuma.

**Kanini Nyondo:** Nataka hospitali iwe ya bure kwa sababu tunateseka. Unaweza kushikwa na ugonjwa, homa ikawa ni ndogo sina pesa na likazidi. Nikienda hospitalini nikilazwa nikafa kwa sababu sina pesa. Nataka hospitali iwe ya bure na shule nayo iwe ya bure kwa sababu mabwana wengine hawana kazi. Ni watu wa mashambani, kulima wanataka wasomeshe watoto wao sasa baba hana pesa. Mtoto akienda shuleni anafukuzwa, itabidi mtoto akae nyumbani kwa sababu hana pesa. Sasa mtoto atazorota na mwisho wake awe chokora kwa sababu hana elimu yoyote. Sisi twataka shule iwe ya bure, hospitali nayo iwe ya bure.

Chifu: sisi tunataka achaguliwe na raia huku nyumbani mara tunatafutiwa chifu ambaye hatufai. Mtu wa kulewa pombe nakuja nyumbani na kutoa maneno yasiyofaa, tunaambiwa huyo ni chifu wenu atakayetawala. Sisi huyo hatumtaki tunataka tumchague wenyewe. Sub chie pia tunataka kumchagua sisi wenyewe vile vile awe akatutawala huyu tuliyempenda mwenyewe. Akifanya makosa, tunamfuta tunachagua mwingine. Na yangu ni hayo machache.

**Bashishi Tsuma:** Nimetoka Puma Location.
Hospitali: nataka iwe ya bure kwa sababu watu wengi wanakufa sana kwa sababu ya pesa. Mtu ataumwa na aende hospitali na hana hata shilingi na labda anatakikana aende Mombasa na kule tikiti ni pesa na kule kunatakikana pesa na hana hata shilingi atakufa pale pale na atachukuliwa arudishwe nyumbani kuzikwa. Huo ni huzuni nataka hiyo iwe ya bure.

Nasisitiza mambo ya shule. Nasema vile kulivyokuwa zamani ingekuwa hivyo tungekuwa na vijana wengi ambao wana akili yakutupinga sisi sana; na hata yule mtoto ambaye babake hana nafasi ndio wanaopita zaidi, apite na baada ya kupita, huko kunatoakikana pesa na mzazi hana hata shilingi. Atarudi nyumbani na elimu zake ambaye angetusaidia lakini sasa atarudi nyumbani kwa sababu ya ukosefu wa pesa. Hiyo tunataka iwe ya bure.

Sisi tunataka majimbo kwa sababu nyumba zetu ziwe karibu karibu. Mambo mengi hapa hatupati barabara na nini. Mambo hawa ni sababu ya kuwa mbali, tunataka majimbo.

**Com. Barasa:** Ahsante sana mzee kwa kusisitiza hayo. Hata kama watu wamesema wewe uko na la kusema ongeza. Sheria imesema kila mtu aseme anavyotaka, bora tusitukanane. Mapenzi Mwaudhi, tutaenda kwa Chuvi K. atafuatiwa na Samuel Karanja.

**Chuvi Kamwenga:** Mimi natoka Puma sub-location. Maoni yangi ni kwamba; chief nataka achaguliwe na sisi wananchi,

sub-chief nataka pia achaguliwe na sisi wananchi. Kuna chairman wa kijiji, yule ndiye mkubwa zaidi kwa sababu neno lolote likitokea katika kijiji mpaka aeleze yeye mwanzo wala asuluhishwe lile jambo mpaka amalize ndio likimshinda litaenda kwa ‘ sub-chief’. Kama halikumshinda atalimaliza yeye, lakini sasa nataka wapate mshahara, walipwe. Wapate chochote hata kama si kikubwa. Kwa sababu wanafanya kazi kubwa hata sub0chief hawezi kufanya kazi inayofanywa na chairman wa kijiji.

Sisi wakulima, kuna mikopo inayotokea ya wakulima wadogo wadogo huku nyumbani; hatupati. Tunataka katiba ijayo itutengenezee hayo mambo ya mikopo tupate na tuzidi kuendelea mbele. Tukipata mkopo kidogo, tutahakikisha kuwa tutaendelea kupamba mashamba yetu. Lakini hatuna nguvu kabisa kabisa huku kwetu. Kwa sababu mikopo ikitokea huko ikija Kwale inaweza kuzama hapo hapo Kwale na haitafika huku. Na wakina mama na vikundi; katiba izidi kuangalia sana wazidi kupatiwa mikopo mikubwa wajiendeleze maishani.

**Sammy Karanja:** Mimi ni mkaaji wa hapa Kinango. Mimi ni mfanyi biashara na pia mhubiri wa kanisa. Kwanza ninapendekeza kwamba iwe na utangulizi wa wazi wa kuonyesha kwamba nchi yetu ni nchi inayoongozwa na maadili na umoja bile kujali rangi wala kabila.

Bunge lisiwe na uwezo wa kurekebisha katiba kuhusiana na vipengele vya nyongeza ya mishahara ya wabunge. Napendekeza ikiwa wabunge wanataka kujadili mambo ya kuongezwa mishahara yao, kuwe na ‘national referendum’ ambayo commission ya constitutional review wanaweza kuita wakilishi kutoka vijijini kuja kupitisha mapendekezo ya wabunge wakati wanataka kuongeza nyongeza ya mishahara yao.

Raia: napendekeza kwamba watoto wote wanaozaliwa nchini Kenya, waweze kupata automatic citizenship. Kusiwe na raia yeyote ambaye anauraia uwili yaani raia wa nchi mbili.

Vyama vya kisiasa ninpendekeza kwamba katiba yetu iruhusu vyama visivyozidi vitatu na kwamba raia wote kwanzia wafungwa na hata wa nchi yeyote, wanaoisi nchi za ng’ambo wawa na haki ya kupiga kura.

Napendekeza kwamba tutakuwa na ‘parliamentary system’ ambayo itakuwa chini ya waziri mkuu ndiye atakuwa kiongozi wa serikali ambaye atatokana na kile chama chenye wabunge wengi pale mbungeni. Rais asiwe mbunge na yeye awe ti ishara ya umoja wa kitaifa. Rais wetu asiwe ‘polygamist’ awe ni mtu mwenye shahada moja ya ‘degree’ ama zaidi. Katiba ipendekeze kwamba wale marais waliyo-retire, ikawaeleza kwa wazi kuhusu ‘welfare’ na usalama wao na mambo ya ‘immunity for prosecution’ napendekeza iwe tu ni kupitia 2/3 of ‘parliament members’ na current sitting parliament waweze kupitisha hiyo ‘ immunity ya president from prosecution. Rais wetu aweze kuchaguliwa na taifa lote kwa jumla na aweze kupata zaidi ya 50% ya kura zilizopigwa. Napendekeza pia maafisa wote wa serikali pamoja na ma-judge waweze kuchaguliwa na PSC na iweze kuwa approved na mbunge. Kuhusu ardhi, napendekeza mikataba yote ya ardhi kuhusiana na familia ya Mazrui hasa kuhusiana na ‘coastal strip’ ikaweza kuwa ‘abolished’ na land ikaweza kuchukuliwa na kuwa chini ya serikali.

Kuhusu local authority, napendekeza kwamba machairman na mamayor wakaweze kuchaguliwa na wananchi wenyewe na isiwe ni wale councillors ambao wako pale 'council' na pia councillors wawe ni watu wenye cheti cha 'form 4' na wakaweze kuhudumia kwa vipindi viwili vya miaka mitatu. Na baada ya hapo wasiwe na uwezo wa kugombea kiti tena. Wafanyi biashara ambao wana biashara zenye mapato zisizozidi shilingi mia mbili basi wasiweze kutozwa kodi.

Mwananchi awe na haki ya usalama bure, afya, elimu bure, haki ya kuwa na jengo ama 'shelter' chakula na kazi.

**Idi Swale:** Mbunge akipoteza nafasi wakati wa 'grass root elections' hii tunayoita mlolongo, akiangushwa asirudi tena mpaka uchaguzi mwingine term ingine 5 years. kwa mfano wako kama watu wawili, akiangushwa angojee asiende chama kingine cha upinzani; abaki pale pale Kanu hata kama ameangushwa until the next general election.

Kabla ya mji kufanywa mji mkuu kama Mombasa na Kisumu kuwe na masharti fulani kwa mfano kuwe na vyuo vikuu, national schools na hata 'infrastructure' kama barabara, maji na mambo mengine yawe yanaambatani na hali ya kuwa mji mkuu.

Armed forces, police iwe contract of about 6 years. mtu akiwa katika kikosi cha polisi akimaliza miaka 6 awe anatoka, ili vijana waweze kuajiriwa. Kusiwe na vijana wanaorandaranda na tunaweza kuwabadilisha katika vikosi kama vile nchi nyingine zinavyofanya. …..

**Idi Swale:** serikali iangalie katika uchumi mambo yafuatayo:-
Iregulate hire purchase.
Insurance premiums
VAT iwe chini, ili wanachi wasijione yakuwa wanakuwa exploited.
Interest rates, hii nafikiri Donde ashaiwakilisha kwa bunge.

Halafu nyingine pia mishahara iwe inaangaliwa mara kwa mara.
Halafu nyingine, tume ya uchaguzi, ikiwa kazi hamtaimaliza by September, mupumzike, tupige kura kwanza, tukimaliza kura turudi tena kwa katiba kwa sababu mnaharakisha mambo halafu ile katiba itakayokuwa itakuwa ni katiba ingine mbaya sana halafu turudi tena. Tena hiyo two thousand and seven tufanye mambo tena ya katiba.

Kwa hivyo ikiwa kazi haitaisha ya katiba mpumzike tupige kura. Tukishapiga kura, turudi tena kwa katiba. Pale tutakapofikia tuendelee tumalize. Nafikiri hapo itakuwa vizuri sana.

Halafu nyingine, mshasema hii ya education should be cheap, I don't know affordable and free.

Nyingine, serikali iangalie mambo ya petroli na bidhaa nyingine zinazoambatana na petroli kama diesel, mafuta taa. Serikali iangalie bei. Wananchi wanagandamizwa sana. wananyonywa sana na kampuni hizi za kigeni za mafuta. Kuna ile nyingine Kobil ilipata faida 100%. Imagine na wananchi lita moja petroli imepanda hatujui, wakati bei imeongezwa inapandisha bei haraka. Bei ikipungua, saa hii kwa mfano bei ilipanda ya crude oil wameongeza kwa shilingi mbili lakini wakati Iraq itaachilia, itauza mafuta bei itapungua bado watakua wako pale pale kwa hivyo serikali icontrol bei ya crude oil na bidhaa zingine zinazotokana na crude oil hapa nchini. Yangu ni hayo tu.

**Com. Barasa:** Shikamoo, Bahati Buku atamfuatia Kassim

**Kassim:** Kwa jumla mimi nashukuru, lakini sikuwa tayari kwa sababu mambo haya niliyapata jana. Kwa hivyo jambo la kwanza nataka kuuliza katiba ni nini? Nisije nikazungumuza kitu inje ya hivyo.

**Com. Barasa:** Sheria za nchi.

**Kassim:** Asante sana. kwa kusema ule ukweli, mimi nitagusia kitu kimoja peke yake ndugu zangu. Mimi nimezaliwa hapa Ngozini na ni hizi shida za hapa katika hii division yetu ninaona . Lakini hili swali ambalo nitauliza hawa wanaohusika ama hawa wanachukua haya maneno ili yapelekwe huko ni kwamba nataka kuuliza. Yani katika hawa watu ambao tunawachagua hapa. Kwa mfano kama mjumbe, Kamsila, hasa mjumbe. Ninajua katika serikali kuna Ministry. Hii ni Ministry gani huko serikalini? Hii Ministry ya mjumbe. Ni Ministry gani huko serikalini?

**Commissioner:** Unataka kujua?

**Kassim:** Basi mimi machache nitamalizia. Ikiwezekana maoni yangu wakati wa katiba hiyo inayokuja Ministry hii iondolewe. Hakuna haja ya kukuchagua, nikija kwako nikikupa shida zangu, wewe mwenyewe binafsi wewe mwenyewe uende ukasaidie. Leo hii kuna pointi nyingine iliyozungumzwa hapa kwamba kuhusu hawa wanyama ndovu, ambayo pengine mtu kama mimi ni mnyonge sana. ukulima wangu kwa kusema ukweli, sina ng'ombe za kulima. Sina uwezo wa kutoa pesa kumpa mwenye trakta. Ni mkono wangu huu peke yake. Leo nimejaribu mahali pangu. Ninatumainia kwamba nitasaidika hapa halafu ndovu aje avuruge kila kitu. Na baada ya hivyo nikienda ama nikitaka kumuona huyu ambaye nimemchagua, nikimweleza shida zangu, kwa kusema ukweli hakuna linalofanyika. Na nina evidence kaabisa nani nazungumza. Hata mkimuliza Kansila wa hapa; nilikwenda naye mpaka Wildlife. Hivi sasa sina minazi, sina migomba ambayo nilikuwa nafikiria naweza kuikata hapa nikasaidika. Safari ingine nikauza hiki angaa nikasaidika. Kwa hivyo tuna shida nyingi.

**Kassim:** Yes

**Commissioner:** Hizo shida zimesikizwa

**Kassim:** Yes

**Commissioner:** Mbunge anayekuwakilisha, akuwasilishie maswala yako.

**Kassim:** That's right.

**Commissioner:** Kwa mfano swala la wanyama. Na kuna mambo fulani tunataka kukusaidia pale. Jee! Kwanza, unataka wanyama, mimea yako ililiwa na ndovu tukulipe pesa ngapi, kwanza?

Halafu pili, ikiwa mjumbe wako hakuwasilishii maswala yako, jee! Unataka tumtoe au unataka tufanye nini? Maanake lazima kuwe na mtu wa kuwakilisha. Lakini kama hafanyi kazi yake vizuri twataka kujua tufanye nini? Una maoni gani wewe ya kufanya?

**Kassim:** Ok. Thank you. Kwa kusema kweli nitakujibu. Tulipoenda safari yetu wildlife. Sisi tulikuwa tumepanga yale yetu tukayaweka hapo. Tuliomba jambo la kwanza; kuwe na ofisi ya wildlife hapa karibu.

**Com. Barasa:** Iko

**Kassim:** Hapa within the division. Na tukaomba hivyo. Iwe hapa ili wakati kukitokea shida kwa wakulima, mili ya wahusika isiwe kazi ngumu ya kupatikana.

**Com. Barasa:** Lingine.

**Kassim:** Jambo jingine; Taratibu hizi za kuwa pengine ikiwa tu ni habari ya kulipwa mipango hiyo wataijua wao kwa sababu tulipofika sisi, tuliambiwa wazi kuwa nyinyi hata mfanye nini hamwezi kulipwa.

**Com. Barasa:** Kwa hivyo nyinyi mlijiashiria kwamba ni lazima mlipwe.

**Kassim:** Sisi tunaomba hivi, ikiwa ni kuharibiwa na kulipwa, kuharibiwa na kulipwa. Hii itakuwa kazi ngumu. Tunaomba wale ndovu wanaofugwa katika wilaya hii wahamishwe, na tunaambiwa kwamba ati ndovu wale wanatusaidia. na tunakuta wanaosaidika ni wachache, wanaoumizwa katika mashambani huko, ndio wengi. Ikiwa kutakuwa na kiwango fulani huko ambacho tutakuwa tukilipwa kwa sababu hawa watu wamekuja katika wilaya yetu, kipangwe na tuwe tutalipwa.

**Com. Barasa:** Sawa. Na huyu mjumbe wako ambaye hapatikani au hakusaidii tufanye nini? Twataka tujue.

**Kassim:** Kuhusu hapa. Kwanza nataka nieleze uwazi. Kuna wengine wamezungumza hapa wenzangu. Na kama nilivyosikia, uzungumze bora tu usikose, usitaje mtu. Nafikiri wakati nikizungumza hapa sikutaja mtu. Lakini kuhusu huyu bwana ambaye tuliemchagua ama wale wale ambao tuliewachagua hasa kile kilele chenyewe, Head of the Nation, nafikiri Rais wetu Moi. Mimi siwezi kusema kwamba yeye ndiye ambaye anayeharibu haya mambo. Kitu ambacho ninasema ni kwamba; jambo la kwanza – ni hawa, mtu kama Kansila, mtu kama mjumbe. Jee! Ikiwa umempa hii ripoti na haipeleki step ingine kwa mjumbe. Jee! Kule kwa rais wetu itafika? Kwa hivyo tunaweza kulaumu huyo rais lakini ikiwa makosa yawe yapo hapa. Mimi nilienda na kansila mwenyewe mpaka wildlife. Tukatoa hii ripoti na, tukamaliza tukaambiwa; "gari hii inaenda Mwele."

**Com.:** Sorry. Naona tume tukikuelewa.

**Kassim:** Alright. Kwa hivyo mimi sina mengi. Yangu ni hayo.

**Com. Barasa:** Asante. Andika jina lako pale. Tatizo la wanyama. Umekuwa ni sugu kabisa. Haya. Tuko na Bahati? Bahati yuko wapi? Bahati Buku atafwatiwa na Abdallah Kutunza.

**Bahati Buku:** Naitwa Bahati Buku kutoka Kinango. Mengi ambayo ningezungumza naona yashazungumzwa tayari. Yangu ni kusisitiza kuhusu upande wa hospitali. Kitambo wakina mama walipokuwa wajawazito ilikuwa hospitali kupimwa ni bure. Saa hii mama hawezi kupelekwa hospitali mimba yake mpaka awe ana pesa. Jee, kama mama hana pesa ile mimba itapimwa? Saa nyingine mama anakuwa na upungufu wa damu na hawezi kwenda hospitali kwa sababu hana pesa, akiletwa hospitali anasikia kufa. Kwa hivyo nilikuwa naomba upande wa akina mama na wagonjwa wote, hilo swala la pesa liwe litaweza kuondolewa. Kwa maombi yangu.

Pili, hospitali yetu imekuwa ndogo wagonjwa kwenye vitanda wanalala wawili wawili hapa na wengine wanalala chini. Kwa hivyo tulikuwa twaomba, swala kama hilo pia liweze laweza kutatuliwa.

Tatu, mortuary yetu ni ndogo, haina friji, maiti wakifa pale huwa wanaoza.

**Com. Barasa:** Zamani tulikuwa na mochari?

**Bahati Buku:** Tulikuwa hatuna lakini kitambo watu walikuwa hawafi sana.

**Com. Barasa:** Sawa.

**Bahati Buki:** Saa hii watu wameongezeka sana.

**Com. Barasa:** Sawa endelea.

**Bahati Buku:** La nne, nilikuwa naomba raisi wetu kuendelee kutuongoza kama vile Hayati Mzee Jomo Kenyatta mpaka akafa mwenyewe. Hilo ndio langu la mwisho.

**Com. Barasa:** Hayo ni maoni yake. Kila mtu ana chozi wake. Abdallah Kutunza atafuatiwa na Mohammed Kassim.

**Abdallah Kutunza:** Mimi kwa jina langu ninaitwa Abdallah Kutunza. Pendekezo langu katika upande wa katiba, ningeomba mwanzo iwekwe serikali ya muda mpaka katiba imalizike. Hii ndilo la kwanza kwa sababu hii katiba ni kitu cha muhimu na ni kitu cha kutegemewa na kila mtu katika hii Kenya nzima. Halafu baada ya hayo, wakati wa uchaguzi ukianza. Wakati wa uchaguzi ukianza, tunataka yale masanduku ambayo yatatumiwa yawe ya vioo sio yale ya kufunika funika yasionekane. Hiyo hiyo ina maana kwamba ni kuzuia ule wizi ambao unaendelea. Unaweza kuona mtu amebeba ile sanduku ukafikiria mle ndani hamna kitu, kumbe kuna vitu vishawekwa ndani tayari. Kwa hivyo naomba katika hiyo katiba itakayotengenezwa, sanduku ziwe za vioo. Na jambo jingine, tukiendelea na upande wa katiba, tunataka serikali iwe ya majimbo. Hiyo ndio serikali tunayoitaka. Katika hii serikali ya majimbo, itatakikana mwananchi wa pale pale katika lile jimbo awe ni rais.

**Com. Barasa:** Endelea.

**Abdallah:** Katika ile serikali ya majimbo, pia kuwe na serikali kuu.

**Com. Barasa:** Endelea.

**Abdallah:** Na katika uongozi wa ile serikali ya majimbo, tunataka katika ule ushuru ambao utapatikana katika lile jimbo 20% (asili mia ishirini) katika kila jimbo, iwe itaenda kwa serikali kuu. Na upande wa usimamizi katika jimbo kwenye maD.C., maD.O., na mapolisi na kila kitu awe mwananchi wa pale pale sio kutoka sehemu nyingine. Na maana ya majimbo sio ati ni kufukuza watu kwenda kutoka hapa kuwa sijui ni bara sijui wapi sio hivyo. Mwananchi mzaliwa wa pale awe ni kabila gani; awe ni mkamba awe ni mduruma, awe ni mjaluo, wote, washikishwe katika hiyo serikali. Na hii serikali ya majimbo, itasaidia kwa sababu kila mmoja katika nchi ile, katika ile jimbo ataonja matunda ya uhuru. Sababu bila hivyo, hakuna mtu – ikiwa serikali ya pamoja wengine bado watabaki maskini mpaka siku ya kufa.

**Com. Barasa:** Maliza.

**Abdallah:** Katika serikali kuu, tungetaka iwe na waziri mkuu. Katika serikali kuu iwe inaongozwa na waziri mkuu. Lakini sio kuwe na raisi wake lakini kwenye serikali kuu, kuwe na waziri mkuu, ambaye atasimamia nchi nzima. Naona sina zaidi ya hiyo.

**Com. Barasa:** Asante sana kwa mawazo yako. Kuna mawazo mengine umeyasema ambayo hatujayasikia tangu tuzunguke Kenya nzima. Kwa hivyo tunakushukuru sana. Mohammed Kassim. Mohammed Kassim ni wewe? Halafu atafuatiwa na Mwaka Tsuma.

**Mohammed Kassim T:** Mwanzo mtanisamehe kwa sababu hali yangu sio nzuri. Ni vile tu nimekuja kwa vile tu nina hamu ya kurekebisha katiba yangu ya Kenya.

**Com. Barasa:** Sema jina lako.

**Mohammed Kassim T:** Kwa hivyo sauti mtakayoipata muwe radhi na hiyo. Mimi kwa jina naitwa Mohammed Kassim Tumbo.

**Com. Barasa:** Tumbo?

**Mohammed Kassim T:** Yaa. Mimi ni mzaliwa wa Moheli location hii ya Kinango tu. Maoni yangu kulingana na serikali inayokuja. Mimi ningependelea wananchi wote wawe wanapata malipo kutoka kwa serikali.

**Com. Barasa:** Welfare?

**Com. Barasa:** Hiyo ni welfare? Welfare?

**Mohammed:** Wawe wanapata malipo.

**Com. Barasa:** Welfare?

**Mohammed:** Yaa. Na nazungumza hivyo kwa sababu, ukiangalia Kenya ilipata uhuru na inasemekana kila mtu awe huru. Na kila mtu aliumia kupigania lakini ukiangalia wanaofaidika ni wachache na wengine bado wanaona zile hali za zamani bado zaendelea ila tu kuna siri moja tu ambao unadanganywa danganywa lakini shida ni zile zile. Kwa hivyo ukiangalia upande mwingine pia mwananchi wa kawaida ambaye hana kazi, kuna ile kitu inaitwa VAT. Pia yule naye anakatiwa. Ukinunua kitu unaona kwamba kile kitu, kuna kitu kinakatwa pale ndani na wewe kazi huna. Sasa wewe unafananishwa maisha yako pamoja na ule mtu ambaye yeye anafanya kazi. Sasa unakuta kwa hali kama hii inaleta masikitisho, afadhali ule mwananchi wa kawaida ambaye hana kazi yuko nyumbani, naye kuna kiwango fulani cha kuwa anaweza kuridhika akafurahia yale matunda ya uhuru hata kama ni elfu mbili (2,000/-) kwa mwezi. Lakini naye angalau asikie kwamba kama ameenda hospitali na hana kitu cha kulipa, aseme mwisho wa mwezi nitaleta maanake anajua kuna kitu kidogo kwa serikali atakachopatiwa. Kwa hivyo sasa

unaona hawezi kuendeleza maisha yake maanake hana kile anachokitegemea.

**Com. Barasa:** Lingine.

**Mohammed:** La pili nitazungumzia kuhusu uongozi wa hawa wabunge wetu. Ningependelea katika serikali inayokuja, hawa wabunge tunawachagua wenyewe kweli lakini kwa vile wanalipwa na serikali na ile pesa wanayolipwa ni pesa ambayo ni pesa yetu sisi wananchi. Ningependa kuwe na mpango fulani ama kuwe na kamati fulani ambayo inachunguza, hawa wabunge wanasaidia wananchi kweli au la. Kwa sababu ukiangalia ile pesa wanalipwa hawa wabunge ni pesa nyingi sana ambayo wanalipwa kwa sababu wasaidie wananchi. Lakini sasa utakuta hii miaka mitano yote amechaguliwa na huu mshahara analipwa, ukijaribu kucalculate ile pesa ametumia, ni pesa ambayo hata haifiki hata milioni mbili (2,000,000/-) kwa wale wananchi. Sasa ni kama ambaye ameenda pale kujitafutia hazina yake mwenyewe. Kwa hivyo kuwe na hali ya kuchunguza hawa watu. Je wamechaguliwa na wananchi lakini pia serikali iwe na mpango wa kuangalia wamsaidia kweli huyu mwananchi ama ni vipi ili wakirudi kule waweze kuhojiwa mambo kama yale.

Lingine la tatu, nitazungumzia kuhusu elimu. Naona hii elimu, ni kitu muhimu sana kwa mwananchi. Na ndio kitu ambayo inaondoa umaskini kabisa. Lakini nikiangalia katika serikali yetu hii. Ni kama ambayo inasisitiza watu wasome lakini pia haina imani ya kuwa kila mwananchi apate elimu kwa sababu utakuta katika sehemu zingine wengine elimu wanapata wengine wanakosa. Na sio eti kwa kuwa wanapata ni kwa sababu ni matajiri. Ni wanapata kwa sababu kuna watu wao fulani ambao ni viongozi katika serikali ndio maana ile misaada inayokuja kwa community development, zinaenda kule kwao. Kwa hivyo mimi nilikuwa naomba katika serikali inayokuja, serikali iwe na mpango kuwa kila mwananchi ambaye hana uwezo wa kufundisha mtoto wake kuwe ma mpango ambao anaweza kusaidiwa hata kama ni deni watakujalipa baadaye lakini hii hali ya kutokuwa na elimu katika hii nchi iondolewe kila mmoja awe anajua. Lakini sasa ukiangalia tumepata uhuru muda mrefu na bado hali ni ile ile. Ukiangalia kama Duruma yetu hii kuna wengine bado wanadanganywa paka leo.

Hata unakuta pia mtu anaambiwa; nichague mimi kuwa raisi, unasema ni wewe maanake tayari hajui sheria yoyote. Hajui qualifications za kiongozi ni ziwe vipi. Kwa hivyo hali ya elimu serikali izingatie sana na kuwe na njia ya kila mmoja awe na elimu ili kuwe na urahisi wa watu kufahamu haya mambo.

**Com. Barasa:** Free education for all?

**Mohammed:** Mimi sizungumzi habari ya free education. Hata kama kutakuwa na charge lakini huyu mwananchi apate ile elimu halafu kule mbeleni itaangaliwa hali ya kulipa lile deni pole pole lakini elimu asiikose. Pale muhimu ni ile education ipatikane.

**Com. Barasa:** Sawa.

**Mohammed:** Lingine nitazungumzia kuhusu uchaguzi.  Huu uchaguzi ningependelea katika serikali inayokuja iangalie hali ya uchaguzi uwe wa haki.  Uchaguzi uwe wa haki mahali popote kwa mtu yeyote anayesimama awe huru asiwe na ile hali ya kuwa anasimama ajaribu kutetea mwananchi mwenzake kwa sababu ameona ana ule uwezo wa kutetea mwananchi mwenzake.  Lakini sasa pindi anapojulikana kwamba yeye ana ule uwezo wa kuja kusaidia, yeye ndiye halafu tena anaangaliwa kwa upande mwingine anaharibiwe zile hali mpaka unakuta yeye ndiye anakuja hafai.  Kwa mwananchi wakati wa uchaguzi atakuwa na uhuru wa kupigania, kutetea mwananchi mwenzake.  Uchaguzi uwe huru, na uwe wa haki na uwe wa wazi.  Kuongezea hapo ni kwamba katika hivi vituo tunavyopiga hizi kura.  Kila kura zinatakapopigwa katika kituo, mimi ningependekeza katika serikali inayokuja zile kura zihesabiwe pale pale.  Katika kile kituo ambacho watu watapigia kura zile kura zihesabiwe pale pale.  Yani kuwe na ule uwazi wa kuhesabu zile kura ili ule mwananchi ambaye amepiga kura pale kituoni jue kura zake katika ule mtu ambaye amemchagua ni kura gani.  Kulikokuwa kuna ile hali yakuwa baadaye kura zikipigwa zikienda inatokea kwamba baadaye kuna hali imefanyika pale ambayo ule mwananchi wa kawaida hataridhika maanake anajua mtu wangu amepita lakini atasikia ule mtu wake ameanguka na ni kwa sababu zimehesabiwa kulw mbele na haijulikani ni system gani ambayo imetumika.  Kwa hivyo kura zihesabiwe katika lile lile polling station.  Kwa hivyo mimi kwa hayo machache kwa kuwa hali yangu si nzuri, nilikuwa na mengi lakini kwa hayo nitasema ahsanteni.

**Commissioner:** Twashukuru sana, ingawaje tunasikitika u mgonjwa.  Sijui kaa umeshakwenda hospitali au mpaka pesa.

**Mohammed:** Bado.

**Commissioner:** Haya, Mwaka Tsuma halafu Alfred Ngome.

**Mwaka Tsuma:** Kwa jina naitwa Mwaka Tsuma kutoka Mazola.  Kwa hivyo nimekuja kuzungumza hapa kitu ambacho kinaniumiza pia.  Kwa sababu mnasema umasikini tuliondoe lakini tutauondoa vipi.  Kama nimefundisha watoto na watoto wako nyumbani.  Na hakuna kazi yoyote ambayo watoto wanafanya.  Umasikini ule nitauondoa vipi mimi.  Na katika hapa nimekuja kumwelezea, kusema sisi tuko hapa tulikotoka tulikuwa tuko mashakani.  Tulikuwa nao wakubwa lakini tulikuwa tuna shida kubwa.  Tulikuwa tunapelekwa kama feli.  Maana feli ikitegwa waende huko na hujui kusoma.  Katika dakika hii ninapozungumza hapa, nimesikia kusiwe na wabunge wowote wale.  Mawaziri wowote wasiweko tuwakilishe sisi wenyewe kwa sababu kubwa hatufanyiwi.  Tutafanyiwa vipi wanadamu hata tukubali.  Kwa hivi ninavyozungumza hapa tuna hospitali katika nyumbani na wakubwa tulikuwa nao nyuma.  Wakubwa tulikuwa nao na hatukupata hospitali.  Lakini ninvyozungumza hapa hospitali ninayo nyumbani.  Ulikuwa uwepo wa kusaidia sisi wengi sana na hatukuwaona hao.  Lakini dakika hii ninapozungumza hapa nimeona songeza kwa nyumba yangu.

**Commissioner:** Hayo unayosema unataka hali iwe nzuri?

**Mwaka Tsuma:** Hee nataka hali iwe nzuri na watu wanaosema yani katiba tusiwe na mkubwa yeyote, mimi nimekataa.

**Com. Barasa:** Lakini wabunge wawepo.

**Mwaka Tsuma:** Wabunge wawepo kwa sababu tumesaidiwa vyengi vyo kutosha.

**Com. Barasa:** Lingine, tena.

**Mwaka Tsuma:** Nimesaidiwa vya kutosha. Kwa sababu hii naomba, mbunge popote alipo yeyote ule akisimama ni mbunge wangu. Lakini anizingatie vile tunavyoendelea. Mpango uwe ule ule usivunjike wala asivunjike moyo kwa sababu hivi sasa tumeanika pia sisi.

**Com. Barasa:** Mama tunataka kuangalia usaidizi.

**Mwaka Tsuma:** Tuangalie kusaidiwa sisi. Nataka tuangalie tusaidia kondoo maskini wa hapa duruma kwa sababu watoto wengi wamesoma lakini hakuna mtoto ambaye yuko kazini dakika hii.

**Com. Barasa:** Haya huyo alikuwa ni Mwaka. Sasa tuko Alfred Nyome. Afuatiwa na Tsuma mwingine. Tsuma Mwangongo.

**Alfred Ngome:** Ahsanteni. Majina yangu ni Alfred Ngome nikiwa Mduruma kutoka hapa eneo la Kinango. Oni langu la kwanza; ningeomba katika katiba hii ambayo inatengenezwa sasa, iondoe kile kipengele kinachosema kwamba rais awe juu ya sheria. Kila mmoja awe sawa sawa, ile sheria iwe inalinda kila mmoja kusiwe na mwingine ambaye amepita hiyo sheria. Pili, pia ningetaka hiyo katiba ambayo itatengenezwa, ule uwezo wa raisi, kama kutakuwa na raisi, upunguzwe. Yale mamlaka yapunguzwe kwa sababu inaonekana amerundikwa mamlaka mengi kwa hivyo naomba yapunguzwe.

Tatu, hiyo katiba ambayo itatengenezwa, ile ya mwanzo ilikuwa kama ambayo ni siri. Watu wengi walikuwa wanajua katiba, anashikwa kwa ametenda kosa na hajui katiba ni nini? Hii sasa maombi yangu ni kwamba nataka iwe ikipatikani kiurahisi hata kama ni dukani mwananchi aiweze kuiona ili ajue ni kitu gani kinanilinda, nikienda hivi nitakuwa nimeenda makosa. Isiwe siri ya watu wachache na wengine wawe hawaijui. Kwa hivyo nataka iwe inapakana kwa urahisi hata kama ni kuuza kwenye kiosks iwe ni hivyo.

Nne, katika hali ya kugawanya rasilimali zigawanywe kulingana na mahitaji ya pale mahali vile yalivyo. Kwa mfano huku Kwale, hatuwezi kulinganishwa na watu ambao pengine kama Nairobi. Kwa hivyo mahitaji ya Nairobi na mahitaji ya Kwale na ukiangalia zile sehemu vile zilivyo yagawanywe kulingana na yale mahitaji ya wale wenyeji wa pale, si kugawanywa sawa sawa.

Tano, na ni ya mwisho naomba hiyo katiba ambayo itakuja iwe hivi.  Mambo ya ardhi, kusiwe na mipangilio mingine ya kwamba kuna mtu fulani anaweza akawa yeye anaweza kumiliki ardhi kuliko mwingine.  Ardhi ya mahali ambapo wenyewe amezaliwa hapo yeye awe ana uhuru wa kumiliki ile ardhi kusiwe na mtu mwingine ambaye ana mamlaka zaidi.  Kwa sababu kuna sheria nyingine nilisikia mahali ya kwamba unaweza kuwa kuna ardhi fulani mahali fulani hata kuwe ni kwako; lakini raisi akisema mahali hapa napataka yeye anachukua, kwa hivyo nataka kipengele hicho kiondoke.  Mwisho ni mambo ya serikali za wilaya, ningeomba yapewa mamlaka zaidi ili wapate kujimudu.  Mara nyingi wakazi wale wanaofanya na County council ama Manispaa unasikia kwamba wanamaliza karibu miezi sita na hawalipwi na si kwamba pesa hakuna, miezi sita na hawalipwi na si kwamba pesa hakuna, pesa ziko lakini hizi pesa zikikusanywa, zinapelekwa kwa hazina kuu halafu ndio waangalie zitafanywa nini.  Kwa hivyo ninaomba katiba hii, serikali za wilaya zipewe mamlaka kuwa zijisimamie zenyewe.  Kwa hayo machache ahsanteni.

**Com. Barasa:**  Umesema. Ninaelewa kizungu.  Anyone.  Sema umesema hiyo uwezo wa serikali kuchukua ardhi.  Hiyo compulsory acquisition of land itolewe.  Itolewe.  Na kama serikali inaona kwamba hawa watu.  Village yako inaitwa nini?

**Alfred Ngome:** Village?

**Com. :** Eh. Yako.

**Alfred Ngome:** Mazoeni.

**Com. Barasa:** Kama serikali inataka kuweka shule hapo au hospitali, tutafanya namna gani?

**Alfred Ngome:**Ifanywe na Concil kuhusisha wale wenyeji ambao wako pale.  Si kuwa yeye pengine ataka asema nendeni mkafanye hivi wat waka….. endeni tunataka ahusishe wale ambao wako pale.

**Com.  Barasa:** Si anakutoa halafu anakulipa pesa.  Serikali inakulipa pesa halafu inajenga hospitali?  Kutakuwa na ubaya gani hapo?

**Alfred Ngome:** Itakuwa kwa sababu ikiwa nitapelekwa mahali kwingine na nisiwe na mahali pa kutosha kama mwituni pa kukaa.

**Com.  Barasa:** Na hospitali tukose?

**Alfred Ngome:** Ndio nimesema hata kama itakuwa dhifa.  Lakini wenyeji wahusishwe.

**Com. Barasa:** Sawa. Haya asante sana. nenda ukaandikishe jina lake pale. Tutampata Tsuma Mwangongo halafu Duka Mangale awe tayari.

**Tsuma Mwangongo:** Ahsanteni sana. Kwa jina naitwa Tsuma Mwangongo. Na katika maoni yangu ambayo twaonelea leo. Kulingana na ile katiba ambayo itafuata ni serikali iwe ya majimbo. Kwa sababu, utakuta sasa ofisi inakuwa moja ambayo mikoa yote inatoa maoni kupeleka huko. Sasa kutimiza ile hali inachukia karibu muda wa miaka ishirini katika sehemu hii ya Kinango au sehemu nyingine yatenda. Na uongozi zaidi unalenga ule mwananchi wa kawaida. Sasa utakuta mwananchi wa kawaida anaendelea kuteseka miaka na miaka hali kwamba ni pile zimepangwa hapa kwa barabara pengine ya Kinango ama sehemu ile nyingine ile percent itatiwa lami ama kufanyiwa marekebisho fulani haiwi hiyo kwa sababu ya ule mzigo mkubwa. Nafikiri ikiwa majimbo kama Pwani ama sehemu ile nyingine, sasa itakuwa kama kila jimbo linakaa nafikiri mwananchi atakuwa anaweza kupata huduma karibu. Hilo la kwanza hilo. Katika serikali ile inafuata, kuhusu hawa watumishi wa uma. Hasa raisi zaidi huwa anatetea uhai wa mwanadamu. Tusema ni uhai wa mwanadamu. Lakini utakutwa sasa jambo fulani na upelekwa kwa maafisa wa uwezo zaidi hata yule afisa naye anamchukulia mtu mwingine mdogo kusingiziwa jambo fulani anawezapigwa hata kufa katika dakika chache kwa sababu amesingiziwa jambo na hajafanya lile jambo.

**Com. Barasa:** Ni polisi au.

**Tsuma Mwangongo:** Polisi, maafisa wa polisi tuseme. Kwa ile sheria ile iangaliwe sana kwa sababu mwanadamu tuseme uhuru. Mtu akitolewa kule kama amesingiziwa na jambo, atoke pale ajitetee mwenyewe akipatikana na hatia jaji ndio ata amua hukumu itampata huko huko kotini lakini sio aanze kupigwa kwanza, kuteswa, pengine hata hajafika kule amekufa. Hiyo nafikiri iangaliwe sana. Na mambo mengine ni kuhusu hii elimu. Elimu tuna miaka karibu thelathini na tisa ama karibu arobaini hivi na kuna wengine hata hawajajua shule ni nini. Na sio kwamba hataki kusoma, ni sababu ya mzigo ambao umemlea mzazi. Na hakuna sheria yoyote katika kipengele cha katiba ambacho kinamwangalia yule mtu ambaye yuko katika hali mbaya tena zaidi akachukuliwa kuwa muhimu. Ni kwamba tu, pelekeni watoto shule lakini hakuna ambaye pengine. Kutakuwa na msisitizo zaidi. Yule ambaye yuko hali mbaya na pengine hana mtoto wake anafaulu zaidi. Kwa hivyo serikali hii ya ambayo hakuja iangalie haki ya mwananchi ana kity hana kity lakini awe atasoma. Nafikiri kufikia hapo ni hapo. Kwa hayo machache nasema ahsanteni.

**Com. Barasa:** Free education? Free?

**Tsuma Mwangongo:** Yaa

**Com. Barasa:** Ahsante sana bwana Mwangongo. Duka. Mangle? Pendale. Oh! Ya. Haya David Chiti, atafuatiwa na Tsuma Nyasi.

**David Chiti:** Ahsante. Mimi kwa majina nikama mlivyosema David Chiti. Na nitazungumza tu labda mambo mawili kuhusu katiba. Kwanza mimi nilikuwa na maoni kuhusu katiba. Na maoni yangu yanasema katika katiba, mimi ningependelea iwe ya majimbo. Na shida ya kuwa ya majimbo ni kwamba tupate kuwa na huduma wa karibu. Kwa sababu tumeona kwamba tuko nao kweli wahuduma wetu kama wabunge tunaowatena katika mitaa yetu na hata macouncil lakini haya yote ni maneno ya kuyangojea yakienda mbali. Lakini tukiwa na majimbo, tunaamini ya kuwa tutakuwa na mtu karibu ambapo hata wale wahuduma wetu wa vijijini watakuwa ni rahisi kufika sehemu zile na kutoa maoni ya wananchi. Hivyo pia, nasema kuwe na hiyo serikali kubwa ambayo ikiongozwa na mtu mmoja ambaye pia yeye atakuwa ana nafasi yake kwa hawa wengine ambo watakuwa wanatuongoza katika majimbo. Kwa hivyo mimi nilikuwa naona ya kwamba, tunapokuwa na raisi mmoja kisha halafu baadaye tuwe na hawa wa majimbo itakuwa kila neno linawasilika vizuri. Sababu ya kusema hivyo ni kwamba, tukiwa katika nchi yetu hii ya sehemu hizi za Kwale, tuko na mambo mengi sana ambayo ni kama hatuoni kama tunaendelea. Kwa sababu tukiwa huku tuna shida hasa za huduma mbili. Kama elimu na afya kwa sababu mambo ya afya hapa tunaweza sema tukiwa Kinango.

Ziko hospitali nyingine ndogo ndogo lakini utakuta hasa mimi naongelea juu ya akina mama ambao wana mimba. Mimi mwenyewe nikiwa ningali bado kijana kidogo nimestaajabu ama nimeona mambo mengi ambayo yanatukumba kule vijijini. Kwa sababu mama anashikwa na mimba, kwanza anakosa kwenda kwa daktari kwa sababu ya malipo. Mimba ile haitaonekana, labda mtoto ule hayuko vizuri. Kwa hivyo hata ikifika wakati wa kujifungua unakuta mama ule anashindwa. Kiwango cha kujulikana huyu mama ameshindwa kutoka kule mashambani mpaka hospitali mama amekufa. Kwa pia hivyo mimi ni ombi langu, kama katiba, kama vile mashule tulivyopata kule vijijini. Naona ikiwa hivyo, hatutapata mambo ya maafa. Hivyo hivyo, unakuta ya kwamba kuna hata watoto. Kuna huu ugonjwa unaoitwa pepo punda. Hapa Durumani naweza sema ni mwingi sana. na hata watoto wetu wengi wanaisha kwa sababu hiyo na huduma hii inakosekana kwa sababu hospitali yetu ni Kinango na iko mbali. Kwa hivyo mimi pia naomba katkia hiyo katiba yetu itakapotufikia, itufikiria sana kupa mambo ya afya katika sehemu zote za mashambani.

Na nikirudi upandi wa elimu. Pia elimu nayo iangaliwe vizuri maana nimesikia tangu mwanzoni kwamba, hapa Duruma ama hapa kwetu watoto wengi waliingia shule lakini hawakuweza kumaliza kwa sababu ya malipo. Hata saa hii sasa wengine wanashindwa hata na kumpeleka mtoto Nursery School kwa sababu ya malipo ya shilingi labda shilingi arobaini ama ishirini. Kwa hivyo mimi nilikuwa na ombi, na maombi kupitia katiba yetu hii mpya ambayo tunaitafuta. Ikiwapo ikapate kutuondelea viwango vile vya malipo hasa hizi shule ndogo – mwanzo wa nursery skuli mpaka darasa labda la nane. Ili hata kama ni malipo ianzie pale Form one na kuendelea huko mbele. Nafikiri itakapotufanyia hivyo tutakuwa na msaada hata kama wengine hatutaenda lakini tutakuwa kidogo tunasonga mahali pa kuwa naweza kuzungumza na baba yangu, naweza kuzungumza na mgeni yeyote kwa lugha inayotakikana. Kwa hivyo mimi ni ombi langu hasa. Tutakapomaliza hivyo, naona kila kijiji kitapata elimu na hakuna mmoja ambaye atashindwa na kuendeleza watoto wake. Kwa hayo machache nasema ni ahsante na mzidi kuendelea.

**Com. Barasa:** Tsuma Nyasi.

**Tsuma Nyasi:** Ahsante sana. mimi ni Tsuma Nyasi, kutoka Ichale sublocation Yokato Village. Maoni yangi ni kwamba katika katiba ya sasa, kati ya raisi wetu wa kwanza ambaye alienda Mzee hayati ni Kenyatta tulikuwa na mabadiliko makubwa na sasa tuna raisi wetu huyo. Kwa hivyo sasa tangu hapo kwa raisi wa kwanza mpaka sasa kuna sehemu nyingi zinazoumia watu na maendeleo inapatikana kwa hibyo tunaona majimbo inaweza saidia zaidi kwa sababu tunaona wakati wote ukienda sehemu za Migori ama Ukambani huko, shida zinaendelea. Kwa hivyo hii mfumo wa majimbo si matusi, ni usaidizi na kuokoa katika sehemu nyingi zinaziumia ila raisi atakuwa mmoja peke yake lakini kila jimbo liwe na Governor wake wakuwakilisha malalamishi kwa katibu mkuu wa Kenya nzima. Si kutengana, ikiwa ni mkamba ni mkikuyu yuko Coast, ni mjaluo, ni mmeru mradi yuko Coast na ni Kenya. Lakini majimbo yatasaidia mwananchi pamoja na elimu yatatapaka mpaka mashinani huko, jambo la kwanza.

La pili, kuhusu elimu. Hakuna kiongozi wowote ambaye anafikia uongozi bila kupita kwa mwalimu hata raisi. Na unakuta walimu wanateseka vibaya sana kwa sababu wanaonekana hawa sawa sawa na mzazi wa kike anabeba mtoto mpaka afikia kiwango. Anastahili kuongezewa mshahara huyu mwalimu kwa sababu yeye ndiye nguzo ya ulimwengu mzima. Katika katiba ni maombi yangu.

Ya tatu, kuna mtu anaitwa Village Chairman. Huyo ni mtu mwingine anapata taabu kuliko assistant chief kwa sababu Assistant Chief hungojea matokeo kutoka village chairman apelekewe kuna hivi na hivi. Kwa hivyo yule ni mtu angestahili kupata kitu chochote kutoka kwa serikali. Kwa sababu yeye ni mtumishi wa umma mmoja wapo ambaye ni inakuwa kama tawi cha kuleta maovu na mazuri kupeleka kwa serikali. Kwa hivyo ni jambo moja chairman ambaye ni mtu mwingine ambaye yuko msitari wa mbele hilo ni jambo la tatu.

Jambo la nne, tunaona mambo ya elimu, ni sawa kusema namna hiyo sio ati watu wanasema upande yao, waseme Kenya mzima. Kwa sababu utakuta ni mahali palikosomwa ndio kuna elimu hata ukambani kuna sehemu unapotembea. Kwa hivyo, yale majimbo yatasaidia elimu kwa kila sehemu si Kwale peke yake. Kwa hivyo neno majimbo, tujaribu kuliangalia katika kativa ya sasa. Ni hayo machache na Mungu awabariki.

**Com. Barasa:** Tunamtaka. Tunamtaka Saidi Mwaguni. Saidi Mwaguni? Niko na rafiki yangu anaitwa Saidi Mwaguni kijana. Sasa si…

Kulingana na katiba hii na maoni yangu ninasema mambo mengi imeshaa zungumzwa inachobaki ni kusisitiza. Kwa sababu kwanza naanzia na hospitali. Hospitali yetu hii tunateseka sana kwa sababu watu wengi wanashikwa na magonjwa na wakiingia pale wengine pesa wanazo na wengine pesa hawana na ukiingia pale wanachotaka ni pesa. Kwa hivyo maoni yangu ningetaka katiba hii ikiwezekana hospitali iwe ya bure, haya. Ya pili kuna mabiashara ambayo inafanywa watu wanafanya mabiashara

kujiendeleza na wengi wao pesa hawana tunataka pesa za mkopo tukijaribu zile pesa za mkopo tunajaribu kuomba na alafu hatuoni pesa za kutosha tutazipata namna gani? Kwa hivyo oni langu ninasema pesa za mkopo ikiwa inawezekana tupate nini? Tupate pesa za mkopo tujiendeleze kama watu wengine. Ni ya pili hiyo. Kwa hivyo sina mengi kwa sababu mengi imeshazungumziwa. Yangu ni hayo, ahsante.

**Com. Barasa:** Na mtoto wa kike apate nini?

**Presenter:** Mtoto wa ? mtoto wa kike si asome.

**Com. Barasa:** Humpati kashamba kadogo kwako.

**Presenter:** Apate shamba langu? Yaani mtoto wa kike anaweza kuridhi shamba langu sio. Kwa hivyo ni mtoto wangu anaweza kupata shamba langu.

**Com. Barasa:** Waraka! Waraka afuatiwe na Chengo Mbilu.

**Waraka:** Katika katiba inayotengenezwa sasa ningependekeza kwamba mamlaka ya rais yapunguzwe. Nikisema yapunguzwe ninasema rais awe kama raia yeyote awe anaweza kushtakiwa anapofanya kosa ata kama yeye ni rais aweze kufikishwa mahakamani kama vile Mwahima alifikishwa mahakamani jana. Mwahima alishtakiwa kwa hivyo rais pia aweze kushtakiwa ata kama ni rais. Hapo hapo kwa rais kwa vile tunazingatia uongozi wa vijana. Rais asizidishe miaka sitini na mbunge asizidishe miaka hamsini na tano. Mbunge wa chini kabisa awe na miaka ishirini na tano na kwendelea. Rais miaka thelathini. Hapo hapo kwa rais, rais awe na shada ama degree katika kiwango cha chini cha elimu na mbunge na diwani awe na kidato cha nne. Councillor awe na miaka ishirini na mitano kuendelea mpaka hamsini na tano pale pale.

Tuwe na elimu ya bure kwa shule za msingi hospitali ziwe bure, kwa magonjwa madogo madogo kama vile malaria kama hayo iwe ni bure na malipo kidogo, kwa malipo makubwa kama yale ya upasuaji angalau unaweza kulipa kidogo lakini kwa magonjwa madogo kama malaria iwe ni bure.

Vyama vya upinzani visimamiwe na serikali na visiwe zaidi ya vitano. Na mwisho Kenya ikiwa nchi ambayo inazingatia dini na inapenda watu waombe Mungu sana basi naona waislamu kidogo hapa hawajapata haki yao vizuri. Kwa hivyo nilikuwa naomba katika katiba ijayo Ijumaa isiwe ni siku ya kufanya kazi iwe ni siku kama vile Jumapili ili mtu aombe Mungu wake vilivyo. Kwa hayo machache asanteni.

**Com. Barasa:** Chengo mwenzake Mali Beganda awe tayari.

**Chengo:** Asante sana kwa jina langu naitwa Chengo Mbilu, mimi ni village chairman kutoka Amani. Ningetaka kuambia katiba yangu matatu ambayo yanauchungu na kwanza naingilia kifungu cha watoto, wanaosoma mpaka wanafika class ya nane na baba yake anakosa pesa za kumwendeleza mbele. Hawa vijana wa kike na wakiume wapatiwe kazi ata kama ni za jeshi.

**Com. Barasa:** Wapatiwe pesa waendelee na masomo. Mtu wa standard eight sio mbali. Ungesema kama mzee ameshindwa tushughulikie mtoto naye afike form 4.

**Chengo:** Hiyo pia ni sawa sipingi umenisaidia sana. asante, waendelezwe yani wasinyimwe haki ya mtoto.

Ya tatu, ni sisi. Ni kama mimi sasa ni village chairman ambaye unaona saa hii nimefika hapa nilikua nimetumwa sehemu ya mbali. Ningetaka nije kama saa tatu lakini nimetembea na nikarudia bibi yangu bila ata robo ya sukari. Kwa hivyo katiba hii ya sasa iangalie mzee na kijiji, maana sisi tuna kazi ngumu, unaweza kuwa uko nyumbani kwako usiku pajirani yako pakawa pana shida, ndiyo utoke. Chief hajui, sub- chief hajui, D.O. hajui, mimi najua nasijulikani.

**Com. Barasa:** Nasema ni nyinyi husimamia kijiji kama hiki?

**Chengo:** Tunasimamia. Yaani neno ni kama hili usiombe watu wakosane. Ukiomba watu wakosane si imani, tunawasaidia kupatana.

**Com. Barasa:** Na wewe ni nani anakuchagua kama mzee wa kijiji. Ni nani anasema wewe ndiye mzee wa kijiji, wako wazee wengi huko kwa kijiji.

**Chengo:** Wako.

**Com. Barasa:** Niambie umekua namna gani mzee wa kijiji?

**Chengo:** Wananchi wenyewe wa kijiji kile chako ndiyo wanawezakuchagua.

**Com. Barasa:** Na unakaa maishani ama wanakutoa.

**Chengo:** Unakaa wakichoka na wewe, ukianza kwenda kona kona wanakutupa.
Ya tatu, naona ni ya mwisho. Ya tatu nitaingilia hii sijui kama nimesema nitaingilia County Council. County Council inaumiza wafanyi biashara. Na pesa zao wakikusanya kule wanakofanyia zile biashara zao kama minanda, si kuna yale maboma ya kuweka ngombe yamevunjika vunjika yote. Mtu akileta ngombe wake akiwa ni mkali ataumiza watu maana hana boma. Na ukimuuza saa ile ile pesa unalipa. Hizi pesa, wasiotengeneza hii minanda yao zaenda wapi? Hii Kinango yenyewe hapa town ni

pachafu ile hakuna. Hakuna wafanyi kazi na pesa kila jioni wanaokota kwa akina mama. Leta pesa, leta pesa. Si kwa mnanda, leta pesa. Na ukiangalia hii town ni vikaratasi vitupu. Hakuna wafanyi kazi wa kuokota hii maghasia. Mvua ikinyesha tunaletewa umbu wa ajabu. Hospitali ni hivyo. Ukienda wewe watetemeka unaambiwa nenda kwa bandika ukanunue dawa hii ni shilingi mia tatu, mia nne. Hauna pesa, ukirudi nyumbani waenda kufa. Mimi sina mengi yangu ni hayo.

**Com. Barasa:** Hayo ni mengi sana. Njoo hapa uandike jina lako, maanake ata tukikupatia mshahara wewe, ata City Council ikija ikilete matrakta ata we! tunakazi hapo. Mali Beganda ametoka nje, Mwanje Felix, Jacob Mangale. Kuna wengine, wote hawako. Waraka alikuweko, Chengo, Mali hawako. Who is here let him start. Give us his name.

**Daniel Thuo:** Jina langu ni Daniel Thuo kutoka Kinango. Mimi ni mwalimu. Sasa maoni yangu ni kwamba rais akichaguliwa awe amepata kura nusu ama zaidi. Na kama hakuna mtu anaweza pata 50% wale wawili wa kwanza warudie mpaka mtu apate at least 50% and above. Alafu polisi, polisi wawe trained for a longer period na training yao includes sociology and psychology. Alafu kuwe na another institution ambayo inatakikana iwe ukiangalia performance ya polisi kwamba kama mtu anamalalmishi kuhusu polisi asiende polisi.

**Thuo:** Yes. Alafu appointment za serikali ziwe zikiwa approved na parliament such that the head of state does not have the final word. Na creations of institutions kama district, province, ministries iwe ikipitia bungeni. Hata number of ministries iwe pia inapitia bungeni. The number of ministers and assistant ministers pia iwe approved na parliament.

**Com. Barasa:** How many ministries?

**Thuo:** In Kenya we should have at least fifteen, each with one minister, that is according to my recommendation. Alafu ningependelea constitution ianze kufundishwa shuleni, kwanzia upper primary, secondary na tertiary levels, such that mwananchi ajue haki yake kuhusiana na katiba, isifanywe siri, katiba isiwe siri. Na la mwisho ni kwamba kuwe na another office ambayo itakuwa ikicheck the parliament kwamba parliament isiwe, kama kuna jambo lao wanataka kufanya wawe wanapitisha bungeni. If there is anything that concerns the parliaments welfare it should be checked by another office, kuwe na ofisi ingine pia ya kucheck.

**Com. Barasa:** How?

**Thuo:** Like in this case where the MPs were voting for their own welfare kama masalaries, kama sijui mabanda ile extension, anapitisha inakua hivyo kwa sababu imepitishwa na parliament. Kunatakikana kuwe another body to check on that individualism in the parliament.

**Com. Barasa:** Who do you think should be in that body?

**Thuo:** The committee we should have people who have served in parliament for more than at least three terms to be able to sit in that other upper house.

Na la mwisho ni kwamba the generated wealth within the province most of it should be retained in that province for development. At least 60% should be left within the province for development. Ni hayo tu asanteni.

**Edward Harry:** Kwa majina naitwa Edward Harry kutoka Kinango. Mimi nina mawili tu ambayo nataka kuwajadilia ambayo yamezungumziwa na wenzangu, ya kwanza kabisa ni kuhusu kura. Ni maoni yangu kwamba kila kura zitakapokuwa zimepigwa kila kituo cha kura kinachopigiwa kura zihesabiwe pale pale bila kuzungushwa zungushwa na kupelekwa katika makao makuu ya wilaya.

Pili, ninaongea kidogo kuhusu dini. Nina amini ya kwamba ni kuondoa imani ikiwa mtu atakuwa anasimama, mwenye dini/mhubiri - yeyote awe anahubiri na kukashifu dini ya mtu mwingine. Hiyo ningeomba katiba hii iingize ndani, mtu kama yule ashikwe na kutiwa ndani kwa mahakama. Kwa hayo machache. Asanteni.

**Com Barasa:** Ngoja tumalize hawa. Ni wewe sasa Chiwaya Chuli.

**Chiwaya Chuli:** Jina langu naitwa Chiwaya Chuli kutoka location ya Makindani. Maoni yangu nilikua naomba kwamba wale chief officers wa Councils wawe under the councillors. Chief officers wa County council wawe chini ya councillors kwa sababu division zao huwa wanasema wanauliza kutoka juu. Alafu parties maximum ziwe parties tano na zote ziwe funded by the government. Key position ama crucial position kama chief justice, A.G., Auditor General ziwe vetted by parliament. Mtu yeyote ambaye ana criminal record na alipatikana kuwa guilty asiruhusishwe kusimamia kiti cha udiwani au ubunge ama urais.

Lingine ni duo-citizenship. Yani mtu kama vile watu wengine wanaweza enda kuishi nchi nyingine na passport ya nchi nyingine. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba mtu akitaka kuwa mwananchi wa Kenya ile nyingine iwe itachukuliwa na serikali, abaki na ya Kenya pekee yake. Na wale wanataka kusimamia kiti cha ubunge ama udiwani ama urais ni lazima wawe walizaliwa hapa nchi ya Kenya. Alafu kuwe na siku tofauti, kura isifanywe siku moja. Kuwe na siku ya kupiga kura ya udiwani, siku tofauti ya kura ya ubunge na pamoja na ya urais. Kwa sababu hii hutenganisha sana wananchi. Siku tatu lakini tofauti tofauti, zisichanganywe kura zao.

Rais term zake ziwe mbili za miaka mitano, mitano. Rais na makamu wake asiwe bunge na achaguliwe direct na wananchi. Kuwe na elimu ya lazima na ya bure kutoka nursery hadi form four. Natural resources ya sehemu tofauti tofauti imilikiwe na community ya area hiyo. Defections wakati kama mtu amechaguliwa kuwa diwani ama mbunge asiruhusishwe kubadilisha chama chake mpaka ule muda aliyechaguliwa kuwa katika bunge uishe. Kama ni kufanya defection ni baada ya ule muda kuisha. Katika mbuga la wanyama zile councils ambazo zina mbuga ya wanyama zipate at least 25% ya gate collection na pia

katika zile hoteli ambazo sio katika council kila mgeni yeyote anayelala kwa hoteli ile 25% iende kwa council.

Na mwisho kabisa ni kuhusu structure system ya government. Maoni yangu ni kwamba kuwe na serikali ya majimbo ambapo wenye jimbo lile wafaidi upande wa kazi na kadhalika. kama vile shirika lolote kubwa ama company yoyoye kubwa kama vyeo vya managerial posts ni kama kumi 75% ziendee watu wa jimbo hilo. Kama ni upande wa kazi za chini 80% ziendee watu wa jimbo hilo. Katika upande wa qualifications ya udiwani na ubunge pamoja na urais lazima anayechaguliwa awe ni mtu ambaye hana makosa mengine kama ile ya kiethics ama moral awe ni mtu yuko sawa. Awe ni mtu ambaye ako na family kama hana family asiwe kiongozi. Elimu yake councillor at least awe na 'O' level education. Katika upande wa jumbe na rais at least awe na degree moja yangu ni hayo tu, asanteni.

**Com. Barasa:** Your version of Federal system of government, we have read many, there are many, I do not know which one you are suggesting to use. I see the American model constitution of ferderalism. Where jimbos are independent but even them, American federalism is a classic example of ferderalism. I think the purpose is to bring governance to the people. To bring services to the people but then in America people hire others on qualification so that if you come from the federal state of South Carolina you can get a job in California. You see they go for competence, so I want to understand you. If yours seems to be a little different where other people should not work in the jimbo of Pwani, the jobs should be reserved for the people of Pwani. And then we have other models of federalism, there is the German one is copied by the South African one where provinces are the ones which are empowered and purely for decentralisation of services and for the local people to participate in governance and also for distribution of natural resources. I do not know, let me understand your model of federalism.

**Chiwaya:** Nafikiri lengo langu ni kuhusu kwanza wale wenyewe katika jimbo ile wajitawale alafu shida kubwa ni ile mambo ya natural resources kwa sababu leo hii ndiyo maana utasikia kila pahali utakayokwenda hasa watu wanasema angalia jimbo. Jimbo lao ni kwa sababu tunasema kama Kenya Ports Authority pesa nyingi ya Kenya inatoka pale na mambo ya wildlife pesa nyingi inatoka katika hiyo mashirika mawili ambapo utakuta kwamba katika ile ngazi ya juu, katika central government watu wa Pwani ni kidogo, so kwa hivyo kama wanaplan mambo ya maendeleo huwa, watu wa Pwani wanawachwa kwa sababu hawana watu wa kuwapigania kule mbele zaidi ni uchungu kwetu na ndiyo maana tunasema kwamba natural resources 80% au 75% ibaki hapa ili sasa iendeleze hii province yetu iwe kama sehemu zingine.

**Com. Barasa:** Bwana Chuli supposing we all recognise the fact that it is poor governance which has been responsible for inequitable distribution of resources. I think if a government is good we do not need your brother to be seated there so that you get something. A good governement will know that everybody is entitled. Supposing you remove the bad governance and had a government which says okay, fine 80% of this will go to Coast will that be a problem to you, and really make sure that you get the resources as a Kenyan will that be a problem? Because what I am getting from the Coast is that the high level of neglect, the high level of poverty I think that is what bothers people. Supposing you had a government which took care of the people of Coast of Kwale and gave them their share of the national cake. I just need to understand from them because really

what they are complaining about is the high level of neglect. Really high level of neglect. Isn't it?

**Mali Begonda:** Maoni yangu ya kwanza ni kwa upande wa president. Tuwe na vyama kama viwili, kinacho ongozwa na kile kingine ambacho kinafuatiza tayari. Kama tunasimamisha president tusimamishe president wawili pekee yake ambapo pia tutakua tuna nafasi nzuri ya kuwa ule mwingine tutakua tumempitisha ule wakati ule mwingine pia tukiona hakutufanyia lolote, tunasimamisha mwingine hata kama ni waopposition, naye tumpitishe tuangalie wakati wake kile atakachofanya.

**Com. Barasa:** Yani kuwe na vyama viwili?

**Mali:** Kuwe na vyama vingine viwili, hata kama vile vingine vitakuako lakini ule wakati wa election kichaguliwe tu kile kimoja ambacho kiko strong kushinda wenzake na kile ambacho kinachosikia, tunataka viwe viwili tu, vile vingine kama vinaonekana havina powers viondolewe, visisimamishwe.

Jambo lingine la pili ni kuongezea kama hii mambo ya shule. Kwanzia standard one mpaka eight, alafu form one mpaka form four kuna kuwa na cost sharing wagawanye hizo pesa.

Jambo lingine ambalo pia nilikuwa nataka kuzungumzia ni hili la bara bara hasa wakati serikali inapanga budget zake na pengine district hii imepeana bara bara fulani kama millioni tano wakati imepatiwa contractor, kufanywe kamati kuhusu hiyo line, kama ni wazee au vijana waangalie huyo contractor kama anafanya kazi nzuri. Kama ile kazi inafanywa lakini ni mbaya afadhali kazi isimamishwe waangalie contractor mwingine lakini hiyo naona pengine wabunge pekee yao wanaangalia kwa sababu ata wewe bwana commissioner we umekuja na ukaona vile murram imewekwa. Ile murram nafikiri iko na miezi sita dakika hii. Na hiyo ni ajabu inaweza kuondolea na maji na ukute pesa zilienda, simuelewi na hakuna kitu kingine kimefanywa itapitishwa tu kuwa bara bara imewekwa murram. Afadhali iwekwe kamati itakuwa nayo, ile kamati ya 90 inachunguza ule contractor anafanya kazi nzuri ama la. Kama haifai ule contractor wapeane hiyo contract kama contractor hafai, anapokonywa ipatiwe contractor mwenye uwezo zaidi ya kutengeneza bara bara. Bara bara ya wananchi sasa, sawa sawa tukaribie wananchi na ikiwa mbaya tikiti inakua juu.

Point ingine ambayo tulikua tunazungumza ni kuhusu hali ya risala. Nafikiri kungekua na commissione special wakati bunge pengine wanataka kama ni bunge kuzungumza mambo ya mshahara kuongezwa mshahara iwe inaongezwa kwa wafanyi kazi wote wa serikali. Rather than ile ya kua unakuta pengine watu kama kuna wizara zingine zilikuwa ziko kwa serikali zikatolewa zikawekwa kwa parastatal sasa utakuta kama yule mtu pengine alienda university ukiangalia ile salary yake na yule ambaye ako parastatal unakuta oh mshahara wao uko juu, nyinyi ambao pengine mlikuwa mnafanya naye mlichukua job group moja, uliachwa pale pale we uko. Kama ni chama pengine ni kitu kupunguzwa kama mshahara ipunguzwe kwa jumla kama ni serikali kuongeza inaongezwa kwa jumla alafu serikali ijaribu kucontrol kitu. Hivi vitu ambavyo vinaanzwa serikali ijaribu kuangalia, kucontrol maana ikiwaciliwa inaonekana wananchi akaenda tonea zaidi. Kwa hivyo serikali ijaribu kucontrol hizo vitu. Na pia

tungeomba hii VAT iondolewe maana ndiyo inaumiza zaidi. VAT hio iondolewe kwa sababu ndiyo inaumiza zaidi.

Kulingani na hii sheria inayozorota na VAT, iko mwananchi wa kawaida ndiyo inaumiza sana na kulingana na kuwa hujui ile hesabu inafanywa muhindi anakufanyia hesabu ya kifuu juu tu ana kuambia serikali yako mwenyewe ndiyo inataka namna hiyo. Kwa hivyo nafikiri hiyo ingeondolea itakuwa bora zaidi.

Alafu ingine ni ile ya maskwota. Naona katika Coast Province Squatters wamezidi. Naona Sudan kam pengine kuna provinces ata kama ziko sidhani lakini ata kama kuna provinces zingine zimezidi squatters kama Coast province, kwa sababu mwananchi ambaye amezaliwa hapa pengine mimi baba yangu, amezaliwa hapa mpaka dakika tunaambiwa hiyo kitu nio crown land. Lakini katika hiyo crown land unakuta wale viongozi amba wanapitisha wanapita na juu wanafika kuta hiyo plot ambayo unakaa ya commissioner of lands hajui yalipelekwa tu karatasi na iko na kila kitu. Sasa wewe unakaa unajua serikali itakuja nyang'anya mahali na ikupatie 'mahali' na kumbe mahali palichukuliwa kitambo. Kitu kama hii ningefurahi kama kingegeuzwa kikawekwa kwa laini mzuri ingekua mzuri sana. Nafikiri sina zaidi na kwa machache nasema asante sana.

Ingine ni hii ilikuwa ikizungumzwa kwa wingi sana mambo hii ya mnazi. Ni kweli kulingana na mnazi ni mti alafu tunaudhamini sana katika Coast province. Mnazi si kitu ya kuleta pesa nyingi sana. Vitu ambavyo tunauza pesa ndogo ndogo na katika ile maji yake ambayo watu hutumia sana ndiyo ambayo wanategemea zaidi. Tunaiomba iwachiliwe halafu wale watu watakuwa wanauangalia iwe na watu kama public health wawe wanaangalia usafi wa vile vitu kwa sababu ata wale watalii kule Diani unakuta wengi wanapenda kwenda kwa sababu ya mambo ya polisi kwa sababu watachukua sambuli ya mnazi lakini nao wanapendelea kunywa ile local brew yetu.

**Com. Barasa:** Pengine itaharibika.

**Mali:** What, wanakunywa kwa vile wanateswa na wale beach boys na ukipatikana na polisi unashikwa. Mama lakini watu wanataka hiyo kitu, kwa hivyo soko ata ile itaharibu iwekwe time ya kuwa watu watatumia kawaida isio ya licence iwe tu wapate place wanatembelea wale watu kama ni club inatembelea wale watu inaangalia usafi wa ile mahali. Ikifanyiwa namna hiyo ata industry itafanyiwa. Itapitishwa kwa sababu kutatokea mgeni mwingine aanze hiyo kitu aifanyie utafiti na ilete kitu na ikilete haitaleta Coast pekee yake itakuwa inalete Kenya nzima.

Meeting Ended at 5.30 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&